BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao sha Saba - Tarehe 19 Juni, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 60

Fedha za *Road Toll*

MHE. MGANA I. MSINDAI aliuliza: -

Kwa kuwa sasa hivi Serikali ya Awamu ya Tatu inajitahidi kutoa fedha za *Road Toll* kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Serikali Kuu na za Halmashauri za Wilaya; na kwa kuwa baadhi ya fedha hizo hupelekwa moja kwa moja kwa Mameneja wa *TANROADS* Mikoani na nyingine kwenye Halmashauri za Wilaya kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na kwa kuwa barabara za Mikoa hutengenezwa vizuri zaidi kuliko zile za Halmashauri za Wilaya kwa kiwango kile kile cha fedha:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo na ina utaratibu gani wa kubadilisha utaratibu huo?

(b) Kwa kuwa kuna baadhi ya Halmashauri zenye Wahandisi wasio bora wanaoshinikiza Makandarasi wasio na vifaa wapewe kazi hizo na kwa kuwa Watendaji yaani Wahandisi na Wakurugenzi wakiharibu kazi mahala fulani, huhamishiwa kwenye Halmashauri nyingine; je, Serikali kwa kufanya hivyo haioni kwamba inalea ubovu na inachukua hatua gani kutatua matatizo kama hayo yanapotokea?

(c) Kwa kuwa baadhi ya Halmashauri hazitoi taarifa ya matumizi ya fedha hizo jambo linalosababisha Serikali ishindwe kutoa fedha hizo kama ilivyotokea kwenye Wilaya ya Kiteto na kadhalika, je, kwa nini Serikali isichukue hatua kwa wahusika badala ya kuwaacha Wananchi wa maeneo hayo kuendelea kuumia kwa kukosa barabara nzuri kwa ajili ya uzembe wa mtu mmoja?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu ulivyo hivi sasa kuhusu mgawanyo wa Fedha za Mfuko wa Barabara ni kwamba 70% ya Fedha za Mfuko huo hugawiwa kwa Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wake wa Barabara *(TANROADS)* kwa ajili ya kuhudumia km. 35,000 za mtandao wa barabara za Kitaifa na Kimkoa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hupata 30% tu kwa ajili ya kuhudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa km 50,000 ili angalau sehemu kubwa iweze kupitika ukizingatia ukweli kwamba barabara nyingi zilizo chini ya ofisi hii zilikuwa kwa muda mrefu hazipatiwi huduma ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, nia ya maelezo haya ni kumsaidia Mheshimiwa Mbunge, kujua tu kwamba iwapo anaona barabara za Mikoa zinatengenezwa vizuri zaidi kuliko zile za Halmashauri za Wilaya hali hiyo inatokana na tofauti za viwango vya mgao wa fedha, tofauti za urefu wa mtandao wa barabara, uwezo mdogo wa Makandarasi katika ngazi ya Wilaya na historia ya matengenezo duni ya barabara hizo siku zilizopita, pamoja na uwezo mdogo wa kitaalam katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haioni sababu za kubadilisha utaratibu huu badala yake ofisi yangu itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuongeza uwezo wa Halmashauri na Makandarasi waliopo hususan katika maeneo ya utaalum na upatikanaji wa vifaa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haihamishi mtumishi yeyote aliyeharibu kazi kutoka kituo kimoja hadi kingine kwani ilishatoa taarifa rasmi kuhusu utaratibu utakaofuatwa. Mtumishi yeyote atakayeharibu kazi atachukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na taratibu zilizopo pale pale kwenye kituo chake cha kazi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2000, ofisi yangu imeimarisha Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kuwapatia Wahandisi wenye vyeti vinavyotambulika *(Graduate Engineers)* ili kuongeza ufanisi wa kazi zao. Idadi ya Wahandisi imeongezeka kutoka 76 mwaka 2001 na kufikia Wahandisi 113 mwaka 2003.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekuwa ikiwahimiza Wakurugenzi wa Halmashauri husika kwamba ni lazima wawasilishe taarifa za utekelezaji zinazoonyesha matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara wanazopelekewa. Bodi ya Mfuko wa Barabara imekuwa ikisitisha upelekeji wa fedha kwa zile Halmashauri zilizoshindwa kuwasilisha taarifa ya matumizi.

Hata hivyo, pamoja na adhabu hiyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekuwa ikiwachukulia hatua za kinidhamu Watendaji wa Halmashauri ambazo zimeshindwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji kulingana na fedha zilizotumika. *(Makofi)*

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa sababu yeye mwenyewe amekiri kwamba sababu mojawapo inayofanya barabara zisitengenezwe vizuri ni uhaba wa utaalam na kwa vile maeneo mengi Wahandisi wa Barabara walioko Wilayani hawana sifa:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi kuwaondoa hawa wasio na sifa wawaweke wenye sifa?

(b) Kwa kuwa Wilaya 15 mwaka 2003 wa fedha zilishindwa kupeleka taarifa na ikapelekea Halmashauri husika kunyimwa fedha ikiwepo Halmashauri yangu; je, Serikali imewachukulia hatua gani Wahandisi hao? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tumekuwa na mapungufu ya Wataalam Wahandisi katika Halmashauri zetu ambao wangeweza kuboresha zaidi kazi zetu katika Halmashauri. Lakini kama nilivyosema katika majibu yangu, zoezi la kurekebisha hiyo hali limekuwa likiendelea kwa kipindi cha karibu mwaka mzima na zaidi sasa na ndiyo maana nimesema idadi ya *Graduate Engineers* sasa imepanda kutoka 76 mpaka 113 na zoezi linaendelea.

Vile vile tunachukua taratibu za kutoa semina mbalimbali kwa ajili ya Makandarasi hawa ambazo zinaendeshwa na Bodi ya Makandarasi katika kujaribu kuwasaidia. Kwa hiyo, kwa kweli zoezi linaendelea na tunafikiri baada ya muda si mrefu tutakuwa tume-*replace* wale *technicians* karibu wote na Wataalam hawa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna Halmashauri 15 ambazo zilishindwa kuwasilisha taarifa zao kwa wakati na hivyo tukalazimika kuchukua hatua za kuwabana kwa kuagiza kwamba hawatapata mkupuo mwingine wa fedha mpaka kwanza watoe maelezo.

Kwa hiyo, tuliwapa muda hadi Desemba 2002 na wote walitekeleza wakaleta taarifa zao *by December* na Halmashauri zote hizo 15 zimepata fedha ambazo tulikuwa tumesimamisha kwa muda katika juhudi za kujaribu kubanana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tungeweza kuchukua hatua za ziada, lakini vile vile, wakati mwingine tunazingatia mazingira ya Halmashauri zetu na uwezo ambao tunajaribu kuujenga.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, zilikuwepo Halmashauri nyingine tatu ambazo nazo zilikuwa zimepata tatizo kwa kuhamisha matumizi ya zile fedha, lakini naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa Halmashauri hizo, hatua zimeishachukuliwa na fedha zimeishakuwa- *released* kwa ajili ya Halmashauri hizo zote tatu. *(Makofi)*

STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ametoa taarifa kwamba sasa namba ya *Engineers* imeanza kuongezeka na tatizo moja kubwa katika eneo hili ni Watumishi na hili jambo linaonekana linaweza kuwa ndani ya uwezo wa Wizara.

Je, Wizara inasemaje kuhusu namna ya kutupatia *engineers* wa kutosha na wanaofaa ili waweze kufanya kazi katika Halmashauri zetu?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyojibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kweli kabisa kwamba Serikali inachukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba Halmashauri za Wilaya zinapata Wahandisi walio na *qualifications.*

Kulingana na Sheria Na. 15 ya mwaka 1997 ambayo inahusu *Engineers Registration Board,* inasema wazi kabisa kwamba: "Mhandisi ambaye hajawa *registered* hatakiwi kufanya kazi zozote za kihandisi." Lakini pia kutokana na *Section* Na. 14 ya Sheria hiyo hiyo inasema wazi kwamba: "Mwajiri yeyote akimwajiri Mhandisi ambaye hajasajiliwa nalo ni kosa."

Kutokana na taarifa ambazo zilifanywa na *Engineers Board* mwaka 2002 iligundua kwamba katika Halmashauri 114 ambazo zilikaguliwa zilikuwa na Wahandisi 211 na katika hao, Wahandisi 20 hawatakiwi kabisa kuitwa Wahandisi kwa sababu hawana *qualifications* zozote. Katika Wahandisi hao, wawili wako Mkoa wa Kagera, wawili wako Mkoa wa Lindi, mmoja yuko Mbeya, mwingine mmoja yuko Mkoa wa Morogoro, mmoja yuko Mkoa wa Mtwara, watano wako Mkoa wa Pwani, wawili wako Singida, mmoja yuko Mkoa wa Tanga, mmoja yuko Dar es Salaam na wanne wako Dodoma. Katika ambao hawatakiwi kuwa *registered.... (Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, nashukuru, tuzingatie muda. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili la Wahandisi limekuwa ni kilio cha Wabunge karibu wote nchi nzima na Wilaya yangu ina tatizo la Mhandisi ambaye

alihamishwa kutoka sehemu moja akaletwa pale na suala hili liko mikononi mwenu kama Wizara.

Je, Wizara inafanya kazi ipi ili kuweza kuhakikisha kwamba Mhandisi huyu anachukuliwa hatua zinazostahili?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba suala hilo alikwishaliwasilisha kwenye ofisi yetu na nimuahidi kwamba tutalifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba tunarekebisha hiyo kasoro ambayo ipo na tayari zoezi limekwishaanza. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba baada ya muda si mrefu tutatatua tatizo lake.

Na. 61

Mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya

MHE. HASSAN C. KIGWALILO aliuliza: -

Kwa kuwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni viungo muhimu kiutawala na kwa kuwa hakuna mafunzo maalum wanayopatiwa ili kuwawezesha kumudu kazi na wajibu wao vizuri zaidi: -

(a) Je, Serikali haioni kwamba kwa kutowapa Wakuu hao mafunzo ya Utawala na Uongozi kunaathiri ufanisi wa Utawala na Uongozi Bora Serikalini?

(b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kutoa Mafunzo ya Utawala na Uongozi unaohitajika kwa nyadhifa hizo?

(c) Je, kwa nini Serikali ilisitisha Mafunzo ya Viongozi hao yaliyokuwa yanatolewa na Chuo cha Maendeleo ya Uongozi - Mzumbe tangu wakati wa ukoloni?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kutowapa mafunzo ya Utawala Bora Wakuu wa Mikoa na Wilaya kunaweza kuathiri utendaji wa kazi zao. Kuanzia miaka ya 1990 Serikali kwa kweli haikuwa na utaratibu wa kuwapatia mafunzo maalum Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Hii ilitokana na ufinyu wa Bajeti wakati huo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa mabadilikio mengi katika mifumo ya kijamii na kiuchumi Serikali imekuwa na mipango ya kutoa tena mafunzo mbalimbali kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Mwaka 2001/2002 Serikali iliandaa

mafunzo maalum ya mwezi mmoja katika Chuo cha *ESAMI* ambapo Wakuu wa Mikoa walijifunza Menejimenti ya Sekta ya Umma pamoja na teknolojia ya mawasiliano na mtandao kwa kutumia kompyuta.

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo yalifuatiwa na mafunzo ya wiki 3 nchini Ireland ambapo Wakuu wa Mikoa walipatiwa mafunzo yaliyohusu Majukumu ya Serikali, Masuala ya Maendeleo, Mabadiliko ya Kisiasa na Kiuchumi Duniani, Uwajibikaji, Uongozi na Utawala Bora.

Aidha, mwezi Novemba 2002, ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ilitoa Mafunzo ya Uongozi na Utawala ya wiki moja kwa Wakuu wa Wilaya wote Wanawake yenye lango la kuboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaandaa mafunzo maalum ya miezi mitatu ambayo yatatolewa kwa Wakuu wa Wilaya wote kuanzia mwezi Agosti mwaka 2003. Wakuu hao wa Wilaya watapatiwa mafunzo ya awali kuhusu shughuli za Mkuu wa Wilaya pamoja na kuwapa mafunzo ya stadi za kazi yakiwemo mafunzo kuhusu Uongozi na Utawala Bora.

(c) Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Viongozi yaliyokuwa yanatolewa na Chuo cha Maendeleo ya Uongozi - Mzumbe kuanzia ukoloni na hata baada ya Uhuru yalisitishwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

Vile vile, Chuo hicho kimebadilisha mwelekeo wake wa kutoa mafunzo. Hata hivyo, Serikali kati ya miaka ya 1980 na 1990 ilikuwa bado inaendesha semina za wiki mbili, mbili, kwa Wakuu wa Wilaya ili kuwapa elimu mbalimbali kuhusiana na majukumu hayo. Serikali itaendelea kutazama eneo hilo la mafunzo kwa Viongozi hawa ili waweze kuboresha utendaji wao wa kazi.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Ningependa kujua mpango ulioelezwa ni wa kudumu ama ni wa kutegemea wafadhili kwa mafunzo ya Wakuu hawa?

(b) Nini kiwango cha chini cha kuweza wao kuteuliwa kuwa ma-*DC* au kuwa Wakuu wa Mikoa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu huu kama ni wa kudumu au hapana, tunachoweza kusema ni kwamba, hizi ni juhudi ambazo Serikali imeanza hivi sasa. Nia ni kwamba uwe ni utaratibu wa kudumu na Mheshimiwa Rais amekwishatoa maagizo na

sasa suala hilo linafanyiwa kazi kuwa na utaratibu ambao utakuwa ni wa uhakika zaidi. Lakini naomba ni-*caution* tu kwamba, kwa sehemu kubwa mambo haya ya *training* ni gharama kubwa, kwa hiyo, huenda hapa na pale tukakwama kutokana na ufinyu wa Bajeti, lakini nia ya Serikali ndiyo hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu viwango ambayo mtu anapaswa kuwa navyo ili aweze kuteuliwa kuwa *DC,* swali hili si jepesi sana kulijibu. Kama mnavyojua, Wakuu wa Wilaya ni Viongozi wa Kisiasa na wanateuliwa na Mheshimiwa Rais, yanayotazamwa ili kuweza kumteua mtu kuwa *DC,* si elimu peke yake, lakini yako mambo ya *leadership* na masuala mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Na. 62

Ucheleweshaji wa Mizigo Bandarini

MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME aliuliza: -

Kwa kuwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kwa wananchi na wafanyabiashara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam kwamba kumekuwako na ucheleweshaji wa utoaji wa mizigo hasa magari na makontena ya mizigo hadi kufikia muda wa mwaka mmoja na zaidi na wengine kushindwa kukomboa: -

(a) Kwa kuwa utaratibu huo umeleta bughudha na lawama zisizo na msingi; je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo kwa wananchi?

(b) Je, Serikali inaona kuna umuhimu au ulazima wa urasimu huo ambao unaangusha hali ya kitengo chetu kinachotegemewa sana hapa nchini?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuwapeleka watendaji wa Taasisi hiyo Zanzibar kuona jinsi wenzao wanavyofanyakazi kwa wakati na kwamba tatizo hilo kule Zanzibar halipo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, lenye vipengele (a), (b) na (c), napenda kueleza kwamba shughuli za utoaji mizigo bandarini huhusisha Taasisi mbalimbali kama vile Wakala wa Meli wa Mizigo, Mamlaka ya Bandari, Mamlaka ya Mapato, Makampuni ya Ukaguzi na waagizaji wenyewe.

Vile vile ili kuhakikisha kwamba ubora wa bidhaa zote zinazoingia ndani unazingatiwa, Mamlaka ya Mapato inafanya kazi kwa karibu sana na Taasisi kama *TBS,* Kamisheni ya Taifa ya Mionzi, Bodi ya Taifa ya Madawa, Kamisheni ya Udhibiti wa Ubora wa Chakula, Kituo cha Udhibiti wa Madawa ya Kilimo, Idara ya Maliasili, Tume

ya Taifa ya Kuzuia Madawa ya Kulevya na Bodi mbalimbali zinazohusika na kuruhusu uingizaji na utoaji bidhaa fulani fulani hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa utoaji wa mizigo bandarini huchangiwa hasa na waagizaji kutotoa taarifa sahihi na vielelezo vinavyokidhi mahitaji ya mamlaka husika. Taarifa zinazowasilishwa kuhusiana na kiasi cha bidhaa iliyoagizwa na thamani yake mara nyingi huwa siyo sahihi. Pamoja na hilo ucheleweshaji unajitokeza kwa sababu ya kutekeleza matokeo ya Sheria mbalimbali zinazohusu udhibiti wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mbunge wa Kitope, kama ifuatavyo: -

(a) Juhudi zinafanywa kupitia *National Shipping Forum* kwa kuwashirikisha wadau wote kutafuta njia ya kuboresha mfumo mzima. Hatua za awali zimeshachukuliwa ili kupunguza mlolongo uliopo, kwa mfano Idara ya Forodha, Bandari ya Dar es Salaam na Kitengo cha Makontena vimeunganishwa kwa mtandao wa kompyuta ili kurahisisha utendaji baina ya Taasisi hizi. Vile vile, *TRA* inaboresha mfumo wake wa sasa wa *Automated System of Customs Data (ASYCUDA)* ili kuoanisha na mifumo ya wadau wengine ili kuleta ufanisi zaidi.

(b) Serikali inatambua na inathamini mchango wa Sekta ya Biashara ya Nje na inafanya kila liwezekanalo kuondoa taratibu zinazosababisha urasimu usio wa lazima.

(c) Ni kweli kwamba utoaji wa mizigo bandarini Zanzibar hufanywa kwa makini na kwa haraka zaidi ikilinganishwa na Bandari ya Dar es Salaam. Kwa kutumia uzoefu wa sehemu mbalimbali ikiwemo Zanzibar, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania inafanya kila liwezekanalo kuona kwamba bandari zote zinakuwa na ufanisi wa kutosha katika kutoa huduma.

MHE. ISSA MOHAMED SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kasema kwamba kweli kuna mlolongo wa Taasisi nyingi pale bandarini unaosababisha urasimu.

Je, Serikali haioni kwamba sasa hivi ni wakati muafaka wa kupunguza Taasisi hizi ili kuondoa urasimu huu katika bandari ile ili watu wasipate usumbufu? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, kila Taasisi iliyoundwa, imeundwa kwa Sheria ambayo tumeitunga sisi hapa Bungeni na kila Taasisi inafanya kazi zake kwa mujibu wa kuhifadhi na kuhakikisha kwamba zile bidhaa zinazoletwa nchini zinaletwa kwa mujibu wa Sheria tulizozitunga wenyewe humu Bungeni.

Kwa hiyo, si rahisi kusema kwamba Taasisi zile nyingine ziondolewe, ukisema unaondoa Taasisi ya Dawa za Kulevya una uhakika gani kwamba zile bidhaa zinazoletwa hamna dawa za kulevya? Ukisema unaondoa *TBS* una uhakika gani kama chakula

kinacholetwa kina-*fit for human consumption?* Kwa hiyo, si rahisi kwa Taasisi hizo kutofanya kazi kwa mujibu wa Sheria zilizowekwa.

MHE. FRANK G. MAGOBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria ndiyo kikwazo katika kutoa mizigo bandarini na ndiyo maana Wananchi wanapata taabu kweli kwa ajili ya kutoa mizigo yao.

Je, ni taratibu gani zinaandaliwa au zinafuatwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa Watanzania ambao wanaagiza mizigo kupitia bandari hii ili wasikiuke Sheria? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* hivi sasa inatoa mafunzo mbalimbali juu ya kodi katika kila Wilaya.

Tatizo kubwa tulilonalo ni kwamba wafanyabiashara wengi huwa hawahudhurii katika semina hizi zinazotolewa Wilayani kwa wafanyabiashara mbalimbali, badala yake tumegundua mara nyingi wanaopelekwa ni wale wafanyakazi ambao hawawezi kabisa kuwawakilisha vilivyo wale wafanyabiashara, hapo ndiyo matatizo yanapotokea. Lakini katika kila Wilaya, *TRA* inafanya kazi hiyo ili kuwaelimisha wafanyabiashara namna ya kutoa mizigo, namna ya kulipa kodi na kodi mbalimbali zinazowahusu.

Na. 63

Kima cha Chini cha Pensheni ya Wastaafu

MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR aliuliza: -

Kwa kuwa katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2002/2003 ilitenga fedha si chini ya bilioni 6 kwa ajili ya kuboresha kima cha Pensheni ya wastaafu: -

(a) Je, uboreshaji huo ulilenga kwenye kima cha chini cha kuanzia shilingi ngapi?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilishatolewa kwa lengo hilo tangu fedha hizo zipitishwe?

(c) Je, hadi sasa ni wastaafu wangapi hawajapata boresho hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mbunge wa Mwembe-Makumbi, naomba kwanza nitoe maelezo ya jumla kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba kila mwaka hali ya uchumi ikiruhusu, kima cha chini cha pensheni ya kila mwezi kinaboreshwa ili kumwezesha mstaafu amudu baadhi ya gharama za maisha. Hata hivyo, kiwango kilichoahidiwa na Waziri wa fedha katika hotuba ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2003/2004 ili kuboresha kima cha chini cha pensheni ya wastaafu kilikuwa kisichozidi shilingi bilioni 1.15 kwa ujumla na siyo shilingi bilioni 6 kama ilivyoelezwa katika swali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa kima cha chini cha pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu wetu ulilenga kwenye kima cha chini cha kuanzia shilingi 72,000/= kwa miezi sita ikilinganishwa na shilingi 24,000/= kwa miezi sita huko nyuma. Utekelezaji wa hatua hii ulianza tarehe 01 Julai, 2002 kama ilivyoelezwa katika kifungu Na. 30 cha *The Public Service Retirement Benefits (Minimum Pension) Order, 2002.*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ni chombo kinachofanya shughuli zake bila kujilimbikizia faida. Serikali hutoa huduma kwa wananchi wake kwa ajili ya kuboresha maisha yao. Hivyo, katika kuongeza viwango vya pensheni nia ya Serikali ni kutaka wastaafu wake waboreshe maisha yao. Nia ya Serikali itaendelea kutekelezwa kila wakati hali ya uchumi wake inaporuhusu kufanya hivyo.

(c) Ongezeko hilo la kima cha chini ni kwa ajili ya wastaafu wote isipokuwa wale waliokuwa wameomba na kulipwa pensheni zao za kila mwezi kwa mkupuo ambao idadi yao ni 173.

MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 baadhi ya wastaafu walikosa malipo hayo. Je, wale waliokosa watalipwa *arrears* pamoja na mafao ya mwaka 2003/2004 yanayoendelea?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, hata hao waliokosa haki yao bado ipo, watalipwa tu. Kama *cheque* ilikwisha chacha ni wajibu wao warudishe *cheque* ile na fedha zao watapewa. Hakuna atakayekosa haki yake ya msingi ya pensheni ya kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama yupo arudishe *cheque* iliyochacha na atalipwa fedha zake, hazipotei. *(Makofi)*

Na. 64

Soko kwa Ajili ya Zao la Muhogo

MHE. HASNAIN M. MURJI (k.n.y. MHE. LYDIA T. BOMA) aliuliza: -

Kwa kuwa zao la muhogo limekuwa likilimwa sana katika Mikoa ya Kusini na huko nyuma wakulima waliweza kuzalisha kwa wingi na kujipatia fedha kwa ajili ya mahitaji na kuondoa matatizo yao na kwa kuwa zao hilo kwa sasa halina soko kabisa na kutumika sehemu ndogo kwa chakula: -

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuanzisha kiwanda Mtwara cha kutengeneza biskuti kutokana na unga wa muhogo?

(b) Kwa kuwa inasemekana kuwa wanga mzuri unatokana na muhogo; je, kwa nini Serikali isimtafute mwekezaji wa kutengeneza wanga ili uweze kutumika hapa nchini na pengine nchi za nje?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo niliwahi kueleza katika jibu langu la swali Na. 4 la Mheshimiwa Hasnain Murji, tarehe 12 Juni, 2001, soko la zao la muhogo linakabiliwa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, lakini utafiti uliofanywa na Kituo cha Utafiti wa Zao la Muhogo kilichopo Kibaha, kwa kushirikiana na Kampuni mbili za kutengeneza biskuti za Azam na Bibi, umebaini kuwa unga wa muhogo unaweza kuchanganywa na unga wa ngano katika utengenezaji wa biskuti kwa uwiano usiozidi 20% unga wa muhogo na 80% unga wa ngano. Uwiano wa unga wa muhogo unaozidi 20% hutoa bidhaa ambazo hazipendwi na walaji.

Kwa kuzingatia mahitaji ya uwiano huu, wawekezaji wengi hushawishika kujenga viwanda vya biskuti katika maeneo ambayo upatikanaji wa unga wa ngano ni rahisi ukilinganisha na upatikanaji wa muhogo tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanga, ili wawekezaji waweze kujenga kiwanda cha kutengeneza wanga kwa kutumia zao la muhogo, mahitaji yafuatayo hayana budi kuwepo: -

(i) Kiwanda kiwe karibu na bandari ikiwa uzalishaji utalenga soko la nje.

(ii) Kiwanda kiwe na shamba au wakulima wakubwa na wadogo ambao watazalisha muhogo wa kutosha katika kipindi chote cha mwaka.

(iii) Uzalishaji wa wanga unahitaji maji mengi na safi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za kuboresha mazingira na mahitaji ya ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi ya muhogo kama hivi vilivyotajwa na

Mheshimiwa Mbunge, Serikali inawashauri wakulima wa muhogo kutumia teknolojia rahisi ya kukausha makopa ya mihogo kwa kutumia mashine ambazo zimefanyiwa utafiti na kuendelezwa na kituo cha utafiti wa zao la muhogo kilichopo Kibaha. Makopa ya muhogo yaliyokaushwa kwa njia hiyo, yana soko kubwa katika nchi za Botswana na Afrika ya Kusini ambapo hutumika katika kutengenezea chakula cha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina nafasi kubwa ya kuuza katika soko la nje endapo uzalishaji utafikia kiwango cha ubora unaohitajika katika masoko hayo. Tunashauri uongozi wa Serikali Mkoani Mtwara uwasiliane na Wizara yetu ya Ushirika na Masoko, pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, ili kuweka mikakati itakayohakikisha kuwa azma hii inafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile inahamasisha matumizi ya zao la muhogo katika soko la ndani, ikiwa ni pamoja na matumizi kama chakula cha binadamu na kutengenezea chakula cha mifugo. Hatua hizi zinalenga katika kukuza soko zao la muhogo na hivyo kuwaongozea kipato wakulima wa zao la muhogo. *(Makofi)*

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Mkoa wa Mtwara Wilaya inayolima muhogo kwa wingi ni Wilaya ya Newala na kwa kuwa Tarafa ya Chilangala haina zao mbadala zaidi ya muhogo na kwa kuwa kuna Kampuni ya *HOLBAT Tanzania Limited* ya kutoka Kenya ilikuwa inanunua muhogo na kusafirisha Ujerumani na kwa kuwa sasa takribani miaka minne kampuni hiyo imesimama kusafirisha muhogo huo:-

(a) Je, Serikali iko tayari sasa kutufanyia utafiti kwa nini kampuni imesitisha kusafirisha muhogo kupeleka Ujerumani?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba muhogo unaweza ukatumika kama chakula cha binadamu, je, sasa Serikali iko tayari kununua muhogo huo na kupeleka katika Hifadhi ya Taifa ya Chakula? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hasnain Murji, Mbunge wa Newala, kama ifuatavyo:-

La kwanza kuhusu kampuni ambayo ilikuwa inanunua muhogo kutoka Newala na sasa hivi imesitisha, anataka kama tunaweza tukafanya utafiti kwa nini kampuni hiyo imesitisha ununuzi wa muhogo. Serikali inaendelea na utafiti wa kutafuta masoko ya mazao mbalimbali ukiwepo pamoja na muhogo.

Kwa hiyo, kama kampuni hiyo ilikuwa inanunua muhogo huko nyuma na sasa hivi, imesitisha Serikali iko tayari kuendelea kufuatilia ni kwa nini kampuni hii ilisitisha ili sababu zitakazokuwa zimebainika ili tuweze tukawaelesha wakulima.

Kuhusu kununua muhogo kupeleka katika Akiba ya Taifa. Nilipokuwa nikijibu swali la Mheshimiwa Hasnain Murji, huko nilikuwa nimeeleza juu ya suala la muhogo jinsi ambavyo soko lake ni gumu kwa sababu matumizi yake yanaingiliana na matumizi ya nafasi zingine kama, vile mahindi, mtama na kadhalika.

Kwa hiyo, tulichokuwa tumeshauri tukasema tu kwamba muhogo unaolimwa Mtwara uweze kuwa unaandaliwa vizuri kwa kuanikwa vizuri ili kuweza kutafuta wanunuzi ambao wanaweza wakaununua kwa matumizi mbalimbali kama nilivyokuwa nimeeleza hapo awali. *(Makofi)*

MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuwa anajibu swali alitaja kwamba Botswana liko soko la muhogo na kwa kuwa yeye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Ushirika na Masoko, anatusaidiaje sisi watu wa Mtwara kuufikisha muhogo huko Botswana, Serikali itasaidiaje hili? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama nilivyokuwa nimejibu katika swali la msingi nilisema kwamba soko la muhogo linapatikana huko Afrika ya Kusini pamoja na Botswana na katika maelezo ya ziada nilieleza kwamba Mkoa wa Mtwara uweze kuwasiliana na Wizara yetu ili kuweza kufanya utafiti wa kupatikana kwa muhogo ambao ni bora zaidi bila shaka ili tuangalie na njia za kuweza kuufikisha huko kama uwingi utakuwa unahitajika kuweza kukidhi masoko yanayohitajika huko Botswana.

Na. 65

Ufufua wa Vyama vya Ushirika

MHE. GEORGE F. MLAWA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina ari kubwa ya kufufua Vyama vya Ushirika hasa Vyama vya Msingi na kwa kuwa wakati Vyama vya Ushirika vilipopoteza nguvu na uhai Serikali iliwastaafisha Maafisa Ushirika wengi ambao walikuwa na ujuzi na uzoefu mkubwa wa kuendesha vyama hivyo na kuwa kwa wakati huo, maafisa wenye ujuzi, uzoefu na ari walikuwa ni wachache sana.

Je, Serikali haiwezi kuwaajiri kwa mkataba baadhi ya Maafisa Ushirika hao waliostaafu kabla ya muda wao ili jamii iweze kunufaika na huduma zao na hivyo kuleta msukumo mkubwa wa kufufua Vyama vya Ushirika na hasa Vyama vya Msingi?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Mlawa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuwastaafisha Maafisa Ushirika lilifanyika mwaka 1994 likiwa ni sehemu ya zoezi zima la Serikali la kupunguza matumizi yake. Hivyo siyo sahihi kusema kwamba Maafisa Ushirika walistaafishwa wakati Vyama vya Ushirika vilipopoteza nguvu na uhai kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema.

Kwa kuwa kigezo kinachotakiwa cha idadi ya Vyama vya Ushirika, anavyopaswa kuvisimamia Afisa Ushirika mmoja ni vyama 7; na kwa vile kwa sasa kwa wastani Afisa Ushirika mmoja husimamia zaidi ya vyama 11, Serikali imekwishatambua umuhimu wa kuongeza idadi ya Maafisa Ushirika na tayari kibali cha kuongeza ikama ya Maafisa Ushirika 300 kimeombwa.

Kwa kuwa taratibu za utumishi wa umma haziruhusu mtumishi aliyepunguzwa kazi kuajiriwa tena katika utumishi, nafasi zitakazopatikana zitajazwa na watumishi wapya, wenye sifa zinazotakiwa. Chini ya utaratibu huo, maafisa Ushirika wapatao 46 wameaajiriwa kati ya mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, idadi ya maafisa 300 ikikamilika inategemewa kuwa huduma za usimamizi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi itakuwa imeboreshwa na jamii inaweza kunufaika na ubora wa huduma hiyo ambayo inategemewa kuleta msukumo mkubwa wa kufufua, kuimarisha na kuviendeleza Vyama vya Ushirika hapa nchini.

Aidha, ili kukuza stadi za maafisa hao na hivyo kuinua ubora na uwezo wa Maafisa Ushirika katika kuhudumia Vyama vya Ushirika, Wizara kupitia Chuo cha Ushirika Moshi, inaendesha mafunzo ya Elimu ya Ushirika Shirikishi kwa Maafisa Ushirika. Hadi sasa Maafisa Ushirika 94 wamepata mafunzo hayo. Lengo la mpango wa elimu shirikishi ni kuwawezesha maafisa waliopata mafunzo na kuweza kueneza ushirika huo kwa wananchi wote kwa ujumla.

MHE. GEORGE F. MLAWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza kama ifuatavyo:

Kwa vile kuwafunza Maafisa Ushirika wapya itachukua muda mrefu mpaka kupata kuweza kutosheleza mahitaji. Je, haiwezekani kwa sasa kutoa mafunzo maalum na kuwatumia maafisa walioko huko vijijini hasa Maafisa Kilimo, Mifugo, Maendeleo ya Jamii kufanya kazi hii ya ushirika ili kuweza kuharakisha ufanisi wa Vyama vya Ushirika hasa Vyama vya Msingi?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Mlawa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilichokisema katika kujibu swali la msingi nilisema kwamba, tuna zoezi la kuajiri Maafisa Ushirika 300 na tunategemea kwamba kama zoezi litakwenda kama tulivyokusudia kazi hii inaweza kuwa imeshakamilika katika kipindi cha miaka mitatu hivi.

Kwa hiyo, hatuwafunzi ili tuweze kuwaajiri, isipokuwa tutawaajiri wale ambao tayari wana uzoefu. Mafunzo niliyoyaeleza ni kwa hao waliopo sasa hivi ili kuwaongezea nyongeza ya stadi ili waweze kufanya kazi zao kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu suala la kuhusisha maafisa wa sekta nyingine katika kusimamia shughuli za ushirika, kama inavyoeleweka kila sekta ina umuhimu wake na hawa maafisa katika kila sekta wanaonekana kwamba wana upungufu na kila idara inataka kuongeza watumishi wake.

Kwa hiyo, tunadhani kwamba tukiendelea na zoezi hili la kuwapa stadi mpya hawa waliopo pamoja na kuwaajiri hawa wapya nadhani kwamba sasa hii itasimiwa ipasavyo.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kudidimia kwa Ushirika kunatokana na muundo wenyewe wa ushirika na namna ya uchaguzi yaani namna wanavyopatikana Viongozi wa Ushirika na ukiritimba wa kuwaondoa viongozi wabadhirifu. Je, ni lini Serikali itayafanyia kazi mapendekezo ya Tume ya Rais ya kufufua Ushirika? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba hayo matatizo aliyoyaeleza yalishabainishwa na Kamati ya Rais, iliyoteuliwa kumsaidia katika kutafuta matatizo mbalimbali yanayousibu ushirika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu, kwamba mapendekezo ya Tume hiyo yameshaanza kufanyiwa kazi kwa sababu hivi sasa sera mpya ya maendeleo ya ushirika ilishapitishwa hapa Bungeni.

Vile vile muda si mrefu tunatarajia kwamba sheria mpya ya ushirika itawasilishwa hapa Bungeni kwa madhumni hayo hayo ya kuhakikisha kwamba mapungufu yaliyokuwa yamejitokeza huko yanaweza yakashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Na. 66

Wananchi Waishio Karibu na Hifadhi

MHE. AZIZA SLEYUM ALI aliuliza:-

Kwa kuwa katika maeneo mengi ya Hifadhi za Taifa vipo vijiji vya wananchi vinavyopakana na hifadhi hizo.

Je, kuwepo kwa wananchi kwenye vijiji vilivyo jirani na hifadhi hizo hakuwezi kusababisha matatizo na Serikali na vile vile uharibifu wa mazingira kwenye maeneo ya Hifadhi?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Matatizo mbalimbali yamejitokeza kati ya Hifadhi ya Taifa na jamii kutokana na vijiji vinavyopakana na hifadhi hizo. Mara nyingi kumekuwepo na matatizo ya mipaka kati ya Serikali za Vijiji na hifadhi za taifa ambayo yametatuliwa na mamlaka mbalimbali husika hususan za Kiserikali kwa mfano ni mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha Kilangali na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi uliotatuliwa na Mkuu wa Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuwepo kwa wananchi kwenye vijiji jirani na Hifadhi za Taifa kumesababisha tatizo la wanyama wakali na waharibifu kuhatarisha maisha ya wananchi hao na mali zao. Licha ya Serikali kutokuwa na uwezo wa kutosha kutoa fidia kwa wananchi wanaoathirika na uharibifu unaofanywa na wanyamapori, Serikali imeweka mikakati ya kudhibiti uharibu huo iki ni pamoja na kutoa kipaumbee katika kuwadhibiti wanyamapori hao na kufanya kila jitihada kushirikisha jumuia za vjiji katika udhibiti wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa wananchi kwenye vijiji vilivyo jirani na hifadhi kunaweza kusababisha uharibifu wa mazingira na kupungua au kutoweka kwa *bioanuai* kutokana na vitendo mbalimbali vya wananchi ikiwa ni pamoja na uchomaji moto ovyo, uwindaji haramu ujangili, ulishaji wa mifugo ndani ya hifadhi, uchimbaji wa madini, kilimo cha kuhamahama, uvamizi kwa ajili ya makazi *encroachment* na ukataji holela wa miti.

Mheshimiwa Spika, hayo yote na mengine mengi husababisha kupotea au kutoweka kwa makazi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi waishio kando kando ya Hifadhi za Taifa, Wizara inaendeleza ushirikishwaji wao katika uhifadhi ili nao, licha ya matatizo yanayowapata kutokana na wanyama waharibifu wafaidike zaidi kutokana na matumizi bora ya wanyamapori.

Napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge, kuwa mnamo tarehe 24 Januari, 2003 Serikali ilizitangaza rasmi kanuni za maeneo ya uhifadhi *(WMAS)* ambapo jumla ya maeneo kumi na sita yalianishwa.

MHE. AZIZA SLEYUM ALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la wanyamapori hasa tembo ambao wameleta uharibifu katika Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Nzega na kusababisha tembo 70 kuua mtu mmoja. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuweza kuwapa fidia wale ambao waliofiwa na ndugu yao? *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda kutoa pole kwa familia na ndugu wa Mzee Hengenduru ambaye alipoteza maisha yake katika Wilaya ya Nzega, kutokana kuuwawa na tembo hivi majuzi. Wizara ina taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni kwamba kulijitokeza tembo kati ya 70 na 200 na wananchi walitoka nje kuangalia hao tembo. Sasa kwa bahati mbaya kulikuwa na tembo ambaye alikuwa na mtoto na wanyama mara nyingi wakiwa na watoto wao wanakuwa wakali sana kwa sababu wanahisi labda wanataka kuwadhuru watoto wao.

Kwa hiyo, yule tembo ambaye alikuwa na mtoto alianza kuwakimbiza wananchi. Wananchi wakakimbia bahati mbaya huyu mzee alikuwa mzee sana na akaanguka, alipoanguka, yule tembo akamkanyaga na kumjeruhi mkono wa kushoto, mbavu na kifuani na kusababisha kifo cha mzee huyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunatoa pole kwa ndugu na jamaa wote. Lakini kilichotokea na kama tunavyofanya kwa kweli haraka tumetuma askari wanyamapori sita kutoka *KDU* pale Tabora na wameelekea Nzega ili kuangalia ni jinsi watashiriki katika kuhakikisha kwamba halitokei tena.

Kwa hiyo, tunatoa pole, lakini kila mara kama nilivyosema kwamba wanyama ni waharibifu na mnyama siyo binadamu. Tunachofanya kama nilivyoeleza hapa ni kwamba kushirikisha wananchi wenyewe, lakini hatuna uwezo kwa kweli kama Serikali kutoa fidia.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea mara nyingi ni kutoa kifuta machozi kwa sababu nafikiri huwezi kuthaminisha maisha ya binadamu na fidia yoyote. Kwa hiyo, tunatoa kifuta machozi lakini wakati huo huo huwa tunapeleka askari pamoja na silaha. *(Makofi)*

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya Hifadhi za Taifa zinakata barabara kuu kama ile ya Mikumi Morogoro, jambo ambalo linarahisisha baadhi ya watalii kusimama na kujionea wanyama mbalimbali pale, kitu ambacho kinakosesha mapato Serikali. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuepukana na hali hiyo? *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwamba suala hili kwa kweli limekuwa linaulizwa mara nyingi sana na kwa kweli Barabara ya Mikumi ni *high way,* isipokuwa tu kama uwezekano wa kuwa na barabara nyingine ambayo itapita pembezoni ndipo ambapo tunaweza kusema kwamba watalii hawa wasiangalie wanyama.

Mheshimiwa Spika, lakini watalii ni wengi sana napenda kusema kwamba wale ambao kwa kweli wana nia hasa ya kuangalia wanyama katika Mbuga ya Mikumi siyo tu wanapita, lakini wanaingia hasa hasa katika Mbuga hizi za Mikumi.

Na. 67

Ufufuaji wa Bwawa la Chato katika Hifadhi ya Mkomazi

MHE. JOHN E. SINGO aliuliza:-

Kwa kuwa idadi kubwa ya wanyamapori katika Pori la Akiba Mkomazi ilihamia Hifadhi ya Tsavo nchini Kenya kutokana na vibali vya uwindaji wa wanyama hao na kupasuka kwa Bwawa la Maji Chato na kwa kuwa hivi sasa Serikali imepiga marufuku uwindaji huo na badala yake kuhifadhi mazingira na wanyama hao ili warejee tena kutoka hifadhi ya Tsavo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya na kufufua Bwawa la Chato, ambalo ndilo lilikuwa kivutio kikubwa cha wanyamapori katika Hifadhi ya Mkomazi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wakushirikisha Wizara ya Maji ya Maendeleo ya Mifugo katika ujenzi mpya wa Bwawa la Chato?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, naomba kutoa maelezo ya awali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Chato lipo umbali wa nusu kilometa nje ya mpaka wa Pori la Akiba la Mkomazi. Bwana hilo lilichimbwa mwaka 1952 na iliyokuwa Idara ya Maji na Umwagiliaji *(Water and Irrigation Department)*. Madhumuni ya kulijenga Bwawa hilo yalikuwa ni kuhudumia wakazi wa Kijiji cha Vumari na mifugo yao ikiwa ni pamoja na shughuli za umwagiliaji hasa wa mboga za majani. Bwawa hilo lilibomoka mwaka 1976.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa idadi ya mifugo, ng'ombe na mbuzi ya wakazi wa kijiji cha Vumari, inafikia 4,500. Kutokana na bwawa hilo kubomoka tangu mwaka 1976 na kutokufanyiwa matengenezo ni dhahiri kwamba wakazi wa Vumari pamoja na mifugo yao wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la maji kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Bwawa la Chato ulifanyika kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Vumari na mifugo yao na siyo kwa ajili ya wanyamapori. Hata hivyo, Wizara yangu inatambua kuwa kwa kutokuwepo Bwawa la Chato, baadhi ya wananchi wa vijiji vinavyopakana na Pori la Akiba la Mkomazi wamekuwa wakivunja sheria kwa kuipeleka mifugo yao ndani ya pori hili na kupata maji na pia malisho. Kwa hiyo, Wizara yangu itakuwa tayari kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Same katika kuandaa mpango utakaowezesha Bwawa la Chato kufufuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa John Singo, kwamba Wizara yangu ipo tayari kuchangia kwa kiasi fulani ujenzi mpya wa Bwawa hilo kama itapatiwa makadirio halisi ya gharama za ujenzi mapema kabla ya wakati wa kutayarisha makadirio ya Bajeti ya mwaka na kama Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo itaona sawa kufanya hivyo. Kwa njia hii Wizara yangu itaweza kujua ni kiasi gani itaweza kuchangia kulingana na kiwango cha Bajeti yake ya mwaka. *(Makofi)*

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, ni kwa nini *Mkomazi Game Reserve* haijawa Hifadhi ya Taifa *(National Park)* baada ya kuwa katika hadhi ya hifadhi kwa muda wa miaka mingi yapata miaka 18 sasa? *(Makofi)*

(b) Je, Serikali itaipa Hifadhi ya *Mkomazi Game Reserve* hadhi ya *National Park* lini?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili hifadhi iwe *National Park* ni kwamba lazima kuna vigezo ambavyo vinatakiwa viwepo. Mojawapo muhimu sana ya vigezo hivyo ni wanyama mbalimbali.

Sasa upande wa Mkomazi kwa bahati mbaya kulikuwa na ujangili mkubwa sana wa kuvuna wanyama hawa. Kwa maana hiyo wanyama kwa kweli walitoweka.

Lakini napenda kusema kwamba hivi sasa tumeweka mikakati madhubuti na tunaandaa *management plan* kwa ajili ya Hifadhi ya Mkomazi. Hivi sasa wanyama wameanza wanarudi kidogo kidogo na kwa maana hiyo baada ya kurudi uwezekano wa kuwa National Park utafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Na. 68

Utaratibu wa Matibabu kwa Wabunge

MHE. HENRY D. SHEKIFFU aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa Matibabu kwa Wabunge na familia zao bado haujakidhi haja na haueleweki vizuri na kwa kuwa sasa umeanzishwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya:-

(a) Je, ni sababu zipi za kutowaweka Wabunge kwenye utaratibu huo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha utaratibu wa matibabu kwa Wabunge na familia zao.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipobuni Mfuko wa Bima ya Afya iliamua kutekeleza kwa awamu kwa kuanza na kundi dogo la Watumishi wa Serikali Kuu *(Civil Servants),* ili kujenga uwezo na uzoefu hasa katika mwaka wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya uzoefu wa mwaka mmoja wa utekelezaji wa Mfuko huu, Serikali ilileta Muswada Bungeni na hatimaye Bunge ililipitisha marekebisho ya Sheria Na. 8 ya mwaka 1999 iliyounda Mfuko huu ili kuongeza wigo wa makundi ya uanachama. Katika Awamu ya pili ya utekelezaji wa Mfuko huu, tumeongeza watumishi wengine wa umma, Serikali za Mitaa na Watumishi wa Serikali Kuu wasio na masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni *(Non Pensionable Operation Staff)* kuwa wanachama wa mfuko.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, hawako katika utaratibu wa kupata huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kuwa hawako katika *category* za utumishi nilizozitaja.

Masharti ya matatibu ya Wabunge yanatolewa na masharti yao ya kazi chini ya usimamizi wa Tume ya Huduma za Bunge.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa wa matibabu kwa Wabunge ni kujilipia wenyewe na baadaye hurudishiwa gharama za matibabu na Ofisi ya Bunge. Endapo Mheshimiwa Mbunge, atakuwa haridhiki na utaratibu huu, anashauriwa apeleke hoja hii kwenye Tume ya Huduma za Bunge, ili iweze kutafuta utaratibu utakaokubalika zaidi na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili.

Kwanza kwa kuwa tatizo la Wabunge kwa kipindi kirefu ni kutibiwa na kuja kuomba warejeshewe fedha hizo na utaratibu huu kwa kweli unawadhalilisha Wabunge kwa kiasi fulani. Kwa kuwa Serikali ni moja hiyo hiyo, ninaamini kwamba Tume itakapopeleka mapendekezo basi suala hili litachukuliwa hatua mapema iwezekanavyo. Je, ni lini na mapendekezo hayo yatatoka lini? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa suala la Wabunge kama viongozi ni muhimu sana wapate tiba nzuri. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchagua muhimu kimoja ambacho kinaweza kusimamia tiba kwa ajili ya Wabunge? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Henry Shekiffu, kama ifuatavyo:-

Suala la kwamba lini mapendekezo yatatoka nadhani alitakiwa alielekeze kwa Serikali. Tume ipo suala ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wenyewe wapeleke suala hili kwenye Tume ili litolewe uamuzi.

La pili kuhusu umuhimu wa kuchagua chombo. Nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge, kwamba si rahisi kuchagua maeneo ya kuwatibu Wabunge kwa sababu kila Mbunge anatoka eneo lake. Lakini kama Waheshimiwa Wabunge watakuwa Dar es Salaam basi nataka niwahakikishie kwamba pale Muhimbili tuna utaratibu madhubuti wa kuwasaidia viongozi katika eneo moja la matibabu. *(Makofi)*

Na. 69

Fedha kwa Ajili ya Utafiti

MHE. DR. AARON D. CHIDUO aliuliza:-

Kwa kuwa utafiti ni jambo ambalo halipewi uzito unaostahili kiasi kwamba kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya shughuli hizo huwa ni kidogo sana na vile vile chombo kinachoratibu masuala ya utafiti nchini hakijatambulishwa kwa uwazi:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa na Serikali kwa ajili ya shughuli za utafiti tangu mwaka 2000 hadi 2003 na kiasi hicho ni asilimia ngapi ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka?

(b) Je, Wizara ya Afya imeshaanzisha mfuko wa fedha kwa ajii ya utafiti *(Health Research Fund)* na una fedha kiasi gani hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua na inathamini sana shughuli za utafiti hapa nchini. Shughuli hizi zinahitaji hazina pevu ya taaluma ikiambatana na mitaji ya kununulia vitendea kazi bora na vyenye kutoa majibu sahihi na kwa haraka zaidi. Hata hivyo kulingana na ufinyu wa Bajeti na kwa kutambua umuhimu wa utafiti, Wizara ya Afya imejitahidi kutenga fedha kidogo ili kuendesha utafiti kwa kadri ilivyowezekana. Kuanzia mwaka wa fedha wa 2000 hadi 2003 Wizara ya Afya ilitenga fedha kwa ajili ya shughuli za utafiti kama ifuatavyo:-

Mwaka 2000/2001 Wizara ya Afya ilitenga shilingi 168,982,021 ikiwa ni sawa na asilimia 0.46% ya Bajeti. Mwaka 2001/2002 zilitengwa shilingi 206,153,316 sawa na asilimia 0.44% ya Bajeti na mwaka 2002/2003 zilitengwa shilingi 175,598,370 sawa na 0.30% ya Bajeti.

Hata hivyo, Taasisi na Mashirika mbalimbali yameshirikiana na *NIMR* katika utafiti na yamechangia fedha zipatazo shilingi 2,158,748,424/= hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Julai, 2002.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya kupitia Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya binadamu, imeanzisha mfuko kwa ajili ya utafiti *(Health Research Users Trust Fund)*. Mhisani wa kwanza kuchangia kwenye mfuko huu alikuwa *Swiss Development Corporation,* ambaye alichangia shilingi 14,000,000/= Hivi sasa mfuko una jumla ya shilingi 240,000,000/=.

MHE. DR. AARON D. CHIDUO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja.

Inakuwaje kutokana na takwimu alizotoa, kila mwaka kiasi kinachotengwa na Wizara ya Afya kinapungua? Je, haioni kwamba kwa kufanya hivyo ni kudumaza utafiti katika Wizara ya Afya? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimwelekeze au nimwonyeshe Mheshimiwa Mbunge kwamba si sahihi kusema kwamba kila mwaka zinapungua. Kwa sababu ukiangalia *figure* ya mwaka 2000/2001 ilikuwa shilingi milioni 168, mwaka uliofuata ilikuwa milioni 206, halafu mwaka uliofuata tena ndipo zilipopungua. Kwa hiyo, sio kwamba miaka yote inapungua, isipokuwa hii hutegemea na Bajeti ya mwaka huo na vipaumbele vilivyokuwepo kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama nilivyosema kwamba kuna wafadhili wengi sana. Kwa kutaja wachache ni *Bilgate Foundation, Rocapela Foundation* na *WHO* wamekuwa wakisaidia kwa kiwango kikubwa utafiti wa afya katika nchi hii. Kwa hiyo, Serikali inachangia kama mchango wake, lakini bado kuna fedha nyingi zinazotoka kwenye Mashirika mengine. *(Makofi)*

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume ya Kudhibiti Ukimwi imetengewa zaidi ya shilingi bilioni 48 mwaka 2003 na kwa kuwa imeonesha kuwa lishe nzuri inarefusha maisha ya waathirika na kuwa kirusi anayesababisha Ukimwi ni aina ya *Retro* inayobadilika badilika; je, ni kwa nini sehemu ya fedha hii isitengwe kwa ajili ya utafiti wa lishe bora na kuwashauri wananchi waweze kuitumia ili kurefusha maisha yao na kujua mwenendo wa kirusi huyu? *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, fedha za utafiti tunazozungumzia hapa ni zile zinazokwenda kwenye Taasisi ya Utafiti wa magonjwa ya binadamu na sio fedha zinazotoka *TACAIDS.*

Mheshimiwa Spika, lakini kama Mheshimiwa Mbunge anaulizia kuhusu *TACAIDS* basi, Serikali ina taarifa ya kwamba moja ya njia madhubuti ya kupigana vita na ugonjwa wa Ukimwi ni kuhakikisha lishe inakuwa bora. Kwa hiyo, bila shaka yoyote, fedha ambazo zipo *TACAIDS* kwa kiwango fulani lazima zitatumika katika kuhakikisha kwamba lishe bora inapatikana kwa wananchi. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kabla hatujaendelea na matangazo, sijapata taarifa ya Kikao chochote cha Kamati kilichopangwa kwa leo. Lakini ningependa kutoa taarifa kuhusu ratiba yetu kwa siku ya leo na kesho, nayo ni kwamba, wale Waheshimiwa waliojiandikisha kuchangia kwa mdomo watamalizika ifikapo saa ya kuahirisha Bunge leo jioni.

Kwa hiyo kesho ni siku ya Mawaziri kujibu hoja. Wataanza Manaibu Mawaziri wawili wa Hazina, watafuatia Mheshimiwa Waziri wa dhamana ya Mipango na Ubinafsishaji Mheshimiwa Waziri Kigoda halafu hapo watakapomaliza majibu, tutasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 ndipo atakapoanza kujibu Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe na itafuatia na kura ya kupitisha au kutokupitisha Bajeti kwa mujibu wa Katiba.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, niwakumbushe tu hasa Wabunge wageni kwamba hoja hiyo inapitishwa kwa kuitwa Mbunge mmoja, mmoja, jina lake kwa kusema ndio au sio.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hiyo ndiyo ratiba ya leo na kesho. Mwisho wa matangazo, Katibu tunaendelea na *Order Paper.*

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/04 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/04

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, wakinipigia makofi sana watanichanganya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kukupongeza wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza leo maana ni kama umeota kwamba leo ni siku ambayo mimi nimezaliwa. *(Kicheko/Makofi)*

Nilipokuwa napewa pongezi na watoto wangu, niliwaambia kabisa nimezaliwa tarehe ya leo, mtoto wangu wa mwisho kabisa wa miaka mitatu akasema kama umezaliwa leo, basi mimi ni mkubwa kwa sababu yeye alizaliwa mwaka 2000. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ina wimbi na mafuriko ya mafanikio, kwa hiyo, kwa sababu yapo mafuriko ya mafanikio, mchango wangu sio wa kuoga. Sikujiandaa na taulo wala sabuni, ila nimejiandaa kuogelea ili kuvuka ng'ambo ya mafanikio ya Wizara hii. Hivyo tutakuwa na hoja mahsusi na mfumuko wa pamoja, nitakuwa na hoja za jumla jumla kwa sababu yale mambo mazito nimeshayaandika kimaandishi na kumpelekea Mheshimiwa Waziri siku tano zilizopita. Hapa nitakuwa natoa habari nyepesi nyepesi. *(Kicheko)*

Habari ya kwanza inasema kwamba, katika hotuba ya Waziri wa Fedha kwenye *Order Paper,* naomba hii habari nyepesi nyepesi muiangalie Waheshimiwa Wabunge. Katika *Order Paper* inasema Waziri wa Fedha, atasema kwamba Bunge likubali kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi, tunakwenda namba mbili, inasema kwamba Bunge lijadili hatimaye liridhie. Ile ya kwanza likubali tu, hapana tutajadili vile vile. *(Kicheko)*

Habari nyingine nyepesi ni kwamba hotuba ya Waziri kwenye kitabu chake kwenye jalada mkiangalia kwenye *dot com* bahati mbaya nimeangalia kwenye *Website* ambayo kweli hotuba nzuri ila kuna neno kodi ya maendeleo ukurasa fulani imeandikwa maendelea.

Kwa hiyo, mtarekebisha maendeleo yale. Sasa kwa kuwa Waziri amesema kwamba hotuba yake alisema kabisa ile ni hotuba ya Waziri, lakini hapa chini anasema kimepigwa chapa. Kwa hiyo, ukitaka hili jalada liwe sahihi, aidha, uandike kihotuba au imepigwa chapa. Najua Wizara nyingine zitakuja hivyo hivyo kwamba unaposema hotuba kimepigwa chapa, hiki sio kitabu. Unatakiwa uandike kitabu cha hotuba kimepigwa chapa. Ndio! Ahsante nashukuru. Hizo ni habari nyepesi nyepesi, nilisema habari nyepesi nyepesi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, habari nyingine nyepesi nyepesi ni kwamba katika hotuba tumefanikiwa kwa kweli kwa wingi wa maneno na wingi wa utekelezaji na wingi wa idadi ya mafanikio. Lakini maneno naomba sasa yawe basi. Mnapochukua maswali yetu Waheshimiwa Wabunge kuna maneno 21, nitataja kumi bora. Kuipokea kama jambo limetokea kwa Mbunge, kulivalia njuga, kulipa kipaumbele, kulichukua na kulipeleka mahali panapostahili, kulishughulikia, kuliangalia kwa karibu, kulifuatilia, kulipa kipaumbele, kuliona, kulifanyia kazi na kuliwekea mikakati.

Hayo ni baadhi tu ya maeneno ambayo yamebubujika katika utaratibu wa matarajio ya historia, majigambo kwa Serikali ambayo imefanikiwa, inaweza kuwa na maneno mengi ya kuwaambia Watanzania waliopokea sera kwa shingo upande. Sasa walipofanikiwa waende kifua mbele. Hizo ni habari nyepesi nyepesi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, habari nyingine nyepesi nyepesi ni kwamba ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge. Nimeweka hapa habari nyepesi kwamba Waheshimiwa Wabunge, mmepongezwa na Bunge hili tukawapigia Makofi. Sasa kesho kutwa, hapa hatupigii kura sera, tunapigia hela. Hii ni Bajeti! Sisi tunatofautiana sera, sio hela. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, tutategemea kabisa Bunge zima litasema ndiyo, kwa sababu usiposema hivyo, ukisema sio tu, maana yake unapinga kwamba watu wako walipe kodi ya maendeleo. *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Rudia hiyo! Rudia!

MHE. SEMINDU K. PAWA: Hii narudia hii!

MBUNGE FULANI: Eh, irudie!

MHE. SEMINDU PAWA: Habari nyepesi nyepesi ni kwamba, mtu atakayesema sio, mngojeni kwa hamu Jimboni kwamba anataka mlipe kodi ya maendeleo. Anataka mlipe ushuru wa mazao, anataka msifuate jedwali la ukurasa 58 ambalo linakadiria mtu sio kwa sura bali kwa aina ya biashara anayoifanya na mambo mengine mengi yamefanikiwa. Tuogelee pamoja tuvuke ng'ambo ya mto. Tusioge, tuogelee. Tunabishana sera, sio hela. Hapa tunapitisha hela. Nimesema mwaka 2002 kwamba Wabunge wanafanya sera na hela, sio kudra. Tofauti na mtu aliyeuliza kwamba kwa nini giza linaonekana, mbona halina sauti na upepo unausikia mbona huuoni? Hizo ni kudra za Mungu hatuidhinishi katika Bunge hili. *(Kicheko)*

Katika ukurasa wa 64 kuna kitu kinaitwa *LPG,* nimefurahi sana kuhusu mpango wa *LPG* kwamba wamepunguza bei kutoka Kilogram moja. Hii ni *Clear Carbon Compound* ambayo ni aina fulani ya *compound* ambayo ni *Liquefied Petroleum Gas* ambayo wakati tulipokuwa tunapitisha mkataba hapa wa kuridhia Mkataba wa Rio wa kuhusu mambo ya utunzaji wa mazingira, mambo ya misitu isiishe nchini. Sasa hili ndio ukombozi. Wenzetu Senegal walifanikiwa kule na ninazo takwimu hapa sitasoma nyingi lakini nitazungumza kwa vielelezo. *(Makofi)*

Kwa mfano, Tanzania yenye watu milioni 35.1 inatumia karibu mita tani 4,000 tu wakati Senegal ambayo ina watu milioni 9.5 tu inatumia mita tani laki moja. Kwa hiyo, misitu yao inarudi kwa sababu huu ndio ukombozi wa kutaka watu hata urban areas, kwa sababu kule Dakar Senegal mwaka 1986 watu wanaoishi Mjini pale Dakar, asilimia 28 tu ya watu wa Senegal lakini wanatumia asilimia 89 ya hiyo *LPG.*

Kwa hiyo, Dar es Salaam nadhani ndio *consumption* kubwa ya mkaa. Kwa hiyo basi, hii hatua ya kupunguza bei hapa napongeza Wizara kupunguza bei ya gesi yenyewe, lakini haiji kwa kufungwa kwenye karatasi. Huwezi kufunga yaani ukitaka ufunge kwenye karatasi au kuwekwa kwenye chupa au ukaweka mfukoni ukaenda nayo kutumia kwenye jiko lako inayeyuka kabla hujafika. Kwa hiyo, inawekwa kwenye *container* maalum. Sasa zile *container* zina kodi. Sasa najua kwamba lazima hii kodi nayo ipungue kwa asilimia hii ili kusudi watu waweze kuzinunua. Ndio! Hizo ni habari nyepesi nyepesi. *(Kicheko)*

Nyingine kuhusu ongezeko la thamani katika upande wa *Mobile Phones* alilieleza vizuri sana kijana wangu jana, Mbunge wa Urambo. Nadhani alilieleza vizuri na hii itasababisha kwamba badala ya tuongee, sasa tunyamaze. Kwa sababu watapandisha na *Celtel* nadhani haifahamiki, kuna *fictitious* zinatokea katika hiyo Kampuni wakati mwingine inaweza ikapanda juu, kwa hiyo akaongeza asilimia tano au saba. Hatungejua kama ni asilimia ngapi wata-*rise* hii *price* kwa hiyo, watu watashindwa kuongea, watabaki nazo hizi kama hirizi. *(Kicheko)*

Lingine, ninapoongea mambo haya itabidi niongee halafu nirudi kwenye Jimbo langu kwamba tayari nimepeleka taarifa kwenye Jimbo, wamefurahi sana kuhusu suala la hii hotuba wananchi wa Vijijini kule Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Ponda, Mifuru, Hewe, Bagiro, Nyemegadu, Mkololo, Kumba, Aamini, Ludewa, Burugi, Kwaba na Lung'ala, wamefurahia.

Pili, nimefurahi na majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tungeomba tupatiwe karatasi zile za mgao wa fedha ya *Road Toll* kama walivyofanya Wizara ya Ujenzi, kwa mfano barabara ya kutoka Madamu kwenda Kinole, Msongizi kwenda Lubungo, Ngerengere kwenda Kidunda, sisomi nanukuu. Naona watu wanaangalia pale, kwa sababu nakwenda kwa mujibu wa Kanuni. Nazijua Kanuni! Nanukuu hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Ngerengere, Kiganila na daraja lile limejengwa *VTTP, KKKT, World Vision* pamoja na *TASAF*. Nasikia barabara hizi zimejengwa kwa hela ya mwaka 2000, 2001, na

mwaka 2002. Kwa hiyo, hivi ni viporo inajenga barabara ya kwenda Kidunda. Kwa hiyo, tungekuwa tunajua mapema Waheshimiwa Madiwani wetu ambao ni Wawakilishi wetu wazuri tu, wangetusaidia kusimamia fedha hizi kwa kujua *amount.* Lakini unazikuta siku ya kikao kama *Jackpot Bingo* kwamba mmepewa hela ya barabara. Habari nyepesi nyepesi. *(Kicheko)*

Habari nyingine ni kuhusu Tume ya Mipango. Hivi Tume ile ya Mipango ni Tume ya Uchumi au Tume ya Maendeleo ya Nchi hii? Maana naona pale imejaza wachumi tu, kwa nini msiweke watu wa miundombinu? Kwa sababu mipango ya Tanzania inaelekea kwenye mpango wa kuelekeza mtu kwenye uchumi. Wekeni watu wa miundombinu, watu wengine, wekeni wahandisi pale ili wa-*plan* nchi hii. Sio watu wa uchumi wanafikiria kuchuma tu hata vitu ambavyo hatukuvipanda. *(Kicheko/Makofi)*

Habari nyepesi nyepesi nyingine kuhusu fedha, tumeona jedwali la nchi zinazosaidia katika nchi hii. Tumesema Canada, tukapiga Makofi, *USA,* tukapiga makofi, sijui na Zambia mimi sikuiona ikitajwa kule. Wameitaja katikati kule lakini kwenye kushukuru sikuiona. Finland, tukapiga makofi. Halafu baadaye katika kuomba akasema kwamba tunaomba katika fedha za nje... Katika ukurasa ule wa jedwali anasema anaomba shilingi 1,175,821 milioni. Fedha hizi ni fedha za Tanzania. Sasa hawa mbona wametoa kwa *Canadian Dollar?* Hiyo *exchange rate* ilifanyika tarehe ngapi mpaka mkajua kwamba *amount* hii ndio tunapewa? Habari nyepesi nyepesi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna matatizo yaliyotokea, *timing bomb.* Nchi yetu tumesema kabisa kwa wananchi waliotuchagua na Ilani ya uchaguzi inasema kabisa, mshikamano, upendo na utulivu. Sasa kuna watu wametulia, lakini wana matatizo. Huu mwaka una matatizo kwa kweli.

Kwanza masuala ya njaa yalijitokeza, siwezi kusema sina *interest* nalo kifedha, ila nina *interest* ya kutoa fedha kwenye mfuko wangu. Kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge siwezi kuhojiwa. Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki pamoja na Wilaya ya Morogoro kwa ujumla, Mkuu wa Mkoa aliyekuja sasa hivi anastahili pongezi. Ametoa taarifa ya njaa na kupeleka Ofisi ya Waziri Mkuu. Kuna matatizo wanafunzi walishindwa hata kwenda kusoma mashuleni. Nimetoa gunia 90 kwa ajili ya uji, watumie wanafunzi na niliwaambia waende wakanywe uji hata wakifunga shule.

(Hapa kengele ililia)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Kengele hiyo inanishangilia. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, katika vitu vingine ambavyo ni *timing bomb* ni masuala ya umeme. Masuala ya umeme yamepanda bei. Napenda kusema kwamba tusiwe kisiwa cha bei ya juu. Tusiwe wabishi wa bei, tuwe wapatanishi wa bei. Niliwaambia wakati wa semina kule kwamba maswali sio mkopo na majibu sio malipo. Kwa hiyo, kama majibu ni malipo ya mkopo wa swali hilo, basi majibu yangekubaliwa pole pole. Mtu akisema taratibu kwa awamu amefanikiwa. Nikisema moja jumlisha na moja, jumlisha na tatu,

usiseme sawasawa na moja jumlisha na moja jumlisha na tatu, hapana! Unasema kwa mkupuo na sahihi, tano! Lakini kwa maswali, ni sahihi kujibu pole pole.

Kwa hiyo, mara nyingi hayako sahihi katika majibu yake kwa sababu hayalengi huko, hayako kwa mkupuo. Kwa hiyo, hapa ninayoyazugumza mtayakubali na kuyachukua kama nilivyosema katika maneno 11 na 21 ambayo mnayachukulia Serikali.

Kwa hiyo, napendekeza katika upande wa umeme tuweke *timeframe* ya kupunguza awamu kwa awamu ili kuwavutia wawekezaji katika nchi hii. Kwa sababu tunavutia tu kwa sheria ya uwekezaji lakini tunaweka kipingamizi. Sawa sawa na karibu basi, wawekezaji. Kwa hiyo, wanakwama wanaogopa. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, suala la umeme liende kwa pole pole kwa sababu mimi niliwaambia katika kubisha bei, kuna mtoto wangu mmoja alikuwa mbishi kuliko watoto wote. Nikawaambia nani mbishi hapo kwa bei akaninunulie mwamvuli? Wakasema Rehema. Nikamwita Rehema, kanunue mwamvuli. Mvua inanyesha. Sasa kwenda kule nikampa elfu tatu, najua tu elfu tatu atapata mwamvuli. Akaenda akamwambia mwenye duka mwamvuli bei gani? Akasema shilingi 3,200/=, akasema sitaki. Akamwambia shilingi 2,500/= akasema sitaki, akamwambia basi shilingi 1,500/= mtoto wewe uondoke! Akasema sitaki. Akachukua hela akasema nimebisha baba mpaka shilingi 1,500/=, hela yako hii hapa. Huu ni ubishi wa kipumbavu, hauleti mafanikio. Uking'ang'ania kitu kwa ajili ya kubisha tu, haisaidii. *Negotiate! (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni habari nyepesi nyepesi. Baada ya kusema hayo ni kwamba nimewapongeza Wabunge wapya wa pande zote mbili na ninapenda kuwaambia kwamba mmechaguliwa na wananchi wenu kwamba ninyi muige, lakini muogope mfano wa mchwa waliyekomaa. Mchwa aliyekomaa mara nyingi hupewa mbawa mbili na huruka kwa madaha kwenda juu. Lakini hajui kwamba mbawa hizo ni za muda, kuna kipindi ambacho mchwa hao huteremka na kukatika mbawa zao na kuanza kutambaa chini.

Hivyo basi, wa kuwaweka mbawa hizo hawana uwezo tena, wangoje mpaka wakati mwingine. Sasa mbawa hizo zimeshuka na wananchi wa Majimbo yenu, tafadhali sana waheshimuni, msiruke mbawa kwa mbwembwe, rudini chini, mwekeni Mungu mbele, umma kati, bakini nyuma. Naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

(Saa 4.22 Asubuhi Microphone ya Spika iliharibika na shughuli za Bunge kusimamishwa kwa muda)

(Saa 5.15 Asubuhi Bunge lilirudia baada ya Matengenezo ya Microphone kumalizika)

MHE. JUMA S. KIDUNDA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwashukuru wataalam wetu wa ufundi wa umeme kwa kurekebisha tatizo hili mapema. Kwa hiyo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kilindi na hasa Wilaya ya Kilindi, naomba nitoe shukrani nyingi kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufanya Jimbo hilo kuwa Wilaya na wananchi wamenituma kuwa wao hawatakuwa mzigo bali watatoa mchango mkuu katika uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha shukrani hizo napenda vile vile kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa hotuba zao nzuri na zenye mwelekeo nzuri wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 uchumi wa nchi hii ulikua wakati Awamu ya Tatu inaanza. Uchumi wa nchi hii ulikuwa katika hali ngumu sana na kwa kweli tunasema ulikuwa katika hali mbaya sana. Viashiria vingi vikuu vya uchumi mkuu vilikuwa viko katika hali ya matatizo kwa mfano *inflation* ilikuwa zaidi ya asilimia 30. Ujazo wa fedha ulikuwa haudhibitiki, kiasi cha kuashiria kwamba kwa ujumla uchumi ulikuwa umekaa katika hali ambayo haiwezi kuchukulika.

Sasa Wizara hizi mbili, wataalam wake wamekaa kutafuta utaratibu wa kuweza kuuhuisha uchumi wa Taifa hili ili tuweze kusonga mbele. Waliifanya kazi hiyo kwa bidii na kwa busara zote na kwa utaalam mkubwa mpaka leo katika Bajeti hii tunazungumzia kukua kwa uchumi kwa asilimia 6.2 na kwamba imefikia mpaka hata nchi za nje wakaona sisi tunastahili sasa hata kufutiwa madeni ili kusudi nguvu ambayo imekwishajengwa katika kipindi hiki iweze kusaidia zaidi maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa na nchi nyingi kama zetu bado zingali zinasuasua katika hatua za mwanzo zile 95 ambazo tulizikuta. Lakini sisi tumeanza kama ni gari tunasema, tulikuta magurudumu yake yamechakaa na yana viraka na mara nyingi yanakuwa na pancha kwa hiyo, gari ya uchumi ikawa haliwezi kutembea. Lakini timu hii kwa makini kabisa wamefanya ukarabati wa magurudumu ya uchumi, uchumi sasa umekaa barabarani na kwamba tuko tayari sasa kuelekea kwenye kupiga vita umaskini ambao ndiyo lengo rasmi na utaratibu mzima wa uchumi katika nchi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inatofautiana kimsingi na Bajeti za miaka iliyopita tangu mwaka 95. Kwa sababu Bajeti za miaka zilizotangulia zilikuwa zina jukumu la kujenga uchumi mkuu, ili kusudi kupata nguvu sasa za kuweza kutafsiri mafaniki hayo katika ngazi za uchumi wa kaya au *micro economy*. Kwa sababu huwezi kupambana na umaskini kama hujakusanya nguvu katika uchumi mkuu. Kwa hiyo, Bajeti za mwanzo kutoka 95 mpaka wa jana kazi kubwa ilikuwa ni hiyo kujenga uwezo wa kifedha na kinyenzo ili kusudi tutakapoingia kwenye uchumi wa kaya.

Mheshimiwa Spika, ndiyo sababu katika kipindi hiki mpaka mwaka wa jana kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi kwamba pamoja na mafanikio yanayozungumzwa na Serikali kwamba uchumi wa nchi hii unapiga hatua na unakwenda vizuri. Lakini mabadiliko hayo hayakuwa yanajidhihirisha katika ngazi ya Kaya, katika

ngazi ya familia. Maana yake hali ya maisha pamoja na kuboreka kwa uchumi mkuu hali ya maisha ilikuwa bado ni duni, ilikuwa bado haina matumaini makubwa.

Sasa tofauti katika Bajeti hii ni kwamba imekuwa sasa ni *returning point,* kwamba Bajeti hii sasa inatafsiri mafanikio makubwa tuliyopata katika uchumi mkuu kuyapeleka katika uchumi wa Kaya na wa familia *house hold economy.* Kwa hiyo, ndiyo maana nasema mtiririko mzima tangu mwaka 1995 mpaka sasa ni utaratibu ambao umepangiliwa vizuri kitaalam katika kukabili tatizo la umaskini kwa sababu ni lazima uanzie kwenye uchumi mkuu, halafu sasa ndiyo tumegeuka tunakwenda kwenye uchumi wa Kaya.

Mheshimiwa Spika, mwanzo unaowekwa na Bajeti hii ambao sasa utakuwa ndiyo mwelekeo wa kupambana na umaskini katika uwanja wa vita. Kwa sababu umaskini hauko katika uchumi mkuu, umaskini uko vijijini, uko kwa wananchi, umaskini uko kule Manzese, kwa wananchi mmoja mmoja katika kaya zao. Kwa hiyo, ukitaka kupigana na umaskini lazima uufuate kule. Sasa naipongeza Serikali kwa kufanya maamuzi ya kimsingi kabisa kuandaa uwanja wa vita kwa kupigana na umaskini na maandalizi yamekwenda vizuri mpaka sasa.

Kwanza kwa sababu katika kupigana na umaskini katika ngazi ya kaya, ngazi ya familia lazima uwashirikishe wale ambao unataka sasa msaidiane nao katika kupambana na umaskini. Kwa hiyo, lazima kwanza ujenge mahusiano ya kirafiki nao. Kwa muda uliopita kumekuwa na kero nyingi kwa mfano kero hii ya kodi ya maendeleo ambayo kimsingi kwa kweli katika Wilaya nyingi ilikuwa inaitwa kodi ya maendeleo kwa makosa tu. Kwa vile sehemu kubwa ya kodi hii ilikuwa inakwenda kwa shughuli za utawala na wala siyo shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, kwa kufuta kodi hii maana yake wananchi wengi sasa watakuwa wanatabasamu na watakuwa tayari kutoa mkono kwa Serikali na viongozi walio karibu nao katika vita hii. *(Makofi)*

Lakini vile vile kuna hatua ambayo nayo naipongeza. Hatua ya kumthamini *VEO* na kumthamini *WEO*. Hawa ndiyo viongozi wa Serikali walio karibu sana na wananchi na kwa kweli ndiyo majemedari ambao wako kwenye uwanja wa vita. Kwa hiyo, tunaweza kuwa tunafanya vizuri sana ngazi za juu kwenye uchumi mkuu. Lakini kama kwenye uwanja wa vita, majemedari hawa hawakuandaliwa vizuri, maana yake ni kwamba vita hiyo si rahisi kuishinda. Wote tumeshuhudia malalamiko ambayo yamekuwa yanaelekezwa kwa *VEO* na *WEO* na kwamba *VEO* na *WEO* wamekuwa wanaonekana kama vikwazo vya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuwaweka kwenye utaratibu wa ajira sasa maana yake ni kwamba vile vile tunawaweka kwenye utaratibu wa uwajibikaji kiutendaji. Kwa hiyo, hii ni hatua moja muhimu ya kuandaa sasa mapambano ya vita hii katika uwanja wa vita.

Lakini lingine ambalo limejidhihirisha katika mapambano haya ni kwamba imejidhihirisha sasa kwamba wananchi ambao ndiyo *partners* wetu katika vita hii ya kuondoa umaskini kule vijijini, hawana sifa mbovu kama vile ambavyo watu wengi

wamekuwa wakiamini kwamba wananchi ni wakorofi, hawataki kushirikiana au hawawezi kudhibiti fedha nyingi sana kwa uadilifu.

Kwa hiyo, haya yote kwa miradi kwa mfano, MMEM ambapo hela nyingi kabisa zilipelekwa kule kule vijijini. Tumeona matumizi yake yamekuwa yamefanyika kwa uadilifu kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, ni kweli kabisa kwamba kama maandalizi yakifanywa vizuri katika ngazi ya chini nina hakika kabisa uadilifu na uaminifu unaweza kutekelezeka kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye yale ambayo ni ya kijimbo kule kwangu. Katika kuandaa sasa hawa ma-*VEO* na ma-*WEO,* nafasi yao zaidi ni ya kimipango. Kwa hiyo, wanahitajika kupata mafunzo ya mipango, upangaji wa maendeleo katika ngazi hizi. Bila ya kuwapa mafunzo haya, maana yake dhamira yote ya kuweza kuleta mabadiliko haitaweza kutekelezeka na katika Taifa hili kuna Chuo kimoja tu ambacho kinaweza kufanya kazi hiyo na chuo hicho ni Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini ambacho kiko hapa Dodoma. *(Makofi)*

Kwa muda mrefu Chuo hicho kimekuwa kinaifanya kazi hii lakini kwa uwezo mdogo. Hakikuwa kimewezeshwa sawasawa. Nafurahi kwamba baada ya Mheshimiwa Waziri, Dr. Abdallah Kigoda, kuchukua madaraka ya mipango na baada ya Mheshimiwa Basil Mramba na timu yake sasa kuamua kwamba maendeleo lazima yaende vijijini, Chuo hiki kimeanza kuangaliwa vizuri sana. Wameanza kupata fedha za kutosha na za uhakika ingawa pengine hela nyingi zaidi zingesaidia zaidi. Lakini kwa kweli wamepata fedha za kutosha.

Sasa nafasi za kuajiri Walimu zinaweza kupanuliwa kwa hiyo ukienda pale Chuo cha Mipango sasa hivi unaweza kuona kwamba kweli Serikali inajiandaa kuweza kuleta mabadiliko katika ngazi sasa ya vijijinij kule ambako ndiyo vita ya umaskini inakopiganwa. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Serikali. Napenda kuwapongeza sana Mawaziri kwa utaratibu wa mtiririko huu wa kupambana na umaskini kwa utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule jimboni kwangu kuna kero tatu kubwa za msingi. Nimeshukuru kwamba sasa imekuwa ni Wilaya. Lakini sasa kuna miradi mitatu ambayo imekuwa inasuasua sana. Kuna mradi wa kwanza ni mradi wa umeme. Mradi huu ulianzishwa tangu mwaka 1998 kutoka Handeni kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kuja mpaka Songe ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya mpya hii ya Kilindi. Lakini kwa muda wote huo umeme huo haujaanza kuwashwa bulb hata moja. Hata pale mpakani bado mradi huu unasuasua. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ifanye utaratibu ili kusudi mradi huu sasa uharakishwe ufike pale Makao Makuu, Songe. Kwa sababu wananchi wamefanya wiring katika nyumba nyingi tu na kwa maana ya kwamba kiuchumi mradi huu sasa hauna matatizo.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ni kwamba mawasiliano ni silaha muhimu katika maendeleo. Lakini katika Wilaya mpya ya Kilindi kule hakuna simu za mkononi. Hakuna simu ya namna yoyote. Ukienda kule Wilayani maana yake ni kwamba

umejiondoa kabisa kwenye mawasiliano ya dunia. Kwa sababu sasa ile ni Wilaya. Maana yake ukienda Wilaya ya Kilindi utakuwa sasa umekwenda mahali ambapo huwezi kuwa na mawasiliano na sehemu nyingine yoyote. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili, ili kusudi mawasiliano hasa ya *TCCL* na mawasiliano mengine ya simu za mkononi basi yaweze kufika kule.

Lingine ambalo ni la msingi ni tatizo la barabara. Naweza kufikiri kwamba sababu moja ya kulifanya jimbo la Kilindi kuwa Wilaya ni kwa sababu ya ugumu wa mawasiliano katika eneo lile. Lakini sasa barabara zilizopo kwa mfano kama ile ya kutoka Makao Makuu Songe kwenda Handeni, halafu kwenda mpaka Makao Makuu ya Mkoa wa Tanga ni kilomita 200. Lakini kilomita hizo zinapitika kwa robo tu ya kipindi cha mwaka. Kwa sababu ya mvua nyingi zilizopo kule. Kuna hii ya Songe-Gairo ambayo nayo ni muhimu kwa ajili ya kuunganika na Dodoma, halafu kuna Songe-Kimbe-Mziha na Mbwewe ambayo inatuunganisha na Dar es Salaam.

Ningeomba barabara hizi ziangaliwe na Serikali ili kusudi ziweze kutengenezwa, kufungua mawasiliano kati ya Wilaya mpya ya Kilindi na sehemu nyingine za dunia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, kwanza niishukuru Serikali kwa kukubali kwamba Ofisi za Wabunge zikae kwenye majimbo yao. Tatizo ni kwamba kwa sababu sasa kuna samani, zinawekwa kule, Ofisi ya Spika inaweka na mali mbalimbali. Tatizo ni kwamba hakuna mtu sasa wa kuzidhibiti kule. Hakuna *Accounting Officer*.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuzungumza machache niliyonayo juu ya hotuba mbili hizi zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa Bajeti zao nzuri na mimi moja kwa moja napenda niseme kabisa naziunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nataka niseme kwamba Bajeti hii ni nzuri zaidi kuliko hata Bajeti iliyopita kiasi kwamba wananchi wengi sana wameifurahia Bajeti hii na uzuri huo ni kutokana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kipindi kilichopita, Bajeti iliyopita na vile vile ushauri wa Kamati mbalimbali zilizofanyika kabla ya kuja Dodoma hapa na pia ushauri wa wananchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri huu wa wananchi mbalimbali walioufurahia itakuwa mtihani mkubwa kwetu kama utekelezaji haukwenda sawasawa. Bajeti hii sasa hivi inatoa mwanga mkubwa sana wa maendeleo kwa nchi na kwa wananchi. Mwanga huu ni kwa ajili ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nataka kwanza niipongeze Serikali au niishukuru Serikali kwa kuteua ile Tume yetu ya Fedha ya pamoja ya Muungano na vile vile nimpongeze Mheshimiwa William Shellukindo, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti katika Tume ile. *(Makofi)*

Tume hii ni ya siku nyingi sana, lakini kwa bahati nzuri Tume tayari imeteuliwa na nawatakia kheri katika utekelezaji wa kazi zao. Kwa sababu kazi za Tume hii hazitakuwa ndogo. *(Makofi)*

Nikianza na mchango wangu sasa, katika mchango huu nitapenda nionyeshe tu wasi wasi wangu juu ya utekelezaji wa Bajeti hii au juu ya namna ya Pato la Taifa linavyoendelea kukua na kutoa tahadhari mbalimbali au ushauri kwa Waheshimiwa Mawaziri na Serikali kwa ujumla. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango alitueleza kwamba uchumi wetu sasa hivi unakua kwa asilimia 6.2. Lakini vile vile akatuambia kwamba kiwango hiki kwa kweli ni kwango cha kuridhisha na mimi nakubali.

Lakini hata hivyo, kwa mujibu wa *population* yetu tunavyoambiwa, inatakiwa Pato la Taifa liongezeke kufikia asilimia 8. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, katueleza kwamba kama tutakwenda hivi hivi itafikia 2006 bado tuko kwenye asilimia 7.4. Kwa kutaka Bajeti hii ifikie asilimia 8 lazima tujikaze, tushirikiane ili tuweze kuendeleza mbele uchumi wetu na hasa tukizingatia kwa kila mwaka kuna ongezeko la watu asilimia 2.9.

Lakini hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kaelezea pia namna ya kutekeleza matakwa hayo ukurasa wa 55, 56 na 57. Sasa haya yalikuwa kwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha na yeye pia katupa moyo kidogo, ametuambia kwamba Bajeti ya safari hii ni ya kuridhisha, ingawaje tunakwenda katika hali ya utegemezi, tunategemea mikopo na misaada kutoka nje kwa asilimia 45. Lakini hata hivyo, ametupa moyo akasema kwamba hii misaada na mikopo tuendelee kuitumia kwa sababu siyo peke yetu hata nchi za Ulaya nchi kubwa kubwa za Asia zinaendelea kwa mikopo katika miradi yake. Kwa hiyo, tuendelee kuitumia na akaahidi mambo chungu mzima kwamba mikopo hii itakwenda kwa sekta mbalimbali za muhimu yaani sekta muhimu zote zitasaidiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa tuna mtihani mkubwa sana kwa sababu alituambia kwamba tuko katika kipindi cha mpito, tunatoka katika uchumi mdogo kuingia katika uchumi mkubwa.

Nataka nitoe ushauri kidogo, hasa tukiangalia kwamba wananchi huko waliko toka siku Bajeti iliposomwa, wako katika kusherehekea. Sasa kama hii sherehe tutaibeza hii, matokeo yake yatakuwa mabaya kwa upande wetu. Sasa lazima sherehe hii izae matunda ya kukuza uchumi kweli kweli.

Wasiwasi wangu ni kwamba kutokana na mwaka 2002 kwamba pesa hizi za misaada na mikopo hatukuweza kuzitumia kikamilifu. Tulitumia chini ya asilimia 50.

Sasa hapa ndiyo wasiwasi wangu kwamba yasije yakatutokea kama yale yaliyotokea mwaka jana ya kuachwa pesa hizi tulizozipata za mikopo zikaenda bure, ingawaje Mheshimiwa Waziri alituambia kwamba sasa hivi pesa zile za mwaka 2002 tayari zimeshapatikana. Kwa hiyo, hakuna wasiwasi. Lakini sasa hata hivyo, kama hatukutekeleza sawa sawa basi matokeo yake yatakuja kuwa yale yale ya kipindi kilichopita. Kwa hiyo, hapa lazima wasiwasi tuwe nao juu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa wasi wasi huu napenda nipendekeze yafuatayo:-

Kwanza, ningeiomba Serikali yenyewe iunde au iwe na mpango mahususi wa kusimamia utekelezaji wa mambo yote haya tuliyoyapanga katika Bajeti yetu hii. Tuwe na mpango makusudi kwa sababu kuna matatizo katika ofisi za Serikali, kuna matatizo kwetu sisi wananchi pia, wafanyakazi. Kwa upande wa wananchi, ningetoa wito kwa wananchi wenzangu kwamba jamani sasa hivi imefika wakati wa kubadili tabia zetu za ukwepaji kazi. Lazima tubadilike kitabia katika utendaji kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, tuache kutegea katika kazi mbalimbali za Serikali, iwe kazi ya Serikali au ya mtu binafsi. Lazima tukwepe utegeaji. Kuna wafanyakazi wengine sasa hivi wanajitia kwenye shughuli za biashara ndogo ndogo badala ya kufanya kazi pale, lazima aondoke katika kazi zile, akashughulikie biashara zake. Kwa hiyo, huu ni utegeaji wa kazi ambao unazorotesha kabisa utendaji kazi wetu. *(Makofi)*

Vile vile tuache urasimu uliomo makazini. Unaweza ukawa una jambo lako ukaenda Ofisini kutaka chochote tu, hata cheti, hata kulipia ada fulani, ukazungushwa, kitu cha kufanya wiki moja kinafanywa pengine kwa mwezi mzima au hata miezi mitatu. Kwa hiyo, tuache urasimu huu ili kazi zetu ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutaka tusiachane nyuma kutokana na uchumi wetu sasa hivi tunapoelekea uchumi mkubwa, kwa kutaka tusiachane nyuma, hasa ukizingatia wananchi wetu wako nyuma kidogo katika shughuli za kuendesha biashara iwe za viwanda au biashara zozote zile, lazima Mheshimiwa Waziri au Serikali ifanye namna ya kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wetu au kwa wananchi wetu ili wananchi wetu nao waweze kukabili ushindani huu wa kibiashara iwe katika viwanda au biashara za aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe mafunzo ya makusudi waweze kuitumia mikopo hii inayotolewa, waweze kuitumia misaada hii inayotolewa. Lazima tupewe mafunzo ili tuweze kukabiliana na shughuli kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hapo hapo nimalizie kabisa pendekezo lingine ni kwamba kuna Mkataba ule wa Huduma kwa Mteja. Mkataba ule haujafanyakazi vizuri, lazima tuseme kweli. Kazi katika ofisi, huduma ziko vile vile au huduma wanazozitoa wafanyakazi ofisini hasa ofisi nyingine ziko vile vile. Kwa hiyo, Mkataba huu wa huduma kwa mteja, lazima usimamiwe ili shughuli za ofisini ziende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niachie hapo kwa sababu kengele tayari, nije kwenye mambo ya ubinafsishaji.

Kwanza, niwapongeze Tume yetu hii ya Ubinafsishaji *(PSRC),* nayo hii nilipata nafasi ya kutembelea sehemu mbalimbali ambazo zimebinafsishwa katika Kamati yetu ya Fedha na Uchumi na sehemu nyingine ambazo hazijapata mtu wa kubinafsishiwa. Katika sehemu hizi, tuliweza kujifunza mengi sana na mimi naunga mkono shughuli hizi za ubinafsishaji kwa sababu ni jambo ambalo linamsaidia mwananchi na vile vile kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, ingawa tulikwenda katika sehemu chache ambazo tulizitembelea au vikundi vichache ambavyo tulivitembelea, lakini tuliona maendeleo yaliyopatikana pale katika makampuni yale au katika viwanda mbalimbali ambavyo tulivitembelea.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu zile tulikuta matatizo mbalimbali na kwa kweli wahusika wa sehemu zile tuseme kwa mfano, viongozi wa viwanda au tuseme kwa mfano, Mheshimiwa Waziri au yeyote tu au Waziri wa Kilimo na Chakula, hawapitii kule kuona mambo yanavyokwenda.

Sasa mimi ningetoa wito kwa Mawaziri wanaohusika waweze kupita kwa sababu sehemu nyingi walisema toka siku ya makabidhiano ya mikataba yao ya kuendesha viwanda vile au makampuni yale hawajapita viongozi wahusika. Kwa hiyo, ningetoa wito watu hawa wenye sekta zao waweze kupitia ili wajue mambo yanavyokwenda kutokana na mikataba yetu kama ndivyo au sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tuligundua kwamba mikataba nayo pia ina matatizo, kwa hiyo, ningeshauri Serikali mikataba hii ya kukabidhiana mambo ya makampuni mbalimbali yaletwe Bungeni hata kwenye Kamati zetu tu, tuweze kuiona mikataba ile na kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika viwanda vingi tulipata malalamiko kuhusu shughuli za umeme. Hapa ningeiomba Serikali itafute namna ya kutatua tatizo hili kwa sababu hili ni tatizo sugu na malalamiko haya ni malalamiko ya siku zote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, umeme ni tatizo kubwa kwa viwanda na kwa wananchi wote kwa ujumla. Nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa kodi mbalimbali zile na ushuru na ada mbalimbali kwa wananchi ambazo zilikuwa kero sana.

Kwa kweli uamuzi huu ulikuwa ni wa busara na lazima tuitolee pongezi shughuli hii na ndiyo maana wananchi wakashukuru na pia wakafurahi ikabidi washerehekehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa juhudi zao. Lakini hata hivyo nitoe ombi kwamba,

kutokana na wimbi lililozuka la ujambazi na majambazi wenyewe wengine ni wa ndani ya nchi na wengine ni wa nje ya nchi, silaha nyingi zimegundulikana kama alivyojibu swali juzi hapa Bungeni, sasa na mimi ningependa Mheshimiwa Waziri au Serikali irudishe ule mradi wa vitambulisho ili wananchi Watanzania tuweze kujuana na itakuwa rahisi kuwagundua hawa ni Watanzania au hawa siyo Watanzania. Suala hili ni muhimu na ni lazima tulichukulie uzito wa aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu *time* imekaribia, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia na ninawatakia kila kheri. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MONICA N. MBEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea naomba nitoe salaamu za pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameapishwa hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitoe salamu za pongezi kwa Ndugu Kitilya, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato na Ndugu Luoga kuwa Naibu wake, kwa kuteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kabisa kwamba ninaunga mkono hotuba zote mbili kwa dhati na bila kipingamizi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu ni salamu ambazo siku ya kwanza kabisa baada ya hotuba ya Bajeti nilipokea simu mbalimbali kutoka kwa wananchi wangu wa Manispaa ya Iringa ambao walinituma kabisa kwamba ni lazima nitoe shukrani na kutoa pongezi, kwa jinsi ambavyo Bajeti hii kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyomalizia, kwamba imekuwa ni Bajeti ya kuwasaidia wanyonge wakiongozwa na wananchi wa Vijijini ambao wengi ni wakulima wadogo wadogo. Kwa kweli kuna mabadiliko makubwa kutokana na Bajeti za uko nyuma.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kutaja mambo mbalimbali ambayo wananchi wa Iringa wameyafurahia, lakini ni vizuri pia nikasema kwa sababu kama walivyosema wenzangu, ni vizuri nikasema ni kitu gani hasa ambacho kwa kweli ni msingi wa furaha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianzia na marekebisho ya kodi, wananchi wamefurahi sana, ruzuku kwa mbolea, uanzishwaji wa mifuko mbalimbali ili wananchi wasio na uwezo wa kutimiza masharti ya Ki-benki waweze kupata mitaji. Hicho ni kitu cha msingi sana na ulipaji wa ada kwa watoto ambao walezi au wazazi wao hawana uwezo. Hakika wananchi wa Manispaa ya Iringa wameshukuru na wametoa pongezi za dhati na mimi kwa niaba yao naomba nizifikishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa na mimi nichangie nikianzia na lile alilozungumzia Mheshimiwa Waziri kuhusu pensheni kwa wastaafu.

Naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali, kwa kuweza kupandisha kima cha chini cha pensheni ya wastaafu na pia nashukuru na kupongeza kwa kuweza kutoa kile kipengele cha mkupuo ambacho kwa kweli kilikuwa ni kero kubwa kwa wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu kwa kawaida walikuwa hawaelewi kwamba ukipokea zile pesa kwa mkupuo, kwa sababu akipigiwa hesabu anakuta kwamba ni pesa nyingi sana, kwa hiyo anaamua achukue kwa mkupuo lakini anasahau kwamba baada ya hapo hata kama amepata shilingi milioni tatu au shilingi milioni nne, anaweza akazitumia katika kipindi cha miezi miwili au mitatu zikawa zimekwisha na kwa maana hiyo anabakia tena hana mkataba na Serikali na baada ya kuwa hana mkataba na Serikali ina maana kwamba ataendelea sasa kupata matatizo kwa sababu anakuwa hana pesa yoyote ambayo anapata.

Sasa kwa kuweza kutoa kipengele hiki, mimi kwa hakika kabisa nashukuru na nakupongeza kwa maana kwamba hawa wastaafu sasa wataendelea kupata pesa katika kila kipindi cha miezi sita na kwa maana hiyo zitawasaidia kuweza kuendelea kuishi vizuri hadi umri wao wa kuishi utakapokuwa umefikia kumalizika katika kile kipindi ambacho Kisheria pensheni inatakiwa kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ombi hapa kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba mwaka 1994 wakati wafanyakazi walipopunguzwa, wakati hesabu zinapofanywa kwa ajili ya kupata pensheni inaelekea, si inaelekea ni hakika kwamba walilipwa kwa mkupuo bila kuulizwa wale wastaafu. Kwa maana hiyo walipewa zile pesa za mkupuo lakini wenyewe walikuwa hawakuomba na kwa maana hiyo kwa sasa hivi wamekuwa wakitufuatilia sisi Waheshimiwa Wabunge kutuomba tuweze kulisimamia hili suala ili waweze kulipwa pesa zile. Jimboni kwangu kuna baadhi yao ambao wamekuwa kila mara wakinifuatilia, wakisema wao kwa kweli wanashangaa kwamba mkataba na Serikali umekwisha wakati wao hawakuomba kwa mkupuo.

Lakini hapa Bungeni nimekuwa nikipokea barua, mimi, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, ambazo ni nakala zinazokwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, zikieleza tatizo hili la mkupuo na wakiomba kwamba waendelee kupewa pesa za pensheni. Mheshimiwa Waziri mimi nina kuomba kwamba kwa sababu wale watu ni wachache, Serikali ione namna ambavyo inaweza kuwasaidia wale wastaafu kwa sababu hawakuomba wenyewe, kama wangekuwa wameomba basi tungesema ni kitu kingine lakini hawakuomba wenyewe. Kwa hiyo, naomba unapo-*windup* utusaidie ili tuone namna gani tunavyoweza kuwasaidia hawa wastaafu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ukiangalia au ukisikiliza kutoka mwanzo walivyoanza Waheshimiwa Wabunge toka kuchangia mpaka sasa hivi, unakuta kila mmoja anashauri *either* kama ingekuwa ni mapato aweze labda kupata chanzo kingine cha mapato, lakini pia kwa upande wa matumizi Mheshimiwa Mbunge anaweza kusema

labda fedha mahali fulani zitolewe ili zipelekwe katika kifungu namba fulani ili kusudi kiweze kusaidia zaidi.

Lakini inavyoonyesha ni kama ambavyo wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika huwa unatuambia ya kwamba, kwa kweli hakuna uwezekano katika kipindi hiki, kwa maana shughuli zote za Bajeti zimeishakwisha. Kwa hiyo, hapa sisi tunachofanya ni kutoa kama ushauri, tunaishauri Serikali ili katika utekelezaji wake, waweze kutekeleza kwa kufuata baadhi ya mambo lakini pia ni ushauri kwa ajili ya Bajeti ya mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natoa ushauri au nilikuwa nataka kutoa ombi kwamba, ninaomba utaratibu ubadilike kwa maana ya kwamba Waheshimiwa Wabunge tuhusike kutoka mwezi March katika maandalizi ya Bajeti. Kwa maana ya kwamba wakati Serikali inapoleta midterm review kwa ajili ya matumizi ya mapato yake, basi Waheshimiwa Wabunge kuwe na Kamati na labda niseme kwamba kwa kweli ningependa labda nije nitoe hoja binafsi ambayo itasaidia kuunda hata Kamati ambayo itahusika na kujadili Bajeti kuanzia ule mwezi March ili kuielekeza Serikali ni wapi ambapo mapato yanaweza kupatikana zaidi na pia ni wapi ambapo matumizi yaweze kuelekezwa. Inapofikia kipindi hiki kila mmoja anakuwa ameridhika, basi inakuwa sasa ni majadiliano ambayo yanakuwa kwa kweli hasa yameweza kukidhi haja ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, nilikuwa napendekeza kwamba Serikali ione ni namna gani sisi Waheshimiwa Wabunge tunavyoweza kuanza kushughulikia Bajeti kuanzia mwezi March, hiyo itasaidia sana. Si kwamba ceiling ya pesa itabadilika lakini katika vifungu tunaweza tukahusika katika reallocation ambazo zitasaidia ili kuweza kukidhi yale ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa tumekuwa tukizungumza kwa dhati kabisa ya kwamba kama ingelikuwa mimi ningeweza kufanya hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi nalisemea kwa dhati hilo kwa maana ya kwamba kama na mimi ningekuwa nimehusika toka mwanzo ili kuweza kuandaa Bajeti hii, ningeweza kuishauri Serikali kwamba sasa hivi pamoja na yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema lakini kwa upande wa Vyuo Vikuu kwa kweli ilitakiwa tupate mkazo kwamba tuweze kupata pesa nyingi zaidi ili ziweze kwenda Vyuo Vikuu. Kama mlivyoona hapa baadhi wamechangia kwamba hakuna pesa ya research, pesa ya research ni ndogo na tunajua kabisa ya kwamba vyuo vyetu vikuu kazi yake kubwa ni research. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mbaya zaidi nadhani mnajua Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mimi ni Mwakilishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Bungeni, kwamba mwaka jana Serikali iliwafadhili wanafunzi 3,300 lakini mwaka huu imepunguza na wamekuwa 2,500, kwa maana hiyo badala ya kwenda mbele kama tunavyosema Kitaifa kwamba tunataka wanafunzi wengi zaidi waweze kuongezeka tunarudi nyuma. Kwa maana hiyo, kama sisi Waheshimiwa Wabunge tungekuwa

tumehusika, basi tungekuwa tumesimamia pale kwamba angalau wanafunzi wengi zaidi waweze kupata ufadhili wa Serikali. Kwa maana hiyo basi, naishauri Serikali kwamba maadam ni wanafunzi wengi sana wamekosa kuweza kuingia Vyuo Vikuu kwa sababu wamekosa ufadhili wa Serikali, basi waongeze muda katika Vyuo vya Fedha kama IFM, DSA na Arusha ili kusudi waliopata division one na two ambao wamekosa Chuo Kikuu basi waingie katika Vyuo Vikuu hivyo ili kusudi wakaweze kusoma kwa sababu kweli wazazi wengine hawana uwezo kabisa wa kuweza kuwalipia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kumalizia, ni kwamba ni kweli baada ya maagizo ya Mheshimiwa Waziri ya kupunguza baadhi ya vyanzo hivi vya mapato, ni kwamba mapato ya Halmashauri zetu yamepungua. Lakini huo ni mwongozo ambao ulikuwa umetolewa toka siku nyingi, toka mwaka jana walikuwa wamekwishatoa mwongozo kupitia kwenye Ofisi ya TAMISEMI kwamba Halmashauri zote ziweze kuandaa mapato kutokana na vile vyanzo ambavyo vitakuwa vimepunguzwa na wakati huo Serikali Kuu iweze kufidia pale ambapo yatakuwa yamepunguzwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu ni kwamba naiomba Serikali pamoja na kwamba ni cash budget lakini iweze kuangalia kwa dhati kabisa ili Halmashauri zetu zisiweze kutetereka katika matumizi yake kwa sababu miaka ya nyuma, hapa nina Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Halmashauri yangu ambayo inaonyesha kwa mwaka jana fedha ambazo zilipatikana ilikuwa ni asilimia 60 tu kama ruzuku.

Sasa kama tumepunguza kutokana na vyanzo vyetu ambavyo vitakuwa vimepunguzwa kutokana na agizo hili la Serikali ambapo wananchi wamefurahia, lakini kama fedha zile hazitaweza kwenda ina maana huduma kwa wananchi zitakuwa zimepungua na kwa maana hiyo itakuwa kama vile umewasaidia kwa mkono wa kulia lakini kwa mkono wa kushoto umewapunguzia na kwa maana hiyo hawataona yale manufaa ambayo Serikali imetamka katika Bajeti hii. Kwa maana hiyo, naomba sana kwamba ruzuku ambazo zitakuwa zinapelekwa katika Halmashauri zetu basi ziende kama ambavyo Bajeti zetu tumezi-bajeti na kutokana na cash budget jinsi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda umepita, naomba basi na mimi nimalizie kwa kusema kwamba, nashukuru na kuipongeza tena Serikali kwa kazi nzuri iliyoifanya katika Bajeti ya mwaka huu na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii ili niweze kuwapa pongezi Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda na Mheshimiwa Basil P. Mramba, kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa kweli zimeonyesha matumaini, sasa hivi kwa kweli tunaishi kwa matumaini, matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii niweze kumpongeza Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga, kwa uteuzi ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kushika chombo madhubuti. Hii yote inaonyesha kwamba kazi yao ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kuweza kuipongeza Serikali kwa uamuzi mzuri wa kufuta kodi ya maendeleo. Kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kilolo, Wilaya mpya, wamefurahi na wameahidi kwamba bado wataendelea kuchangia nguvu zao kwa bidii ili kuleta maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda. Kwanza, nimpongeze yeye binafsi na wataalam wake, leo hii tunapozungumza habari ya kupanda kwa uchumi wa Tanzania lazima tusifu shughuli ya ubinafsishaji kwa sababu baada ya kuamua kufanya ubinafsishaji kuna Mashirika kwa mfano *TBL, Tanzania Cement, TTCL, Kagera Sugar* na Mtibwa yameongeza Pato la Taifa. Kwa hiyo, mimi binafsi naweza kusema kwamba wao ndiyo waliotufutia kodi za maendeleo kwa sababu wanalipa wao sasa *deficit* ile, wao ndiyo wanasaidia kulipa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mapungufu, hayo tunaweza tukayarekebisha, bahati nzuri mimi niko kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, tumepata bahati ya kutembelea Mashirika ambayo yamebinafsishwa kwa wazawa na Mashirika mengine ambayo yamebinafsishwa kwa wageni, tumeona matatizo. Kuna sehemu ambayo wazawa ni wababaishaji na kuna sehemu ambayo kuna wageni wababaishaji, sasa mpaka inakatisha tamaa kwamba kumbe unaweza ukampa mzawa lakini akaharibu tu kwa kutumia uzawa. Sasa hii ni vizuri tukapimana kuona; je, huyu mzawa kweli ana nia ya kutusaidia sisi wazawa au ni mzawa mbabaishaji au anatumiwa? Kwa hiyo, ni vizuri tukawa tuna utaratibu wa kwenda kuratibu Makampuni yetu au Mashirika ambayo tumebinafsisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ni vizuri sasa tukaweka sera zetu za ubinafsishaji vizuri hasa kwenye viwanda ili tuweze kukusanya kodi nyingi na nafikiri baadaye itafikia tu wakati wazee tutakuwa tunawalipa kodi kwa sababu tutakuwa tuna fedha nyingi tu.

Mheshimiwa Spika, pia nichangie kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hotuba ya Bajeti. Sasa hivi kwa kuwa tumekwishaondoa kodi za maendeleo mategemeo yetu yatakuwa ni kwa watu, wenzetu wakusanya kodi wa *TRA*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kitilya na Mheshimiwa Luoga kazi ambayo mnayo mbele ni kubwa. Sasa kwa kuwa watu wengi wamekwishachangia sana katika maeneo mengi, mimi ningependa kugusia maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, eneo mojawapo ni ambalo limelalamikiwa na mwaka jana lililalamikiwa, ni la Bandari. Mimi nafikiri wale *COTECNA* na *ICS* ikiwezekana waondolewe kabisa kwa sababu kitu cha ajabu ni kwamba wale *COTECNA* na *ICS* wanapata fedha nyingi sana za walipa kodi lakini kazi yao wao ni ya ukadiriaji, *COTECNA* wanafanya ukadiriaji, *ICS* ukadiriaji na pia *TRA* ukadiriaji. Sasa kitu cha ajabu ni kwamba mizigo huo huo mmoja unatofautiana, huyu anakadiria hivi na huyu hivi, sasa matokeo yake mzigo unakaa muda mrefu bandarini, sasa inachukua fedha nyingi mwenye mali baadaye sasa anachukia, sasa hatuwezi kuboresha na ile ni sehemu ambayo tunategemea tutapata mapato mengi. Kwa hiyo, ili tukusanye fedha nyingi wale

jamaa waondoke halafu zile fedha ambazo tulikuwa tunatumia kuwalipa tuwape mafunzo ya kutosha watu wa *TRA,* kama elimu ya kutosha tumeishapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulipitisha Sheria mpya ya uthaminishaji wa mizigo ambayo tuliambiwa itakuwa ya uwazi na ukweli, lakini mpaka sasa hivi haijatumika. Sasa mimi nafikiri ni vizuri Sheria ambazo tunazitunga wenyewe baadaye tukawa tunahakikisha ya kwamba kweli zinatumika? Kwa hiyo, mimi nakushauri Mheshimiwa Waziri kwamba kazi ya kwanza ambayo itabidi Mheshimiwa Kitilya na Luoga waifanye ni *either* kuwaondoa wale jamaa wote au abaki mmoja ili kupunguza ile bughudha na kero ambazo hasa ndiyo zinasababisha rushwa pale bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia sehemu nyingine ambayo nafikiri ni vizuri ikafanyiwa kazi, ni upande wa madini kwamba kuna hii *road and fuel levy.* Kwa hao wenzetu mimi nafikiri iangaliwe vizuri kwa sababu zile fedha zinakwenda kwenye matengenezo ya barabara lakini na mitambo wanayoleta wale jamaa ni mizito, inaharibu barabara na ukiangalia kiwango ambacho wanalipia kodi, wanalipia dola laki mbili ndizo zinazolipiwa ushuru, lakini mafuta yanayozidi hapo yanakwenda *free.*

Sasa ukipiga hesabu za haraka haraka unakuta wale watu kwa mwaka mzima wanalipia mafuta miezi mitatu tu lakini miezi mingine tisa yote inakwenda tu. Sasa ni vizuri tukaangalia, ikiwezekana turekebishe hiki kitu ili tuweze kupata fedha nyingi kwa sababu sasa hivi tunatakiwa tupate fedha za kutosha hasa kwa hawa wawekezaji ambao tuna hakika kwamba nao wanajiendesha kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa uamuzi mzuri wa kuamua kutoa upendeleo maalum kwa *the big four,* ile mikoa ambayo ilikuwa inalima vizuri zamani, Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Mimi nina hakika kabisa sasa hivi Serikali imeamua kweli kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishieni ya kwamba kwa kuwa mpango huo unalenga Mkoa wa Iringa, wananchi wa Wilaya ya Kilolo hasa wa Vijiji vya Ng'ang'ange, Muhanga, Kitowo, Ilula na Kitonga watafanya kazi kubwa ya kilimo. Lakini ninachowaomba ni kwamba, pembejeo zifikishwe kwa wakati unaotakiwa. Pembejeo zishushwe bei ili sisi tuweze kulisha Miko. Ile Wilaya ya Kilolo peke yake inaweza kulisha zaidi ya Mikoa minne kama tutafuata hayo mambo ambayo nimewaambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba miundombinu kwa sababu sasa hivi wakati Mikoa mingi inalia na njaa, Kilolo tuna mazao lakini tunashindwa kuyasafirisha kwa sababu ya barabara, miundombinu na kadhalika.

Sasa kuna barabara ambayo mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri ningekuomba kama utapata nafasi uweze kuja Iringa, kama utaimarisha hiyo barabara utaona jinsi pato la Taifa litakavyopanda. Barabara hiyo inatokea sehemu za Ilula inakwenda Mlafu, Isagwa kutokea Lulanzi - Kilolo. Hiyo ikiimarishwa ikawa ni barabara ya Mkoa mimi

nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri sisi tutawaomba tu watu wa Moshi muendelee kulima kahawa lakini mahindi tuachieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya kutoka Buhanga kwenda Mngeta, hiyo ni barabara ya ukombozi pia kwenda Wilaya nyingine, kama ingeimarishwa tungekwenda kuungana na treni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie habari za mgao wa fedha. Sasa hivi fedha nyingi zinatoka Serikali Kuu zitapelekwa kwenye Halmashauri. Sasa hizo fedha zizingatie idadi ya watu wa Wilaya zile halafu pia ziwe za uwazi kama zile za elimu zinavyotolewa kwamba fedha zimetolewa zimepelekwa kiasi fulani na zidhibitiwe na uwezo wa kudhibiti fedha tunao kwa sababu tuna wataalam ambao wamebobea, ambao wanaweza wakazifuatilia hizo fedha zisiibiwe. Pia tuwashirikishe Waheshimiwa Wabunge kwamba Wilaya fulani fedha zimekwenda kiasi fulani na zitafanya kitu fulani. Kwa hiyo, tukiweka *transparency* ya namna hiyo tutaona umuhimu wa kupambana na umaskini ambao umekithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sikufanya haki kama sitampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa kuamua kujenga Uwanja wa Taifa. Lakini mimi napenda kuwahakikishia *TRA* kwamba kama mtatupa msaada mkubwa hasa Serikali na uwanja ukajengwa maana yake ni kwamba tutawapata wachezaji wengi ambao tunaweza tukawauza nje na kuongeza pato la nchi hii. Nchi kama Nigeria, Ghana na Senegal pato la Taifa linategemea michezo. Mchezaji mmoja leo hii anauzwa mpaka milioni 300, mchezaji mmoja tu. Sasa Taifa linapata kiasi gani? Lakini unapozungumza habari ya michezo watu hawakuelewi. Kwa hiyo, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizungumzia sana habari ya umuhimu wa Benki Kata na *SACCOs*. Sasa kuna sehemu ambazo zimeitikia ikiwepo Kilolo, sisi tayari tuna *SACCOs* zaidi ya 12 lakini hatujawezeshwa.

Nawashukuru sana watu wa *CRDB* ambao wamekuwa bega kwa bega kutusaidia, Mheshimiwa Waziri lakini nakuomba uweze kutuwezesha, maana yake kwa mfano sasa hivi pembejeo zile ambazo tumenunua, anayetoa mipoko ile ni *EXIM Bank* peke yake, sasa mtu wa Kilolo hata ile kufika *EXIM* ni matatizo. Sasa tungeweka utaratibu, angalau basi mmeamua kupeleka nguvu Iringa basi Iringa pale tuwe tuna Benki yetu ambayo mwananchi wa kule Kilolo aweze kuja kufuata pembejeo pale kwa kukopeshwa, utakuwa umetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, niungane mkono na Mheshimiwa Monica N. Mbega kuhusu wastaafu, kwamba waliopewa pesa za mkupuo kwa kweli angalau wafikiriwe, hali ni mbaya. Kwa hiyo, wapewe kwa mwezi hali ni mbaya sana.

Halafu pia na hawa wazee waliopigana Vita Kuu ya Pili. Wale wazee inawezekana wao baada ya kusikitika sana maana wapo, baada ya kusikitika sana hata

mvua zimeanza kukataa kunyesha. Sasa ni vizuri tukawafikiria ili kwa kweli waweze kutuombea kwa Mwenyezi Mungu ili mambo yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi. Pia niwapongeze kwa dhati kabisa Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili waliotoa hotuba zao hapa Bungeni, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda pamoja na Mheshimiwa Basil P. Mramba, kwa hotuba zao nzuri kabisa na niunge mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliojiunga ndani ya Bunge hili kwa kura za wananchi, niwapongeze wote kwa sababu hata wale walioingia kupitia Vyama vya Upinzani, ni matunda ya Chama cha Mapinduzi. Bila maamuzi mazuri ya Chama cha Mapinduzi wasingekuwa hapa, kwa hiyo ni lazima Chama cha Mapinduzi kijivunie kwamba ni matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ningependa niseme kwa ufupi yaliyojitokeza katika hotuba hizi mbili. Kwanza kabisa, imejitokeza ya kwamba ukuaji wa Pato la Taifa letu unaongezeka na ni lazima tupongeze Sera za Chama kinachotawala na utekelezaji mzuri wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, imejitokeza kwamba ukuaji wa pato la Serikali unaongezeka. Kama tunakumbuka katika miaka saba (7) iliyopita pato letu lilikuwa ni shilingi 25 bilioni kwa mwezi, sasa ni zaidi ya shilingi bilioni 100.

Kwa kweli ni lazima tuipongeze Serikali na tuwapongeze sana wenzetu wa *TRA* kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimpongeze sana Mkurugenzi ambaye hivi sasa hayupo, Ndugu Sanare, kwa kufanya kazi nzuri kabisa katika kipindi chake. Naamini amejenga misingi ya Shirika hili, misingi mizuri, misingi ya kujivunia. Vile vile napenda kumpongeza Ndugu Kitilya kwa kuchaguliwa kuongeza tena Shirika hili. Naamini atafanya kazi nzuri zaidi, atakwenda mbele. Serikali itaendelea kupata mapato hatutarajii turudi tena kuanza kukusanya mapato kidogo tunatarajia misingi hii iliyojengwa na Ndugu Sanare itaendelezwa na kazi nzuri itafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyo mbele yetu ni nini? Mimi naona kwamba pamoja na kuongezeka kwa pato la Taifa na pato la Serikali ni kuboresha maisha ya Watanzania. Kwa maana nyingine, ni kwa namna gani pato hili la Taifa na Serikali litaboresha maisha ya Watanzania? Hiyo ndiyo changamoto iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, niishukuru Serikali kwa maamuzi kadhaa ambayo imeyafanya katika bajeti hii. Moja ni kufuta karo za Shule za Msingi. Matokeo yake ni kwamba imepandisha *registration* ya wanafunzi wa darasa la kwanza kutoka

asilimia 56 mpaka zaidi ya asilimia 90. Ni lazima tuipongeze sana Serikali. Ni kazi nzuri na ya kujivunia. Pia katika bajeti hii tumeona kwamba ruzuku ya Elimu ya Sekondari kwa watoto wenye wazazi wasiojiweza imetolewa.

Hili ni jambo ambalo ni lazima tuipongeze sana Serikali. Pia Serikali itaendelea kugharamia Elimu ya Juu ya wanafunzi wetu. Maamuzi haya ni maamuzi ya maendeleo maana yake unapoelimisha watu kimsingi ndio unajenga msingi wa maendeleo kwa sababu maendeleo sio mali pake yake. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili, katika kipindi cha miaka minne iliyopita, nakumbuka hotuba moja ya Mheshimiwa Kasapira aliwahi kusema ni vizuri tufike mahali tuanze kupanga maendeleo ya nchi yetu kimaeneo na bajeti hii naamini imeanza kukidhi ombi hilo lililotolewa na Mheshimiwa Kasapira miaka minne iliyopita pamoja na Wabunge wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu sisi Wabunge wa Mikoa minne ambayo zamani ilijulikana kama *the big four* ukiangalia maswali na hotuba zetu kilio chetu kilikuwa mbolea. Kwetu sisi Mikoa hii minne unapozungumzia mbolea maana yake unazungumzia uhai wetu. Kwa hiyo, kwa kweli nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutoa ruzuku katika mbolea. Nina taarifa kwamba pesa zilizopangwa kwa ajili ya mbolea ni pesa za kutosha na naitafsiri bajeti hii kama imetoa jukumu maalum kwa Mikoa hii minne kuzalisha chakula (nafaka).

Mheshimiwa Spika, ili tafsiri yangu iwe sahihi au malengo haya yafikiwe, ninayo maoni yafutayo. Fedha hizi zilizotengwa, naambiwa ziko kama bilioni sita zitumike katika ruzuku ya mbolea peke yake. Nasema hivi kwa sababu katika bajeti za nyuma Serikali imejitahidi sana kuwasaidia wakulima wa nafaka katika nchi yetu. Lakini kila nafuu ilipokuwa inatolewa imekuwa ikitekwa na wafanyabiashara wachache wajanja. Sasa hili naliona kama ni tatizo kubwa. Sasa safari hii Serikali imetenga fedha za kutosha, nadhani lazima utolewe utaratibu ambao utamhakikishia mkulima wa chini kabisa, wa kijijini bei ndogo ya mbolea maana yake ndio mlengwa katika bajeti hii. Mlengwa hapa sio mfanyabiashara ni mwananchi wa kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbolea katika Mikoa hii minne yanakadiriwa kufikia tani kati ya 50,000 - 60,000 kwa mwaka. Mbolea hii gharama yake ya dukani ni kama shilingi bilioni kumi. Serikali imetoa bilioni sita ruzuku maana yake ni nini? Kwa tafsiri ya haraka haraka ni kwamba bei ya mbolea itapungua zaidi ya nusu ya bei iliyopo sasa. Haya ndio matarajio yetu kwamba bei ya mbolea kutoka Sh.8,000-9,000 bei ya sasa madukani tunatarajia itakuwa kati ya Sh.3,000-4,000 ndio matarajio yetu na ndio liwe lengo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia nchi yetu katika rekodi zake tuliwahi kufikia matumizi ya mbolea tani 260,000 kwa mwaka kati ya miaka 1988-1992. Sasa hivi matumizi yetu kwa hotuba ya mwaka jana ya Waziri wa Kilimo ni tani 140,000 maana yake ni kwamba tunatumia mbolea kidogo zaidi. Unapozungumzia kilimo nchi yoyote mtu atakuuliza ebu nipe takwimu zako za matumizi ya mbolea. Hata kabla hajaenda

shambani anafika Ofisini kuangalia takwimu zako za matumizi ya mbolea. Sasa ni matarajio yangu kwamba kupungua kwa bei ya mbolea kutokana na ruzuku iliyowekwa na Serikali matumizi ya mbolea ndani ya nchi yataongezeka na uzalishaji wa nafaka utaongezeka na tutaachana na hili tatizo la nchi kulia njaa, njaa imepata uhuru miaka 40 iliyopita kila siku tunazungumzia njaa, njaa, kwa nini? Hakuna sababu. Gharama yenyewe ya mbolea kama nilivyosema matumizi yetu ndani ya nchi hayazidi shilingi bilioni 25 mapato ambayo kwa Serikali ni ya wiki moja tu. Kwa hiyo, naamini kabisa tatizo la mbolea katika nchi yetu tutakuwa tumelimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia yako mambo ambayo tumeishauri Serikali siku nyingi na naomba hili pia Serikali ilione kwamba katika miaka ile ambayo tulikuwa tunazalisha nafaka kwa wingi tulikuwa na tatizo kubwa la soko. Nisingependa kufika huko na ili tusifike huko basi ningeshauri Serikali ijaribu kuangalia uwezekano wa kuunda Bodi ya Nafaka ili mwaka ambao tunakuwa na nafaka nyingi tusiwe na sababu ya kuruhusu uagazaji holela wa nafaka kwa sababu ndani ya nchi yetu tunakuwa na nafaka za kutosha. Hii itatoa nafasi kwa mazao yanayozalishwa ndani ya nchi kuuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali itumie yale maghala ambayo yapo sasa hivi kwa kuhifadhi nafaka. Naamini kwamba nchi ikiwa na upungufu wa chakula wafanyabiashara wanaweza kukidhi mahitaji lakini nchi ikiwa na njaa, naamini hakuna mfanyabiashara atakayekwenda kule kwa sababu njaa inafunga milango ya kuuza na kununua. Njaa ni jambo kubwa na nchi ikiwa na njaa itakuwa ni jukumu la Serikali kulisha wananchi wake. Kwa hiyo, bado naamini maghala mengi ambayo yaligharamiwa na Serikali hii kujengwa ni vizuri zikatumika kwa tahadhari ya Taifa linapokuwa limepata uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni juu ya hatari kubwa ambayo sisi wananchi wa Iringa na Morogoro tunakabiliwa kutokana na madhara yanayoweza kujitokeza katika Kiwanda cha Karatasi *SPM Mgololo.* Jambo hili naamini tumelizungumza kwa urefu kabisa na Serikali inaelewa kwamba pale kuna matanki ya sumu yanayoweza kuhatarisha maisha ya wanadamu na wanyama kwa maelfu. Sasa tumekuwa tukiomba Serikali ikiwashe kiwanda kile kiendelee kufanya kazi. Kwa bajeti ya mwaka jana, Serikali ilisema kwamba haina fedha. Naamini kwa bajeti ya mwaka huu Serikali itakuwa na fedha ya kukiwasha kiwanda kile zinatakiwa Sh. 2.8bln ili kiweze kufanya kazi. Kiwanda kile kikiachwa kama kilivyo madhara yake yatakuwa ni ya historia kwa Afrika. Kwa sababu tunaelewa sidhani kama Serikali yetu itatufikisha hapo. Kwa hiyo, naomba hizi fedha ambazo zimeombwa kwa utaalam kutoka katika kile Kiwanda cha *SPM Mgololo* ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, tunaendelea kuiomba Serikali iendelee na juhudi za kukibinafsisha kiwanda kile. Kiwanda kile kiko katika mazingira mazuri kuna msitu mkubwa kabisa wa hekta zinazofikia 42,000 naamini ni *potential* nzuri au ni kivutio kikubwa kwa wawekezaji ambao wanaweza kuzalisha karatasi katika kiwanda kile.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kusema jambo moja kwa ufupi kwamba kwa kweli pamoja na nafuu iliyotolewa ya gharama ya umeme katika viwanda vikubwa bado nafuu hii haitoshi. Ni vizuri Serikali ikaangalia tena gharama ya umeme kwa viwanda vinavyotumia umeme mwingi. Gharama hii bado ni kubwa haijatoa unafuu wa kutosha kuvutia uwekezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni vizuri TAMISEMI sasa wakaangalia vizuri matumizi ya fedha zinazopitia katika mfuko wao. Ziko barabara ambazo ni za Kitaifa lakini bado zimeachwa katika Halmashauri na Halmashauri hizo haziwezi kuzihudumia barabara hizo. Barabara mojawapo ni ya Nyigo - Mgololo inayokwenda katika Kiwanda cha *SPM Mgololo.* Ni barabara yenye urefu wa kilomita karibu 70. Barabara ile haiwezi kutengenezwa na Wilaya na kwa kweli itakuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa wawekezaji kwa sababu mahali penyewe hapafikiki kwa sababu ya ubovu wa barabara hii.

Si sahihi hata kidogo barabara muhimu zinazokwenda katika maeneo muhimu ya uchumi wa nchi kuachiwa Halmashauri. Mimi nadhani barabara hizi ni vizuri zikachukuliwa na Taifa ili kweli ziweze kuhudumiwa ipasavyo ili ziwe ni vivutio vya uwekezaji katika nchi. Kwa sababu kama umejenga kiwanda mahali ambapo hapafikiki kwa urahisi nadhani kiwanda hicho kinakuwa na matatizo mengi na kinakuwa ni kikwazo cha kuwavutia wawekezaji katika nchi yetu. Naamini kabisa kwamba suala la barabara muhimu kama Nyigo - Mgololo inayokwenda katika Kiwanda kikubwa kabisa cha Karatasi katika Afrika itachukuliwa na Serikali Kuu badala ya kutegemea fedha kidogo zinazopelekwa katika Halmashauri yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naamini huo ni mfano, naamini nchi yetu ina barabara nyingi za namna hii. Kwa hiyo, katika ule mfuko unaopitia TAMISEMI ziwepo fedha zinazokwenda katika Halmashauri lakini ziwepo fedha zinazobaki katika mfuko wenyewe kwa ajili ya kuhudumia barabara zake muhimu moja kwa moja. Wizara ya Ujenzi imezigawa barabara zake katika mafungu matatu makubwa. Ziko barabara za Kitaifa, barabara za Mkoa na barabara muhimu za vijiji. Kwa hiyo, ni vizuri na mfuko huu pia ukazipanga barabara kutokana na umuhimu. Nadhani itakuwa ni makosa kufikiria kwamba barabara zote zina umuhimu unaofanana. Nadhani ni makosa ya kiuchumi kwa sababu kuna barabara nyingine zina *economic return.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

MHE. ABU TOWEGALE KIWANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii ya kuchangia kwenye Bajeti hii ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani kutoka Jimboni kwangu kwa Serikali kufuta Kodi ya Maendeleo na kero nyingine za kodi ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kutupokea sisi Wabunge wapya kuungana na ninyi kwenye jukumu hili zito na nyeti la kutunga sheria kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa nidhamu kama sitashukuru Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi na Halmashauri Kuu kwa kurudisha jina langu ili niwe mgombea wa Jimbo la Kilombero kwenye Uchaguzi Mdogo uliopita. Nashukuru, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kuweza kukipigia Chama cha Mapinduzi na hatimaye kupata ushindi dhidi ya Vyama vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nina deni kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi ngazi zote, Taifa, Mkoa, Wilaya, Kata hata kwenye Shina kwa kuhakikisha ushindi unapatikana kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Wabunge wa Jimbo la Kilombero kwa mchango wao mkubwa wa hali na mali kwenye Uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza pia Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri ambapo wameelekeza kuondoa umaskini katika nchi yetu wakijaribu kabisa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kuchangia sehemu ya kilimo. Naamini kabisa kwa nia njema Serikali imeamua kutoa ruzuku za pembejeo kwa Mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Iringa na Mbeya lakini naamini kabisa siku za usoni wakiliangalia pia na Jimbo la Kilombero kwa sababu halihitaji mbolea na uwezo wake mkubwa kwenye kilimo na umwagiliaji nadhani tatizo la njaa pia linaweza kuondolewa. Kilombero ina hususani ukubwa wa hekta milioni moja mia mbili ishirini na nne. Ardhi ambayo inaweza kulimika na ina uwezo wa kumwagilia upatao hekta laki tatu na thelathini na sita. Naamini kabisa Serikali ikitoa unyonge wa watu kujikwamua na umaskini basi itakuwa na uwezo wa kuzalisha chakula kwa ajili ya manufaa yao wenyewe na kuchangia pato la nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusiana na uwekezaji. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumzia kufupisha kikomo cha muda wa miaka mitano kwa wale wawekezaji. Ninaamini amefanya hivyo kwa nia njema kabisa kwa sababu watu hawa wameshaingia. Lakini naomba kwenye michanganuo itakayokuja baadaye kwa hao watakaokuja kuwekeza taasisi husika pamoja na *TRA* wachunguze michanganuo hiyo vizuri ili kosa hili lisirudiwe tena. Jukumu la Serikali yetu ni kuwakwamua wananchi wetu, wanyonge wetu sio wanyonge wa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napenda kuchangia ni juu ya bajeti yenyewe. Kwenye vyanzo vya mapato nilivyoangalia kwenye hotuba Mwaka 2002/2003, Kodi ya Mapato ilipangiwa ichangie 22%, *VAT* ichangie 13% na Ushuru wa Forodha

ichangie 42%. Matokeo halisi ni kuwa *Income Tax* imechangia 25.3%, Ushuru wa Forodha 39.4% na *VAT* 15%. Sasa ninavyoona kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004 mchango huo unafikia 73% badala ya 77% iliyopangwa mwanzoni. Tunajenga uchumi wa kujitegemea sasa lengo la kurudisha mpaka 73% kidogo naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha akarabati Bajeti hiyo kwa sababu kama uchumi wetu ni wa kujitegemea na hasa baada ya kufuta kodi hivyo kurudi nyuma ni kukiuka kidogo taratibu za Bajeti ambazo zinataka malengo ya Bajeti yasiwe chini sana au yasiwe juu sana ili yaweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, sidhani kama nina la zaidi la kuzungumzia ila tu kusisitiza kwenye lile la mwanzo pindi Serikali itakapoweza kutoa msaada kwenye sekta ya kilimo kuboresha barabara zake. Barabara za Kilombero ni mbaya.

Ninaomba kwa taratibu zote na kwa njia za haraka tupatiwe barabara ya lami kutoka Kidatu - Ifakara - Masagati- Mlimba - Uchindile sehemu ambazo zina uwezo mkubwa wa kilimo. Ilovu ambayo ilichukua *Kilombero Sugar* hivi sasa imeshaweka uzalishaji wa kutosha kufikia tani 100 na Serikali imeshawapa ardhi hekari nyingi tu iweze kuzalisha ili hapo baadaye waweze kufikisha tani 200 hiyo sehemu inaitwa Lipa kwa hiyo kuna kila sababu ya Serikali kufikiria kujenga hii barabara kwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tukumbuke kuwa Mgodi wa Umeme wa Kihansi uko Mlimba, Kilombero. Kwa hiyo, kutokana na uwezo wa *Kilombero Sugar* na Mgodi wa Kihansi na hali ya hewa, ninaomba barabara zikarabatiwe ili kilimo kiweze kuinuka na watu wangu waweze kuondokana na umaskini. Ninasema Serikali imewanyong'onyeza watu wangu sio kama ni wavivu wa kuzalisha, hapana uwezo huo ukitolewa watazalisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba niunge mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutofautiana kidogo na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu toka nifike nilikuwa na wasiwasi labda pengine kutaja jina la Mwenyezi Mungu humu ndani ni kosa, kumbe sivyo hasa nilipoangalia kile kiapo mwisho unamalizia kusema Mwenyezi Mungu nisaidie. Nasema hivyo kwa sababu naona Waheshimiwa Wabunge kila anayesimama huwa anasahau kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu. Nilikuwa na wasiwasi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza nataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuamka salama, nikawa mzima na nikawa na uwezo wa kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, sasa nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuniona na kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ufafanuzi kidogo kabla ya kuanza kuchangia. Kuna hili suala limekuwa likizungumzwa sana la huyu Ruhani.

MBUNGE FULANI: Nani?

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba katika sisi Wabunge suala hili la Ruhani hakuna. Suala la Ruhani liko katika viti sita upande wa Wawakilishi kwa upande wa Zanzibar. Sasa Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi na suala la Ruhani sisi Wabunge sote ni safi, wazima hatuna tatizo la Ruhani.

Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi, hamna tatizo. Hata Mheshimiwa Spika, wakati tunatoka alinitania akaniambia aah hii ni ninyi Ruhani mliosababisha umeme kukatika, hapana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Lakini kabla sijachangia, naomba sana Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie hasa sisi Wabunge wapya labda pengine naweza nikateleza unaweza ukasikia aah utaratibu, utaratibu, hii kwa kweli kwa mara ya kwanza naomba sana Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika hata nikiteleza basi mvumilie kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Spika atakulinda. *(Kicheko)*

MHE. ALI SAID SALIM: Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Kifungu cha 34(1) ambacho kiko kwenye ukurasa wa 29. Hapa imesemwa kwamba katika kipindi hiki Serikali itakuwa inatoa kiasi fulani cha fedha za misaada kutoka nje kuipa Serikali ya Zanzibar. Napenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu nchi yetu ya Zanzibar ni nchi ambayo hali ya uchumi wake iko chini sana na hali ya wananchi wetu kimapato na matumizi kwa kweli iko chini sana.

Kwa hiyo, naipongeza Serikali lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie tena kwa sababu hiki kiasi ambacho kimetajwa humu cha 4.5% ni kidogo mno. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri angalau uongeze kidogo ili kuisaidia Serikali ya Zanzibar. Ni Serikali yenu ya CCM sio ya *CUF* lakini wananchi watakaoneemeka watakuwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuchangia na hapo hapo umesema hii ni katika azma ya kutekeleza muafaka, nashukuru sana. Sasa twende na azma hii hii ya kutekeleza muafaka, utakumbuka kwamba Mheshimiwa Rais wa Tanzania aliunda Tume ya Kuchunguza matukio ya tarehe 26-27 Januari, 2001. Tume ikaja Pemba ikafanya kazi baadaye ikapeleka ripoti yake. Katika ripoti ile na kwa mujibu wa muafaka, imeelezwa kwamba walioathirika watapewa fidia na ilielezwa kabisa katika muafaka ule kwamba sio zaidi ya tarehe 31 Desemba, 2002.

Sasa lililonitia wasiwasi kidogo na kunivunja moyo ni kuona kwamba katika bajeti hii sioni kasma yoyote iliyotengwa na Serikali ya Muungano ili kuwasaidia watu hawa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie suala hili. Kwa kweli watu

walioathirika wapo na wako katika hali mbaya sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri Jumapili hii tufuatane naye twende Pemba akijionee mwenyewe hawa yatima, vilema walivyoathirika siku moja Jumapili asubuhi jioni tunarudi naamini tukienda tukirudi, Mheshimiwa Waziri atatafuta pesa popote watu wale waweze kufikidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya kujenga Ukumbi mpya wa Bunge. Kwa mawazo yangu, nafikiri kuna kitu muhimu zaidi tungeweza kufanya kwanza kabla ya kuongeza ukumbi huu kwa sababu ukumbi huu tulionao hivi sasa pamoja na akina mama juzi kusema kwamba kuna 30% yao haijakamilika sasa ikikamilika ukumbi utakuwa mdogo lakini mimi naona kwa hiyo haja nitakayoitaja sasa hivi tungeweza kutekeleza haja hiyo ili hiyo asilimia 30 basi tukaongeza kiti kimoja kimoja upande huu huku mpaka juu na huko kimoja kimoja mpaka juu ili fedha hii iende katika hayo madhumuni nitakayoyasema. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhumuni yenyewe ni kupendekeza kwanza litafutwe eneo hapa Dodoma la pamoja ili ziweze kujengwa nyumba kwa ajili ya Wabunge. Hii itasaidia kiusalama. Sasa hivi Wabunge wamechanganyika kila mahali sisi tumechelewa bahati mbaya tumekuja tumepata kihoteli kimoja ucharwa, uchwara tu pale hakina usalama wowote. Sasa kwa kweli kama Serikali itaweza kujenga nyumba za pamoja kwa Waheshimiwa Wabunge hata kudhibiti usalama wao itakuwa ni rahisi. Juzi nimesikia kuna baadhi ya Wabunge waliingiliwa wakaibiwa pesa, sijui kama ni kweli au vipi lakini habari hiyo mmeisikia. Kwa hiyo, kama tutakuwa na majengo ya pamoja, nafikiri tatizo hili la kuibiwa haliwezi kutokea. Kwa hiyo ikiwezekana suala hili ulitazame ili tuweze kuongeza kiti kimoja kimoja huku na huku ili akina mama hawa waweze kupata nafasi katika Bunge lijalo 2005. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri amesema fedha za maendeleo kwa Halmashauri za Wilaya zitakuwa zinakwenda moja kwa moja katika Halmashauri husika kuliko utaratibu wa zamani ambapo zilikuwa zikipitia kwenye Mikoa.

Mheshimiwa Spika, napongeza utaratibu huu kwa sababu utaondoa urasimu hapa katikati lakini natahadharisha Mheshimiwa Waziri kwamba ni vema ukaandaliwa utaratibu mzuri ili kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumiwa kwa azma iliyokusudiwa vinginevyo kama utaratibu mzuri hakuandaliwa ili kuhakikisha fedha hizi zinatumiwa kwa mambo yaliyokusudiwa tutashtukia fedha hii imefikia mikononi mwa watu wachache na azma nzima ya Serikali itakuwa haina faida yoyote.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni ushuru wa simu za mkononi. Simu za mkononi si jambo la *luxury* ni huduma ya lazima na ni sehemu ya maendeleo. Sasa hivi simu za mkononi wakulima wa kawaida tu wanakuwa nazo, wavuvi na watu wengine. Kwa kuwa ni huduma ya kijamii na ni sehemu ya maendeleo, nadhani Mheshimiwa Waziri angetafuta sehemu nyingine ya kuongeza ushuru ili huku ukafutwa kabisa kabisa ukapelekwa kwenye vinywaji baridi, vinywaji moto na sigara. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kuwa muda japo kama unatosha lakini sina la ziada, sisemi kwamba naunga mkono sasa hivi, isipokuwa nitaunga mkono Bajeti hii baada ya kupata ufafanuzi mzuri wa haya ambayo nimeyazungumzia, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa asubuhi hii inatosha. Kama nilivyosema Mheshimiwa Aridi atakuwa wa kwanza na Mheshimiwa Esther Nyawazwa ajiandae kufuatia. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 06.46 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza jioni hii ili na mimi nichangie hoja za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wabunge wote wapya ambao wamejiunga na Bunge lako Tukufu baada ya chaguzi ndogo ambazo zimefanyika mwezi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue vile vile nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri sana za bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niwapongeze Manaibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara za Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba za bajeti za Wizara hizo ambazo zimewasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu wiki iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza kwenye vifungu vichache vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwenye huduma kwa mazao. Serikali imesema itazitaka Wilaya kuteua zao moja la biashara na zao moja la chakula ili yapewe msukumo maalum kupitia bajeti yake kwa kupata pembejeo, mbolea na madawa ya kuulia wadudu na kutiba magonjwa ya mazao. Naomba Serikali iwe makini katika suala hili kwa sababu nina uhakika itasaidia sana katika kupiga vita umaskini hasa kwa wananchi walioko Vijijini na vile vile kuongeza pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa zao la korosho ambalo linalimwa katika Mikoa isiyopungua sita hapa nchini. Mkorosho mmoja ambao umetunzwa vizuri kwa kupaliliwa mapema na kupuliziwa dawa kama inavyotakiwa mkorosho huu umeonekana kutoa korosho zaidi ya kilo hamsini mahali pengine. Sasa kwa mfano, kwa Wilaya ya

Masasi sisi tuna mikorosho milioni tano, ikiwa kila mkorosho basi utatoa kilo hamsini Wilaya ya Masasi ina uhakika wa kupata kilo milioni mia mbili hamsini. Ukichukua bei ya korosho kwa kilo moja hivi sasa ya shilingi 360/= basi Wilaya ya Masasi ina uhakika wa kupata shilingi bilioni tisini kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Lakini kwa kukosa huduma nzuri sasa hivi Masasi inazalisha kilo milioni kumi na nane peke yake. Kwa bei ya shilingi 360/= kwa kilo Masasi inapata shilingi bilioni sita mia nne themanini milioni. Kwa hiyo hapa tunaona tofauti kubwa kati ya mkorosho ambao umetunzwa vizuri na mkorosho ambao haujatunzwa vizuri. Kwa hiyo kuwawezesha wakulima wa korosho kupata pembejeo za kuhakikisha mikorosho yao wanaipulizia kama inavyotakiwa ni dhahiri kuwa pato la Taifa litaongezeka na wakulima wa korosho wataondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza awali kuwa korosho hulimwa katika Mikoa isiyopungua sita hapa nchini. Haya ambayo nimeyasema kwa Masasi nina uhakika hali ipo hivyo hivyo katika Wilaya za Newala, Tandahimba, Nachingwea, Lindi, Tunduru, Mtwara Vijijini na sehemu zingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, ikiwa mikorosho yote nchini itafufuliwa nina imani kuwa Tanzania ndani ya kipindi kifupi inaweza ikazalisha korosho kiasi cha tani laki tano na kuendelea. Naomba Serikali iwe makini katika suala hili, wananchi wakulima wa korosho wapo tayari, sana sana wanachokosa ni pembejeo lakini wanajua kuwa umaskini wao utaondoka kutokana na zao la korosho. Kwa hiyo mimi nina hakika kabisa kwa Wilaya yangu ya Masasi korosho ndilo litakuwa zao ambalo litachaguliwa.

Mheshimiwa Spika, manufaa hayo tena yataongezeka zaidi ikiwa suala la ubanguaji korosho nchini nalo litatiliwa mkazo na Serikali. Kwa hiyo naomba pamoja na kuhakikisha uzalishaji wa korosho unaongezeka lakini vile vile korosho hizi nazo zibanguliwe zote nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo, sasa niende kwenye suala la kodi ya maendeleo. Kuhusu kufutwa kwa kodi ya maendeleo naishukuru sana Serikali kwa hatua hiyo muhimu. Lakini bado kuna umuhimu wa kuona maendeleo yanakuwepo kwenye Wilaya zetu. Tumehakikishiwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa pengo litakalotokana na kufutwa kwa kodi ya maendeleo Serikali italifidia. Hata hivyo mimi sikubaliani na *formu* la itakayotumika kufidia pengo hilo kwa sababu amesema yataangaliwa makusanyo ya miaka mitatu na kutafuta wastani ndiyo utakaofidiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza kuwa yaangaliwe makusanyo ya juu kwa kipindi cha miaka mitano au kumi iliyopita, sasa yale ambayo yalikuwa makusanyo makubwa zaidi ndiyo yafidiwe. Lakini kwa kuangalia makusanyo ya miaka mitatu inawezekana kutokana na hali mbaya ya hewa Wilaya zikashindwa kukusanya kodi kutoka kwa wananchi wake, lakini kwa miaka kumi nina hakika kuna mwaka ambao makusanyo yalikuwa makubwa zaidi. Kwa hiyo, yale makusanyo ndiyo yafidiwe kwenye Wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekee kwenye suala la njaa. Ni kweli kuwa Tanzania mwaka huu inakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula au njaa. Wilaya yangu ya Masasi ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimekumbwa na upungufu huo wa chakula. Upungufu huo wa chakula umetokana na ukame uliosababisha mazao mengine kukauka. Lakini vile vile katika Kata zingine ndani ya Wilaya yangu umetokana na uharibifu au tatizo la wanyama waharibifu hasa yale maeneo ambayo yanapakana na mbuga za wanyama. Kwa hiyo, wananchi walijitahidi kulima, tena kule kwetu tulikuwa na kampeni ya ONJAMA lakini sasa ile mihogo ambayo ilipandwa imekauka na kinachoonekana ni mizizi tu ambayo haiwezi kuvunwa. Kwa hiyo, nasema Serikali ijiandae kusaidia haraka sana tatizo hili la upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba na mimi nitamke kuwa ninaunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja. Lakini mwisho nikushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi hii na vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuchangia hoja mbili zilizopo mbele yetu. Ili nisije nikasahau naomba niunge mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge walioingia hivi karibuni katika Bunge letu hili Tukufu. Nilikuwa naomba tu waje kuwakilisha wananchi, wao malumbano ya kisiasa yawe nje ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda wa Mipango na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba wa Fedha. Hotuba zao zote mbili ni nzuri, zinaeleweka na kila Mtanzania mwenye uelewa ameipokea kwa furaha nyingi sana. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kujielekeza katika bajeti hii kuhusu kilimo. Nashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wamelenga hasa hasa kitu muhimu ambacho Watanzania tulitegemea kukusanya kodi tu, kilimo tulikiacha mbali sana. Kwa Bajeti hii kama kweli tutakuwa na mshikamano, sekta zote zishirikiane na Mheshimiwa wa Mipango na Waziri wa Fedha ambaye ametenga kiasi kikubwa kwa ajili ya kilimo nafikiri Tanzania itakuwa nchi mojawapo ambayo haitakuwa na njaa tena. Hivyo, nilikuwa naomba katika suala la kilimo tusiwaachie hawa Mawaziri wawili, lazima tuwe kama treni. Kichwa kiwe ndiyo Waziri wa Mipango, mabehewa yawe viongozi, sisi Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mabwana Shamba na Mabibi Shamba, Maafisa Mipango wote na Watendaji wote ambao wanashughulika na kilimo. Tusipowaunga mkono wenzetu tutakuwa tunajadili tu kilimo, lakini hatutafika popote. Lazima sasa kuwe na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa bajeti itakapopita tuhakikishe kwamba uwajibikaji unafuatiliwa. Kila mtu awajibike kwenye eneo lake. Hivyo lazima sasa kama sisi viongozi Wabunge tuwaeleze wananchi wetu kila mtu afanye kazi. Inasikitisha unafika asubuhi unakuta vijana wenye nguvu ambao wanategemewa na Taifa hili

wanacheza karata asubuhi, hawana kazi yoyote ya kufanya wakati tuna mabonde makubwa sana ambayo yanatakiwa kulimwa.

Tuwe na mpangilio tu mzuri ambao utawawezesha hawa vijana na akina mama ambao wana uwezo wa kulima wakalima mashamba hayo ili Tanzania kwa kweli tuwe hatuna njaa wala umaskini ambao tutakuwa hatuuzungumzii tena. Hivyo naomba sana tuwahamasishe watu wetu Watanzania, tuone kilimo ndiyo kazi yetu ya kujiajiri, tusisubiri tu kuajiriwa maofisini.

Mheshimiwa Spika, hivyo nilikuwa naomba Mkuu wa Mkoa ahakikishe kila mtu kwenye Mkoa wake anawajibika. Mimi huwa natoa mfano wa Mheshimiwa Mzindakaya, samahani sana naona hayupo huwa napenda kumtolea mfano. Alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, aliweka kambi ya kilimo, je, hiyo nafasi ya Mkuu wa Mkoa imekwisha, si bado wapo Wakuu wa Mikoa kama Mzindakaya? Hii ni tabia ambayo alikuwa anaifanya Mzee Mzindakaya, watu sasa wahamie kwenye maeneo ya kilimo, wasikae mezani tu wanaandika mikakati na mipangilio, lakini hawafuatilii. Hivyo naomba sana Watanzania wote vijana, sisi akina mama tupo tayari, tukafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie jambo lingine kuhusu elimu. Mheshimiwa Dr. Kigoda ameelezea katika ukurasa wa 32, napenda kutoa pongezi nyingi sana kwa Serikali yetu kwa kuongeza asilimia kwa wasichana kuendelea na kidato cha tano. Lakini idadi hiyo kweli bado ni ndogo kwa sababu wanafunzi wa kike waliachwa nyuma sana. Kwa hiyo, ni ombi langu tena nalileta kwa Serikali yetu Tukufu izidi kutufikiria, kwanza shule ni chache, wanafunzi walikuwa hawachaguliwi kwa uchache wa shule. Kwa mfano, mimi Mkoa wa Mwanza nina shule mbili tu za wasichana ambazo ni Bwiru na Ngaza. Aidha watoto wa kike wamezaliwa wengi na wana akili nzuri. Hivyo nilikuwa naomba Serikali iendelee kutufikiria.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuchangia, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye ukurasa wa 42 (v) amezungumzia kwamba kuna wanafunzi 6019, walifaidika na mfuko wa kusomeshwa. Sasa nitapenda Mheshimiwa Waziri anisaidie, walitumia vigezo gani? Hawa watoto yatima wa Vijijini wamo au nafasi 6019 zimechukuliwa na watoto wa Mijini? Hivyo nilikuwa naomba tuwe tunaangalia na uwiano kwa watoto wetu wa Vijijini, kuna watoto Vijijini wana akili sana, lakini unakuta wapo mbali na Makao Makuu ya Wilaya, wapo mbali na watu wa kuwasaidia, wanakosa kujiendeleza ipasavyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba huu Mfuko ambao umetengwa na Serikali, basi uwe na uwiano, asilimia ngapi ziende Mjini na ngapi ziende Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba vile vile nizungumzie suala la nishati. Watu wengi sasa hivi na sera yetu ya Chama cha Mapinduzi imesema kwamba tuhakikishe umeme unafika Vijijini. Inaniwia vigumu sasa kuridhika na uamuzi huo wakati sasa watu wanatamani sana wawe na umeme, lakini nasikia sasa hivi kuna upungufu wa nguzo. Sasa sijui na ninaambiwa kwamba nguzo hizi zinatoka Afrika ya Kusini huko Malya zitafika kweli au miti yetu Tanzania imekwisha mpaka tunaagiza kutoka nchi za nje? Je, Tanzania yetu kweli imefikia mahali hatuwezi kupanda miti kama hiyo ya nguzo za umeme, mpaka tunaagiza nchi za nje? Ndiyo watu wapate

umeme? Ninakuwa na wasiwasi sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili tuliangalie kwamba sasa kama kweli tunataka watu wetu wapate umeme tujaribu kupunguza basi hata malighafi zetu za nchini hapa zitumike na watu wetu waweze kuuza miti yao kwa ajili ya kuleta umeme.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la ulinzi na usalama. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani, vijana wetu Polisi wamefanya kazi nzuri sana. Lakini kazi nzuri hii wameifanya labda baada ya kuona wameuawa, hili nazungumza kwa masikitiko kwa sababu majambazi walikuwepo. Tulizembea kwa kweli Tanzania, tuliona askari wetu labda hawakuwajibika ipasavyo. Bahati mbaya sana majambazi yamekuja kuwazoea mpaka wamekuja kuwaua. Lakini sasa kwa kazi nzuri wanayoifanya na ninaipongeza Wizara ya Fedha kuwatengea fedha nyingi sana. Hivyo nilikuwa naomba kutumia nafasi hii kuwaomba vijana wetu wafanye kazi vizuri.

Lakini Mheshimiwa Spika, hapo hapo natahadharisha Watanzania wenzangu haya matukio yanayojitokeza. Majambazi tena kutoka nje yameua askari wetu. Vijana wameandamana, watu wakachoma bendera na Serikali haijasema chochote. Sijasikia Serikali imesema kitu chochote. Kama dini nazo zinaingia kwenye mambo ya kisiasa sijui. Ninafikiri dini ni kuabudu Mungu ili kuwapunguzia watu dhambi. Inakuwaje kundi la watu wa dini fulani linafikia mahali kuchoma bendera ya nchi fulani. Tanzania tunasema nini? Hilo nilikuwa naomba katika ulinzi na usalama tuwe makini kwani hili tunaweza kuliangalia tu lakini baadaye litatuletea matatizo zaidi. Hivyo naomba vijana wetu wawe makini wakati wowote kwa sababu huko tunakoelekea siyo kuzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda sasa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mramba. Nampongeza sana kwa kutujali sisi wanawake. Amemteua Mhasibu Mkuu mwanamke. Sisi wanawake hatuombi vyeo kwa kuomba tu ila uwezo tunao, akili tunazo, kwa hiyo Mama Blandina Nyoni hakupendelewa na mtu yeyote. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mramba, kwa kuona kwamba uwezo tunao wa kusimamia fedha za Serikali ziweze kutumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TRA* wanafanya kazi nzuri sana, wanakusanya fedha nyingi na ambao ndiyo tulikuwa tunawategemea sana kupandisha uchumi wetu wa nchi hii. Kwa hiyo, naomba *TRA* kukusanya fedha zetu ili Tanzania na sisi tuonekana kwamba tunajali makusanyo ya kodi zetu. Hivyo nilikuwa napenda kuomba mwanamke mwenzetu asiletewe majungu kwa sababu ni mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tabia mtu akifanya kazi nzuri watu wanakuzunguka, wanakuja kuleta maneno amefanya hivi na hivi. Lakini nilivyokuwa na imani kwa Mama Nyoni kwa kazi ambayo ameionyesha na *system* nzuri aliyofunga pale, nakuomba sana Mheshimiwa Mramba umwone huyu kwa jicho la husuda. *(Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Asimwone kwa jicho la husuda.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Usimwone kwa jicho la husuda. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mramba umwone kwa jicho zuri, naomba nirekebishe kwa jicho zuri kwa sababu anafanya kazi vizuri na atasimamia fedha za Serikali yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, napenda niwashukuru sana Waziri wa Fedha kwa kufuta kodi ya maendeleo. Kila mtu aliyesimama hapa kuchangia juu ya kero, kero kubwa ilikuwa kwa akina mama. Nasikitika Mheshimiwa Mchemba alisema hakuna redio za usiku, kuna redio za usiku, redio mbao. Ilifikia kipindi nitawasemea wenye ndoa za halali, sisemi ndoa ambazo za kujificha ficha. Ilikuwa inafikia wakati Vijijini mtu sasa mchana kutwa amefanya kazi, sasa wanakutana nyumbani, watoto wameshalala, wanataka kufungua kipindi maalum, unasikia mlango unagongwa ngo ngo ngo, kodi kodi inabidi mama amchukue baba amweke darini.

Kwa hiyo, ilikuwa ni kazi ngumu kwa sisi akina mama kuficha waume zetu darini. Kwa hiyo, hili wanawake wamefurahi sana. Kwa hiyo, tunashukuru sana na akina mama wote wanalipokea hili kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nilikuwa naomba basi nihitimishe kwa kumwomba Mheshimiwa ambaye atakuja kwenye sekta ya barabara anisaidie maana tuna sera ya kutengeneza barabara ili tufungue mawasiliano ya Wilaya kwa Wilaya. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa atakapokuwa kwenye bajeti yake ya ujenzi anisaidie kunieleza barabara ya Malampaka, Malya, Mwahalanga, Bukwimba, Sumve, Koromije kwenda Kisesa atusaidie watu wa maeneo yale ili tuweze kusafirisha mazao yetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hizi kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, naomba nami nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo ili niwe mmoja wa wachangiaji katika hotuba hizi mbili za Mawaziri wa Fedha na Mipango. Kabla ya yote niwapongeze Wabunge wapya ambao wamejiunga nasi hivi karibuni kufuatia chaguzi ndogo zilizofanyika mwezi wa tano. Naomba niwakaribishe sana Bungeni, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa niwapongeze Mawaziri hao wawili kwa jinsi walivyotayarisha Bajeti zao na jinsi mipango ilivyotayarishwa kwa sababu leo nadhani manung'uniko ni madogo kuliko miaka yote iliyopita ambapo sasa tunao mpango mzuri na Bajeti nzuri na ninaweza nikajumuisha kwamba Bajeti yetu ni Bajeti inayomjali Mtanzania. Ni Bajeti rafiki kwa watu wote, ni Bajeti mkombozi na nadhani ni Bajeti yenye hisia ya ujasiri amani. Kwa hiyo, naomba niwapongeze kwa dhati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze pia wenzetu ambao wamechaguliwa kusimamia mapato ya nchi hii Ndugu yetu Kitilya kuwa Kamishna Mkuu na Ndugu Luoga kuwa msaidizi wake. Toka Jumatatu wamekuwa wakipongezwa si kwa sababu ya kupongezwa tu lakini kwa sababu kazi wanayosimamia ni kiini kikubwa cha Bajeti hii na ndiyo maana tunawapongeza kwa dhati kwa kuteuliwa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Waheshimiwa Wabunge wengi kuchangia kwa muda wa siku nne si kweli kwamba unaweza ukawa na jambo jipya kabisa, lakini ni vizuri tukakazia baadhi ya maeneo ambayo ni muhimu katika mpango huu na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuuelekeza kwenye Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji kwa kuangalia kile kipengele cha kukua kwa uchumi. Napenda niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imetuonyesha kwamba uchumi wetu umekua na kukua kwa uchumi ni hatua muhimu ya kupunguza umaskini kwa wananchi wetu.

Katika viashiria vya ukuaji wa uchumi tumeona dhahiri, ukichukua viashiria vichache kwa mfano, ukichukua ukuaji wa pato la Taifa kuanzia mwaka 2000 - 2003 na hii *projection* ya 2003/2004 ni dhahiri kwamba uchumi wetu unakwenda vizuri. Tumepata mafanikio, mwaka 2000 uchumi ulikua kwa kasi ya asilimia 4.9, lakini umeendelea kukua na tunadhania kwamba kwa *projection* hii mwaka 2004 uchumi utakuwa umekua kwa asilimia 6.3.

Lakini Mheshimiwa Spika, vile vile inakuwa *complimented* na mfumuko wa bei ambao kwa miaka hiyo hiyo umekuwa ukipungua. Mwaka 2000 mfumuko wa bei ulikuwa asilimia sita na umeendelea kupungua na mwelekeo wa 2004 ni kwamba mfumuko wa bei utakuwa kwa asilimia nne.

Haya ni maendeleo makubwa, kama ukuaji wa pato ungekuwa unakua peke yake na mfumuko wa bei ungekuwa unakwenda juu ni dhahiri kwamba uwezo wa wananchi kununua bidhaa ungepungua. Lakini kwa kuwa pato la Taifa linaongezeka na mfumuko wa bei unapungua ni dhahiri kwamba uwezo wa wananchi katika kununua bidhaa unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika viashirio vingine tumeona uwiano wa uwekezaji wa pato la Taifa, huu haukuongezeka sana japokuwa utakuwa umeongezeka kwa ukubwa wake, lakini ukiangalia kwa asilimia ni kwamba tumeendelea kuwekeza asilimia karibu kumi na saba kwa muda wa toka 2000 mpaka 2001 na hatujajua mwaka 2003 na 2004 tutawekeza kwa kiasi gani.

Kwa hiyo, ningeomba Waziri anayehusika alitazame hili na angalau atupe *projection* kwamba tunategemea katika mwaka 2003 kuwekeza kwa uwiano gani. Nadhani hilo ni jambo muhimu ambalo litaweza kutufanya tuweze kujipima katika uchumi wetu pindi bajeti hii itakapokuwa inasomwa tena mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwenda vizuri katika pato la Taifa, pamoja na mfumuko wa bei kupungua, bado tuna matatizo mawili makubwa. Riba za amana zimekuwa zikipungua. Kwa hiyo, hii imekuwa haishawishi sana watu kuweka akiba kwa wingi kwenye Benki zetu kwa sababu mwaka 2000 riba za amana zilikuwa asilimia 4.2, mwaka 2001 asilimia 3.5, mwaka 2002 asilimia 3.1. Kwa hiyo, inaonekana dhahiri kwamba, hii inazidi kupungua. Lakini ukiangalia riba za mkopo zimekuwa zikipungua

kwa wastani, mwaka 2000 ilikuwa asilimia 19.6, mwaka 2001 asilimia 16.4 na mwaka 2002 asilimia 15.7, ni dhahiri kwamba kuna uwiano wa kupungua riba. Lakini vilevile kuna uwiano wa kupungua riba za amana. Lakini ukitazama ule mfumko wa bei ukilinganisha na riba za amana na riba za mkopo ni dhahiri kwamba hatupati manufaa makubwa sana katika riba za amana. Kwa sababu ule uwiano wa kupungua katika riba za amana na katika mfumko wa bei zinaonekana kama zinashabihiana wakati hazipaswi kushabihiana.

Mheshimiwa Spika, sasa nitazame kidogo huu ukuaji wa Pato la Taifa, kama kigezo cha kuongezeka kwa uchumi ama kukua kwa hali ya uchumi hapa nchini imesaidia vipi. Nadhani kama tulivyosema kwamba, haionyeshi dhahiri au mara moja kama imemsaidia sana mwananchi kijijini. Lakini mwananchi anaweza kuona mabadiliko makubwa katika uwekezaji kwenye elimu, uwekezaji kwenye barabara na sasa tunazungumzia uwekezaji kwenye kilimo ambacho mwaka huu kimepewa kipaumbele kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita. Kwa hiyo, Serikali inatakiwa kufanya nini kusudi hali hii ya kuongezeka kwa pato iweze kwenda kwa mwananchi mmoja mmoja ili kaya iweze kujenga uwezo wa kujitegemea zaidi na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo na kwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya *GDP* inategemea kilimo, ni dhahiri kwamba kuwekeza zaidi kwenye kilimo kutasaidia sana kubadilisha hali za wananchi wetu vijijini. Kwa hiyo basi, ili tuweze kuwasaidia wananchi hao lazima tuweke mazingira mazuri. Serikali sasa lazima iweke mazingira mazuri ya uwekezaji kwa wananchi vijijini. Tukiangalia kuwa kilimo ndiyo muhimu sana ni dhahiri kwamba kama utafiti wetu utafanywa vizuri, kwa mfano, utafiti wa mbegu bora, tumeona tulipotembelea kwenye Kituo cha Utafiti kule Dar es Salaam kwamba, tayari kituo kile kina raslimali kubwa, kina watafiti wazuri na kimeanza kufanya utafiti wa uzalishaji mbegu kwa kupitia njia ya *vegetative propagation.* Kwa hiyo, kama njia hii itaimarishwa zaidi, ina maana tutaweza kupata mbegu bora kwa wingi kwa wakati mmoja kuliko tulivyokuwa tunafanya sasa. Kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali kuliangalia sana suala hili la uzalishaji wa mbegu kwa njia za kisasa ambapo unaweza ukapanua zaidi uzalishaji huu kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Vilevile nawapongeza kwa kazi hii nzuri ya kutoa ruzuku kwa mbolea ambayo inasaidia ku-*complement* suala hili la uzalishaji na kuimarisha kilimo. Lakini ningependa niseme kwamba, inawezekana pengine ni vizuri tukaiona ile Mikoa 4 ambayo imepata mchango huu wa ruzuku, ikaonekana kama ni Mikoa ya kuanzia kupata uzoefu ili iweze kuendelea na kwenye Mikoa mingine hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niingie suala la pili katika Wizara hii ambalo linahusu ubinafsishaji. Nawapongeza sana Serikali kwamba tumeona katika maelezo yao kwenye vitabu vyote viwili kwamba, hali ya uwekezaji wa Mashirika haya ambayo yamebinafsishwa hasa yale Mashirika makubwa makubwa ni nzuri sana. Katika Mashirika haya, mchango wa Mashirika haya makubwa umekuwa ni mara nne zaidi kwa Serikali ukilinganisha na mwaka 2001 na 2002. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa. Lakini yapo matatizo ya aina mbili katika ubinafsishaji wa Mashirika. Tatizo

la kwanza, ni matatizo ambayo yako kwenye Mashirika yaliyokuwa ya Umma. La pili, ni tatizo ambalo liko kwenye Mashirika au Makampuni ambayo ni ya binafsi bado na yalikuwa ya binafsi. Sasa katika Mashirika haya ambayo yamebinafsishwa hasa Mashirika ya Kilimo, Bodi hizi za mazao ambazo ndiyo tunadhani zinasimamia Mashirika hayo yaliyobinafsishwa, sheria inayounda Bodi hizi haina meno, haina uwezo wa kusimamia Mashirika haya yaliyobinafsishwa kikamilifu kama ilivyokuwa wakati yakiwa Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali itazame uwezekano wa kuhuisha sheria hizi zinazounda Bodi ili ziendane na wakati huu wa sasa wa ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili, ni Mashirika au Makampuni yale ambayo yalikuwa ni ya binafsi na yanaendelea kuwa ya binafsi lakini ni makampuni makubwa, kwa mfano, mashamba ya chai na baadhi ya mashamba ya mkonge. Mashamba haya hayana msimamizi maalum kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, waliyo na mashamba haya wanafanya wanavyotaka, hawalipi wafanyakazi mishahara inavyostahili, hawalipi mishahara ya kutosha na katika baadhi ya mashamba kwa mfano, mashamba ya chai kama kule kwenye Jimbo langu, Shamba la Dindira, Shamba la Balangai, Shamba la Ambangulu na kwenye mashamba ya mkonge, Shamba la Mabogo, Shamba la Kwalukonge na mengineyo, bado hayana usimamizi na wafanyakazi hawalipwi kama inavyostahili. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali itazame ni jinsi gani Wizara Mama za Mashirika haya au za mazao yanayoendelea kwenye makampuni haya wanaweza kusimamia zaidi Mashirika haya ili yawe ya manufaa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona jinsi usimamizi ulivyo mgumu katika mashamba ya mkonge, wale mliotembelea hivi karibuni, ile Kamati iliyotembelea mtakuwa mmeona dhahiri kwamba, mashamba mengi yamekufa, yapo mashamba machache sana unaweza ukayahesabu, Gomba ambalo ni la binafsi, mashamba ya Amboni ambayo yamenunuliwa, lakini mashamba yote hasa yale ya *Katani Limited,* kwa kweli yamekufa. Mashamba yote isipokuwa mawili yamefungwa. Miundombinu karibu yote imetoweka. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, usimamizi unahitajika zaidi na ningeomba Serikali isilifumbie macho suala hili hasa la *Katani Limited* ambapo miundombinu kwenye mashamba mengi imekwishatoweka, lakini bado tunafikiria *rearbitration*. Kwa hiyo, nadhani siyo wakati wa *arbitration* sasa ni wakati wa kuchukua hatua inayostahili.

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie kwa Wizara ya Fedha, kwa kuangalia mambo mawili tu. Kwanza niwapongeze kwa kutoa zile kodi ambazo ni kero kwa wananchi. Lakini kuondoa kodi hizi iwe ni changamoto kwa wananchi wetu kufanya kazi zaidi ili tuweze kupata manufaa na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

La pili, ni tatizo la kodi ya ardhi, naipongeza Serikali kwamba imepunguza kodi ya ardhi kutoka Sh. 600/= mpaka Sh. 200/= kwa eka. Lakini naomba niwaombe kwamba katika mashamba makubwa kwa mfano, mashamba ya chai, ambayo hayalimwi eneo lote miaka yote lazima wabakishe eneo kubwa la msitu wa asili naomba kodi ile kwenye sehemu hiyo iondolewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hizi mbili zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nami niungane na wachangiaji walionitangulia, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wameingia Bungeni hivi karibuni na kuwaambia kwamba, tushirikiane katika kusukumu gurudumu la maendeleo ya nchi yetu kwa pamoja. *(Makofi)*

Pili, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kutokana na kazi nzuri na ya mafanikio walioifanya ambapo asilimia kubwa ya wachangiaji wameipongeza kazi yao. Kwa hiyo, hii ni ishara ya kwamba kazi iliyofanyika ni nzuri na inastahili pongezi. Hivyo, pongezi hizi pia ziende kwa watendaji wote ambao wameshiriki katika kufanikisha kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende moja kwa moja katika maeneo ambayo nilihisi pengine ningelizungumza mawili, matatu na nadhani pengine yanaweza kusaidia katika kuiboresha bajeti hii. Ningeanza na eneo la kilimo. Juhudi za Serikali zimeonekana na nia njema katika kukikuza kilimo hasa pale Serikali ilipoamua kuchukua eneo dogo katika nchi yetu kwa kuchagua Mikoa fulani hivi, itumike kama ni sehemu ya kuanzia. Huo ni mwelekeo wa matumaini na ni imani yangu kwamba, kutoka hapo itakuwa ni kuendelea na maeneo mengine katika kuyaongezea nguvu ili kuongeza huo ufanisi uliokusudiwa.

Lakini vilevile ni vyema katika kuboresha hali hii, Serikali ikawa na mtazamo mwingine wa nyongeza katika eneo lingine ambalo naamini bado nchi yetu haijalitumia hata kwa asilimia 5 katika uchumi nalo ni eneo la uvuvi. Upande wa uvuvi wa kwenye maziwa nimeangalia kitabu cha hali ya uchumi wa Taifa imetaja tu. Kwa upande wa maziwa imeonyesha uvuvi ule wa Sangara, lakini upande wa baharini wametajwa pweza, ngisi na kamba. Lakini sasa Sangara ni jamii ya papa, sasa baharini hawa wako wengi sana tena wa aina nyingi na bahati nzuri nchi yetu ina eneo kubwa sana la bahari. Kuna eneo ambapo liko wazi mpaka unafikia maeneo ya huku *Far East*, hapo pako wazi kabisa. Cha kushangaza zaidi ni kwamba, tunatoa leseni sasa waje watu kutoka nje kuvua ndani ya eneo letu, kana kwamba sisi wenyewe tumekinai wakati bado tunayo shida kubwa sana na zaidi ya hayo, hao wanaovua wanaondoka na samaki kama walivyo wanakwenda nao nje hawawi-*processed* hapa nchini kwetu. Kwa hiyo, kama ingelikuwa wanakuwa *processed* hapa kwetu ina maana pia ingelisaidia kukuza ajira kwa watu wetu. Kwa hiyo, hilo nalo pia ni tatizo. Sasa ile ni malighafi ya bahari, inaondoka vilevile kama ambavyo inaondoka dhahabu, pamoja na madini mengine yanavyoondoka na hawa samaki ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, hii ni kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vyema nayo tukaipangia utaratibu unaoeleweka na wa kuendelea vipi itaweza kutumika. Ninaamini eneo hilo lina uwezo wa kuziba lile pengo la asilimia 45 la msaada kutoka nje katika kuziba pengo la bajeti, kwa sababu

bahari inao uwezo wa kuziba pengo hili. Kwa hiyo, nadhani tungefikiria kuona umuhimu wa kuitumia bahati hii tuliyojaliwa kuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende eneo lingine kuhusu masuala ya kodi. Wenzangu wote waliotangulia wametoa pongezi nyingi sana na kumtakia kazi njema mtendaji mpya, ambaye jina lake nimelisahau.

MBUNGE FULANI: Bwana Kitilya.

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Ndiyo huyo huyo. Sasa kwa kuwa ni mpya na mimi sina budi kumpongeza na kumtakia kazi njema. Lakini pongezi zangu nazitoa kwake zikiwa ni deni. Deni ninalolizungumza liko katika hali ifuatayo:- *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maeneo ambayo yameandikwa ndani ya vitabu vyetu hivi, pamoja na hiki cha Benki Kuu ya Tanzania, hili eneo la Bandari ya Zanzibar linachangia sehemu ya haya mapato. Lakini kitabu hiki cha Benki Kuu katika ukurasa wa 14 naomba ninukuu kinasema: *"Tax on imports however decline by eleven point four percent from Tanzania shillings, four point nine billion recorded during the corresponding quarter in 2001/2002 to Tanzania shillings four point three billion due to the general decline in import through the Zanzibar Port"*. Hii ni 2001/2002, sasa hii *decline* imeendelea 2002/2003, kiasi ambacho ile bandari sasa hivi unaweza hata ukacheza mpira, hakuna kitu ni nyeupe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa masuala ya kodi yamekuwa na *contribution* yake na wengi wamelalamika na hili suala bado linaendelea kulalamikiwa. Sasa deni ninalompa yule bwana tuliyemtaja pale mwanzoni, afanye *study* hapa aone nini tatizo. Kwa sababu tatizo hili limeshasababisha ukosefu wa ajira ya maelfu ya watu ambao walikuwa wakitegemea mapato yao na kuendesha maisha yao kupitia bandarini. Kwa hiyo, leo nampongeza lakini mwakani tukijaliwa, hali hii ikiwepo nitakuja na shutuma nzito na mimi hili nitalifuatilia na nitamshutumu kwa kumtaja na jina hasa. Kwa hiyo, kwa leo nampongeza sana na nakutakia kila kheri katika dhamana yako hii mpya na Mungu atakusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la mawasiliano. Katika eneo la mawasiliano kumeongezwa hizi gharama za muda wa mawasiliano katika hizi simu za mkononi *(airtime),* kutoka asilimia 5 mpaka asilimia 7. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha pia akatuambia kwamba katika nchi nyingine za *East Africa* wao wako mpaka asilimia 10. Sasa kwa bahati mbaya sana amelinganisha pamoja tu, yapo maeneo mengi ambayo wenzangu wapo chini zaidi ukitulinganisha na sisi. Lakini kachukua hapa hapa tu kwenye hizi *airtime* basi, hakwenda maeneo mengine. Lakini sasa bahati nzuri tuliyonayo Tanzania hii, sina hakika kama na wenzetu wanayo, haya maeneo hizi *gate way,* tunao uwanja mpana sana, lakini bado hatujautumia.

Nimejaribu kuangalia nadhani kitabu hiki cha hali ya uchumi, kuna maeneo mengi sana ambapo mwaka 2002, nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na

Uchukuzi, alikiri kwamba kuna eneo kubwa sana la mawasiliano kupitia *ZANTEL* ambalo bado halijatumika. Sasa hapa inaonekana mpaka mwaka 2002 idadi ya wateja wa Kampuni ya *ZANTEL* walikuwa wateja 35,000 tu, wakati ambapo *gate way* yao hii ni kubwa kuliko ile ya *TTCL*, sasa hilo ni tatizo. Nadhani kwa kuwa hawa wame-*invest* ndani ya nchi zetu, hakuna sababu kwa nini tusinufaike nazo. Kwa hiyo, hili nadhani watakapopanua ule wigo wao wa mawasiliano na nafasi ya kodi itaongezeka na matokeo yake itakuwa ni manufaa kwa nchi yetu. Kwa hiyo na hilo nadhani lilikuwa na haja tulione na tulitumie kikamilifu kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuangalie baadhi ya vifaa vingine ambavyo navyo vimeongezewa hizi gharama za kodi. Naangalia kuna hii dawa ya mbu ya kuchoma lakini nadhani si dawa ya mbu, hii ni sumu ya mbu. Dawa hutoa nafuu, sumu inaua, lengo ni kuua mbu. Sasa kutoka asilimia 10 imepandishwa mpaka asilimia 15, vyandarua kutoka asilimia 0 mpaka asilimia 10, pengine Mheshimiwa Waziri alikuwa ana nia njema kabisa ya kuvisaidia viwanda vyetu vya ndani, lakini hakutoa maelezo hayo. Sasa ni vizuri katika vitu kama hivyo vinavyowagusa watu wengi sana ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia suala hilo, lakini tatizo limekuja hapo hatukuelewa sasa nia yake nini, kuongeza tatizo au kupunguza tatizo. Sasa iwapo uzalishaji ndani ya nchi yetu kwa hizo dawa za mbu na vyandarua uko juu sana kiasi ambacho hatuna ulazima wa kupata ongezeko kubwa kutoka nje, nia yake itakuwa ni njema. Lakini iwapo hatujitoshelezi kwa hivyo vinavyotoka nje tunaongeza kodi, ina maana hilo litakuwa tatizo. Kwa hiyo, mjadala hapa umekuja kwa misingi hiyo. Kwa hiyo, ni vyema hizo siku zijazo hili tuliweke wazi ili hii isitupotezee muda mwingi sana kimazungumzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu katika kipengele hicho hicho ukurasa wa 55 kuna vifaa maalum vya mawasiliano kwa njia ya redio, hili nadhani alikusudia hizi tunazoziita *radio call*. Lakini vilevile pamoja na hayo bado kuna haja sasa hivi kama ambavyo Serikali iliangalia umuhimu wa kompyuta tukapunguza kodi, sasa hivi nchi yetu twende hatua nyingine, sasa Serikali iwe na mtazamo vilevile wa kupunguza kodi kwenye hizi redio za kawaida, ambazo kila mwananchi anahitaji kujua matukio ya kila siku. Kwa hiyo, ni vyema tukapaangalia na hapo. Televisheni zamani ilikuwa anasa, lakini sasa hivi hatuko hapo, sasa hivi ni chombo cha lazima, ni chombo muhimu kwa kila mtu kuwa nacho. Sasa nayo pia tuangalie nafasi ya kupunguziwa kodi ili wananchi wengi wamudu kuwa na televisheni, kwa sababu hiki ni chombo muhimu, zamani ndiyo kilikuwa cha anasa. Lakini dunia mahali ilipofikia televisheni tuiite labda sasa hivi ni chombo cha lazima kumudu kununua na kutomudu kununua ni suala lingine. Lakini sasa tupunguze kodi ili hawa Watanzania walio wengi wamudu kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi la ubinafsishaji limechukua nafasi kubwa sana na linaendelea. Lakini vitu ambavyo tunajaribu kujifunza vingine vina matatizo mengi sana. Mfano, *TTCL, TANESCO,* kumekuwa na malalamiko. Kwa hiyo, nadhani Serikali itupatie tathmini. *TTCL* toka imebinafsishwa wale waliopewa wameongeza nini zaidi ya vile ambavyo wamepewa? Teknolojia imeongezeka kwa kiwango gani, uwezo wa mawasiliano umeongezeka kwa kiwango gani? *TANESCO* muda ambao tulikuwepo pale Dar es Salaam tumeona kila wakati umeme ukikatika, sasa hili ni miongoni mwa jipya

walilokuja nalo au kuna lingine la ziada? Kwa hiyo, ni vyema tungelipatiwa tathmini ili Watanzania wakajua na ndipo pale watakapoona umuhimu wa kubinafsisha. Nadhani vinginevyo ndilo hili tatizo sasa watu wanahofia *NMB* itakuwaje. Sasa tuki-*experience* matatizo tu ndipo tunapokuwa waoga kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja zote mbili. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. EMMANUEL E. KIPOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia muda huu jioni hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli unapozungumza katika dakika za mwisho ambazo wachangiaji wengi wamekwishazungumza, inakupa tabu sana kukwepa kukiuka Kanuni ya 49(10) inayozuia kurudiarudia maneno yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Ukitaka ukwepe sana unaweza ukasababisha mambo yaliyotokea hapa asubuhi. Leo nimejifunza sana asubuhi kwamba, hizi *microphone* za Bunge lako Tukufu, zinapenda sana kuhudumia mambo mazito mazito. Kwa kweli zinashindwa kabisa kuhudumia mambo mepesi mepesi. *M*imi nilichojifunza nimeona kama Waheshimiwa Wabunge saba au watano tukizungumza nyepesi nyepesi utaahirisha Bunge lako kwa siku tano. *(Makofi)*

Ninaomba Mwenyezi Mungu, anisaidie nisikiuke Kanuni ya 49(10). Nianze kwa kuwapongeza watoa hoja wote wawili, kwa kweli hotuba zao zimekuwa nzuri, kuna maeneo machache ambayo ningependa niyazungumzie kama mawili hivi na muda ukiniruhusu nitazungumzia na jambo lingine la tatu. Ninavyoiangalia nchi yetu hasa katika utumishi wa umma, kwa maana ya wafanyakazi wa Serikali, mimi naona kuna mgomo. Idara zote za Serikali zina mgomo wa kufanya kazi. Manesi wako kwenye mgomo wa kudumu, Walimu wako kwenye mgomo wa kudumu, Madaktari wako kwenye mgomo, sijui kama ninaeleweka ninachosema, kwa sababu tunaona wanavyofanya kazi? Lakini kwa kweli kazi wanazofanya sidhani kama zinafikia kile kiwango cha juu cha uwezo wao wa kutenda kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na hii mimi nimejaribu kufikiria kama *nurse* alikwenda kusomea u-*nurse*, wengi wao hawakulazimishwa kwenda kusomea u-*nurse,* wamekwenda kwa mapenzi yao, mimi napenda niwe *nurse,* lakini amekwenda kazini sijui kwa nini amepoteza ile *interest* iliyomsukuma yeye kwenda kufanya kazi ya u-*nurse*. Vilevile hata walimu walikwenda kusomea ualimu kwa mapenzi kabisa kwamba mimi nataka niwe mwalimu wa shule ya sekondari, wa shule ya msingi, lakini amefika kule kwenye kazi yake sijui kimetokea kitu gani ameamua kugoma kufanya hiyo kazi! Kaka yangu Mheshimiwa Leonard Derefa, juzi alisema kwamba, Shinyanga tunakuwa wa mwisho katika matokeo ya darasa la saba na darasa la nne Kitaifa, akasema labda tuna upungufu wa walimu, mimi nafikiri kuna lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilivyotazama na kufikiria kuna mambo kwa kweli makubwa ya kibajeti ambayo yanahitaji kufanyika ili wafanyakazi wetu waweze kufanya

kazi vizuri. Lakini pia kuna mambo mengine makubwa ambayo hayahitaji bajeti yanayohitaji kufanyika ili wafanyakazi wetu waweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya mishahara, mishahara kwa kweli ni midogo, sitaki kulizungumzia hili, kwa sababu kila siku hali ya uchumi wetu tunaielewa, tunategemea misaada, bajeti yetu inategemea misaada asilimia 45, naelewa na sitaki kulisemea hili ni la kibajeti na ninatumaini kila Mtanzania anaelewa hali yetu tuko wapi. Hatuwezi kusema sasa tutalipa malaki wakati hatuna, hilo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kuzungumzia ni mambo tu ya kiutaratibu ambayo yatawapa motisha wafanyakazi kufanya kazi. Nataka nizungumzie suala la pensheni. Mfanyakazi anaajiriwa, anatumikia Taifa kwa miaka 25 au 30 anapostaafu hivi kuna mgogoro gani asipewe pensheni yake mara moja. Suala la udogo wa pensheni kwa kiasi kama cha shilingi 20,000/= nampongeza Mheshimiwa Waziri amepandisha, hili la uchache au udogo wa pensheni yenyewe ni suala la kibajeti sitaki kulizungumzia. Lakini hili suala la utaratibu wa wastaafu kulipwa kwa wakati hivi lina mgogoro gani? Halihitaji Bajeti linahitaji kupanga vizuri. Hivi kweli huko Serikalini hatujui kwamba mwaka huu 2003 au 2004 tuna wafanyakazi wangapi ambao watastaafu, hivi kweli hatujui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliambiwa hata watu wa Treni wanaweza sasa mabogi yao yanaposafiri kwenye reli wanaweza kutokea Dar es Salaam wakajua kwamba hili bogi letu sasa hivi linafika Godegode. Sijui kama niliambiwa habari za kweli, hayo ni mambo ya teknolojia nafikiri linawezekana. Wanaweza wakaangalia kwamba behewa letu sasa lina mzigo fulani limefika wapi kule, Mlimba, wanaweza wakaangalia. Hivi Serikali haiwezi ikaangalia kwamba Mwalimu wetu fulani yuko Mtwara atastaafu mwaka kesho tuandae mafao yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilikuwa Dar es Salaam limetokea jambo la kusikitisha ni la kusikitisha kweli kweli, naomba niliseme hapa kwa huzuni. Kuna Mwalimu mmoja amestaafu kazi mwaka 2001 akitokea huko Lindi, amekaa huko Lindi anasubiri mafao yake ya pensheni hakuna majibu. Ameamua kusafiri kwenda Dar es Salaam maskini wa Mungu mzee huyu miaka mitatu iliyopita amestaafu, kwa vyovyote hana hela hata ya kula. Yule mzee alifariki katika stendi ya Ubungo na Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo ambayo kwa walimu wenzake wanayaangalia, hivi wanafanya kazi kwa maslahi ya nani? Kama Taifa watakapomaliza kulitumikia linawasahau kiasi hicho, unawategemea walimu hawa wafanye kazi, hata ningekuwa mimi ningekuwa na mgomo. Tunaona walimu wanakwenda darasani wanafuma vitambaa ili angalau wajiongezee kipato kwa sababu hawana matumaini katika *future* yao kule mbele. Licha ya udogo wa pensheni, ule usumbufu mkubwa wa kuipata hiyo pensheni. Ninapendekeza Serikali ifanye marekebisho ya haraka katika suala zima la utaratibu wa kulipa pensheni watu wanaostaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningekuwa mimi nimepewa madaraka hayo kwa kweli nasikitika kusema kwamba, ningeya-*misuse* kwa kuwaondoa wote wanaoshughulikia jambo hilo na kuunda Kitengo kipya cha kushughulikia jambo hilo. Kutoka ngazi ya kijijini anakofanyia kazi mtu kama kipo *anyway* mpaka ngazi ya mwisho huko wanakolipiwa. Hivi kuna ugumu gani jamani kompyuta zipo na kila kitu kipo, kwa nini yanatokea mambo haya?

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu kilimo. Bajeti hii nzuri kama tulivyosema wote na mimi nasema ni nzuri na pengine nisiishiwe muda huko pembeni niseme kwamba naiunga mkono hoja kwa asilimia mia. Suala la kilimo ni jambo ambalo kwa kweli limekuwa linapewa kipaumbele kila tunapoketi hapa. Mwaka 2002 kuna rafiki yangu mmoja baada ya kusikia hiyo Bajeti ambayo tuliibatiza kuwa ni Bajeti ya Kilimo, alizungumza hapa sipendi kumtaja *actually* alikuwa *over-excited*. Akasema kabisa Wabunge wote lazima twende Majimboni kwetu tukatekeleze Bajeti hii. Mimi nilitoka nikaenda Jimboni kwangu nimekaa kijijini nimeanza kulima, lakini nasikitika kusema kwamba, pamoja na Bajeti hiyo nzuri ya mwaka 2002 au mwaka huu unaoisha kesho kutwa, sijaona badiliko lolote kwa mkulima wa kule kijijini kwangu mwaka2002. Alivyokuwa akilima mwaka 2001 na mwaka 2000 ni vile vile na ni mbaya zaidi pengine kwa sababu mwaka huu wa 2003 kule kwetu mazao yote yameungua na jua. Fedha zile zingekwenda pengine zingetengeneza hata vidimbwi vya kumwagilia maji pengine tusingeathirika kama tulivyoathirika mwaka huu. Sasa fedha hizi zimeishia wapi tulizozipitisha mwaka 2001? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Mramba, anakubaliana na mimi katika hotuba yake ukurasa wa 40. Sasa anakubali kwamba, fedha hizi zitaondoka kule kwake ziende moja kwa moja kwa Maafisa Kilimo wa Wilaya, hii ni kukubaliana na mimi kwamba, fedha za mwaka 2001 hazikufika kule. Mimi katika Jimbo langu kule nasema kwamba hazikufika, sikuona mabadiliko. Sasa mwaka huu tena nashangilia sijui nikakae tena nisione mabadiliko na kwa kweli tunasifia lakini nafikiri kuna mambo ambayo yanahitaji kufanyika. Tunapanga vizuri lakini hatutekelezi kama tunavyopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mramba au Serikali imekubali kupeleka fedha hizi kwa Maafisa Kilimo wa Wilaya. Mimi nina wasi wasi kwamba, tuko pale pale. Hawa Maafisa Kilimo wa Wilaya ambao kila siku Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa anajitahidi na nampongeza kuwa kila anapofanya ziara, hasiti kuwaambia waende mashambani wakashirikiane na wakulima, wako mijini. Leo tunawapelekea fedha mimi sijui kama kuna maandalizi yamefanywa kwenye hizo Idara za Kilimo huko Wilayani. Zinapelekwa hizi fedha kule kwa Maafisa Kilimo wa Wilaya pengine zikakae tu au zifanye nini, sijajua kabisa kuna utaratibu gani uliopangwa pale, inasemekana zitafanyia mazao mawili la biashara moja na la chakula moja. Maandalizi mimi nadhani bado. Hatuna Mabwana Shamba, hatuna Mabibi Shamba, sijui kama wapo, mimi kule Jimboni kwangu jamani nasikitika huwa siwaoni. Siwaoni sijui kama wenzangu mnawaona naomba mnigawie kidogo, lakini kwangu siwaoni. Sasa huyu Afisa Kilimo wa Wilaya anazitumiaje hizi fedha.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hapo kuna jambo la kuangalia na kunahitajika jambo lifanyike ili kunusuru tena hali ambayo itakuwa hivyo. Kwa sababu zinaweza zikaenda fedha pale Wilayani tukakaa kule vijijini, tunaokaa vijijini tunasubiri fedha zije sijui zinakuja kwa aina ya mkopo au zinakuja kwa njia gani tukakaa huko tusione. *At the end of the day* tutakuja mwaka kesho, itakuja Bajeti nyingine tunasema ni Bajeti ya Kilimo. Bahati mbaya kuna maneno lazima tuache kuyasema sasa. Kila siku tukija hapa tunaambizana kilimo sasa tunakubaliana ni sekta mama, ni sifa nyingi ambazo kwa kweli tulianza kuzisikia zamani mno na wengine bado tukiwa mashuleni. Sasa mpaka leo bado hatujajua umuhimu wa kilimo, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya kilimo nafikiri hapo nataka nizungumzie hotuba ya Mheshimiwa Kigoda kwa uchache. Katika ukurasa wa 32 wa hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Kigoda, amezungumzia kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo na mimi nafurahi sana kwa sababu ninakotoka kwenye Jimbo langu nawawakilisha karibu asilimia 95 ni wakulima wadogo wadogo. Sasa amesema kunahitajika wadau mbalimbali wafanye mambo ili sekta hii iweze kupata mapinduzi. Mimi ninavyodhani na sio lazima iwe sahihi, lakini ninavyodhani, kuna wadau wawili tu katika sekta ya kilimo, Serikali na wakulima wenyewe. Kwa upande wa wakulima kwa kweli naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza wanavyojitahidi kufanya kazi katika mazingira magumu, wanavyojitahidi kuzalisha bila kujua watauza kwa shilingi ngapi, wanavyojitahidi kuzalisha bila kujua hayo mazao yao yatalindwa vipi. Kwa upande wa Serikali kuna mambo mengi yanahitaji kufanyika. Nasikitika kusema kwamba, kama mdau, Serikali imesema kazi yake itakuwa ni kuvutia wawekezaji, nafikiri hatuna haja sana ya kuvutia wawekezaji nafikiri kubwa zaidi la kwanza liwe ni kuwawezesha wakulima wetu wadogo wadogo na kuwa na uwezo wa kuzalisha kulisha Taifa hili. *(Makofi)*

Kwa upande wa Serikali tunategemea ilete pembejeo. Naipongeza kwa mikoa minne iliyofanya utaratibu angalau wa *subsidy,* tunaipongeza lakini nashauri ingekuwa kwa nchi nzima. Utafiti haufanyiki ndio kazi za Serikali hizi. Sasa sioni mdau mwingine. Mambo ya mawasiliano kwa wakulima ni hafifu, mambo ya masoko ndiyo balaa tupu. Mtu anaweza kuzalisha eka moja ya pamba akapata kilo zake hizo chache kwa sababu hana ujuzi, hana huduma yoyote ya ugani ambayo ni mambo ya Serikali, mwisho wa siku anazalisha kwa gharama ya shilingi 500/= anauza kwa gharama ya shilingi 200/=. Nafikiri wadau wawili hawa, Serikali bado yuko nyuma. Kwa kweli Serikali inahitaji sasa iyavalie njuga majukumu ambayo yako kwake. Iwape mikopo wakulima, pembejeo ziwafikie na sio kuwafikia, ziwafikie kwa wakati. Utafiti ufanyike, mawasiliano yafanyike, masoko yatafutwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha na ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Kabla sijasema yale niliyotaka kusema ninaomba niseme mwanzo kabisa kwamba, naunga mkono hoja zote mbili. Ni hoja nzuri na zenye kuleta matumaini makubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie katika hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Naomba nijielekeze katika eneo la urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, ibara ya 68 mpaka 70 katika kitabu chake cha hotuba. Ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba, mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao wanakubaliana mia kwa mia juu ya sera ya chama chetu ya kurekebisha na kubinafsisha Mashirika ya Umma. Lakini mimi najenga hoja kwamba, ziko njia mbalimbali za kubinafsisha, haiko njia moja tu ya kuelekea ubinafsishaji, hii ndiyo hoja yangu na nafikiri ndiyo hoja ya Wabunge wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu mbinu yoyote itakayotumika kubinafsisha Mashirika yetu ingejengwa katika misingi miwili na naomba niitaje. Msingi wa kwanza ushiriki wa umma kwa kutumia raslimali zao wenyewe. Msingi wa pili, ni maslahi ya umma na Taifa la Tanzania kuweka kando maslahi binafsi na kuweka mbele uzalendo. Mafanikio ya ubinafsishaji yatapimwa kutokana na jinsi gani tumetekeleza misingi hiyo miwili. Ibara ya 68 Mheshimiwa Waziri, anatoa taarifa ya ubinafsishaji anasema hadi Machi, 2003, Mashirika 266 yamebinafsishwa, 134 yamenunuliwa na Watanzania, 16 wawekezaji wa nje, 116 ubia kati ya wawekezaji wa nje na wa ndani.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi haziwezi kuonyesha ukweli kwa sababu ambazo nitazisema. Takwimu hizi zingekuwa na maana tu kama zingeonyesha thamani ya Mashirika yaliyonunuliwa. Idadi ya Mashirika inaweza ikawa kubwa, lakini thamani yake na nafasi yake katika uchumi wa Taifa ikawa ndogo sana. Watanzania wangependa kufahamu hili idadi peke yake haitoshi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ukilitazama juu juu nalo unaweza usipate ukweli nalo linahusu ubia kati ya wawekezaji wa nje na wa ndani. Uchambuzi wa kina ukifanywa utaonyesha kuwa ubia huu ni ubia bandia, ubia wa jina, ubia wa kutimiza masharti, ubia uchwara. Ndani ya ubia huu mwenye kauli, mwenye uwezo wa mwisho ni mwekezaji wa nje. Kwa hiyo, mwekezaji wa nje siku zote na mimi nataka nipigie mstari siku zote atajenga mazingira ya kumnunua mwekezaji wa ndani na mifano tunayo, samaki mkubwa kummeza samaki mdogo ni sayansi. Kwa hiyo, idadi ya Mashirika 16 yaliyopata wawekezaji wa nje bado inaweza ikawa si sahihi kwa sababu hata yale ya ubia yana sura ya uwekezaji wa nje. Kwa hiyo, unaweza ukafanya hesabu tu wakajumlisha yakawa ni ya nje.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa tatizo la kutumia takwimu za *PSRC*. Takwimu ambazo zinataka kuonyesha kwamba, *PSRC* imefanya kazi nzuri kwamba, wananchi wameshirikishwa katika zoezi hili. Lakini nasema si kweli. Lakini liko jambo lingine ambalo *PSRC* inataka kufanya na nataka niliseme hapa, inakusudia kufanya tathmini ya zoezi la ubinafsishaji. *PSRC* imetangaza kwenye magazeti na ninayo nakala ya gazeti kama Waziri hakulisoma anaweza akasoma hili hapa *Business Times* la tarehe 23 Mei, 2003. Linasema kwamba: "*PSRC* inahitaji watu au Makampuni ambayo yatafanya tathmini ya zoezi hili la ubinafsishaji kama ilivyotekelezwa na *PSRC*. Wanaohitaji kufanya kazi hiyo wajiandikishe na wachukue vitabu vya zabuni kutoka *PSRC* na wavirejeshe *PSRC*". Tangazo linasema hivyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama Wizara inataka kufanya tathmini kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba Serikali inapata tathmini, utaratibu huo uliotangazwa una kasoro na unaweza usitupe ukweli wa tathmini yenyewe. Tarehe 30 Mei, 2003, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, alitoa taarifa kwa umma. Taarifa ya umma hii hapa kwamba, zoezi la tathmini linafanywa na Wizara na sio *PSRC*. Kama huu si ubabaishaji basi ni kujikanyaga. Nasema zoezi la tathmini ni la Wizara, basi Wizara yenyewe ingetoa tenda si tunazo zile zabuni za Wizara. Wizara yenyewe ingetoa zabuni, watu wakachukue vitabu Wizarani, warudishe Wizarani ndio utaratibu wa Kiserikali. Lakini masanduku ya *PSRC* eti kazi ya Wizara, hiki ni kiini macho Mheshimiwa Spika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia dondoo mojawapo hapa dondoo ya (b) katika tangazo hili inasema kwamba, watakaofanya kazi hii waonyeshe kazi za ubinafsishaji zilizobaki na wakadirie muda kiasi gani unahitajika kuzimaliza. Ni wazi kutokana na dondoo hii *PSRC* ingependa kuendelea kuwepo inajijengea uhalali. Kwa maoni yangu hakuna tena suala la kubinafsisha na kwa kweli *PSRC* pengine yenyewe sasa inahitaji kubinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama bado Mashirika machache yanatakiwa yabinafsishwe basi yarejeshwe Wizarani kama ilivyokuwa *Kilimanjaro Hotel.* Yarejeshwe Wizarani kazi ya kumalizia imalizike huko na tumeona imefanikiwa kwa *Kilimanjaro Hotel.* Lakini vile vile nashauri Wizara yenyewe ndiyo isimamie tathmini ya zoezi hili. Taarifa iletwe Bungeni kwa kupitia Kamati zake na hilo ndio ombi letu. Naomba kutoa hoja hii Wizara isimamie zoezi la tathmini na taarifa iletwe Bungeni kwa kupitia Kamati zake inaweza kuanza kwenye Kamati.

Nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Mramba, kwa kumteua Mama Blandina Nyoni, kuwa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Mama Blandina atashangaa Mwalimu wake asiposema lolote basi itakuwa kuna upungufu. Mimi nimekuwa Profesa wa Mama Blandina, ninamfahamu Mama Blandina, ni mama mwenye juhudi, mama mwenye upeo mkubwa, ni hodari wa kazi, kwa hiyo, nafasi aliyopewa anastahili kupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nategemea Mheshimiwa Waziri, atatoa maelezo lakini kama nilivyosema mwanzo sina ugomvi wa msingi katika hoja hizi mbili naziunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kabla ya yote naomba kuchukua nafasi hii ya kipekee kabisa kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, Viongozi wa Chama na Serikali Mkoa wa Arusha, Mwanza, Serengeti na kwingineko nchini. Wananchi wote wa Arumeru Mashariki na Arumeru Magharibi, Arusha na kwingineko. Ndugu na marafiki walioshiriki na kutufariji katika majonzi yaliyotupata kwa ajili ya kifo cha aliyekuwa mke wangu mpenzi, Ekaeli Mbise, aliyenitoka kwa ajali ya gari tarehe 6 Aprili, 2003. Naomba niwataje kwa kipekee Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Wakuu wa Mikoa ya Arusha, Bw. Babu na Mwanza Ndugu Ole Njoolay na ndugu zangu

wengine wote. Mungu ailaze mahali pema roho ya aliyekuwa mpenzi mke wangu, Ekaeli. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili, kwa kazi yao nzuri ya hotuba hizi mbili za Bajeti ambazo zimetolewa kwa umahiri wa hali ya juu na zimekidhi mahitaji ya Watanzania wengi kiuchumi, kimaendeleo, kijamii na hata kisiasa. Naomba pia niwapongeze Ndugu Kitilya na Ndugu Luoga, kwa kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais, kuiongoza *TRA* na kuiendeleza kazi ambayo imeachwa kwenye ufanisi mzuri, ulioachwa na Ndugu Sanare na labda niseme kwamba, Sanare yeye alichofanya ni kutuwekea *benchmark* na *threshold* ya *performance* na anachomwachia Kitilya na mwenzake ni changamoto na hiyo changamoto ni kufikia makusanyo ya shilingi bilioni 200,000 kwa mwezi na nadhani huo uwezo uchumi wetu unao. Pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, ambao walichaguliwa kipindi cha mwezi uliopita. Nawapa hongera sana na karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika Bajeti moja kwa moja. Naungana na wenzangu kwamba, Bajeti ni nzuri lakini kuna maeneo ambayo ningependa nipate ufafanuzi na majibu ambayo hayana chenga. Nina maeneo mawili ambayo ningependa niungane na mwenzangu Mheshimiwa Mrope kwamba, nami nisipopata majibu ya kutosha nitakuwa na wasi wasi na huenda nikatoa shilingi. Hili moja linahusu suala la Mradi wa Maji Mji wa Arusha. Linahusu *Management* ya *Counterparts,* nakumbuka hilo suala limezungumziwa kwa kiasi kikubwa wakati tukiwa kwenye Kamati na tukapata taarifa kwamba, suala la ku-*manage Counterpart Funds* ambazo zilikuwa zinakwamisha utekelezaji wa miradi ya wafadhili kwa kiasi kikubwa lilikuwa limetatuliwa. Tulikubali na hatukuwa na sababu ya kukataa kwamba sio tatizo tena.

Mheshimiwa Spika, lakini taarifa nilizonazo ni kwamba, Mradi wa Maji wa Mji wa Arusha umekwama kwa ajili ya ukosefu wa *Counterpart Funds* kutekeleza huo mradi. Mji wa Arusha ulipata mfadhili ambaye alikuwa tayari na ameshatoa fedha na tayari mradi ulikuwa uko tayari kuanza kutekelezwa, vifaa viko vimelala, mitambo iko tayari imekaa imepumzishwa hapo, lakini *Counterpart Funds* ndizo zinangojewa mradi utekelezwe. Tayari Mji wa Arusha ulikuwa unasubiri kunywa maji ya huo mradi. Bahati mbaya mpaka sasa bado huo mradi hauja-*take off.* Wageni wetu wa Kimataifa walioko kwenye hiyo *Geneva of Africa,* kama unavyosifiwa, tayari wanaanza kuwa na wasi wasi kuhusu *status* ya miundombinu ya Mji wa Arusha. Miundombinu ya Mji wa Arusha iko kwenye hali ambayo si nzuri na si ya kuridhisha. Mradi huo wa Maji ulikuwa unataka kuchangia kuongeza hali ya miundombinu ya Mji wa Arusha, lakini tunakwamishwa. Mheshimiwa Waziri, tunaomba tupate jibu la huu mradi kwamba ni vipi hizo *Counterparts* zinaweza kupatikana na tupate uhakika kama mradi huo utatekelezwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu Soko la Tengeru. Soko hili liko kwenye Jimbo langu la Arumeru Mashariki na ni kilomita karibu 12 kutoka Mji wa Arusha kuelekea Moshi. Wengi wanaokwenda Arusha wanalifahamu, limebanana nimekuwa nikilipigia kelele hapa karibu kila wakati ninapopata fursa ya kuchangia kwenye Bunge hili. Nilipata ahadi mwaka 2002 kwamba, tungepata mradi si tu wa kulijenga hilo soko,

bali pia shamba ambalo tungelipata kuweza kupanua ili wananchi wetu wa pale barabara kuu ya Arusha - Moshi, tatizo hilo lingeweza kutatuliwa, mpaka leo bado! Kwa kweli naona kelele tunayopiga hapa na ninachotumwa na wananchi wangu inaonekana kwamba hazifiki. Sijui niseme nini tena na ninaona sasa hivi labda njia ya kusema zaidi ni kuondoa shilingi na niko radhi kuiondoa mpaka nitakapoona kwamba nimepata majibu ya kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu ahadi ambazo zilitolewa wakati wa kampeni. Kuna ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni kuhusu mkakati wa kuboresha nyumba zetu, nyumba bora Tanzania. Ahadi hizo zilitolewa kwenye ngazi ya juu sana na tukaona aah kweli, miaka mitano ijayo tutaanza kuona dalili, tukaona mfano Chamwino ukatokea mradi ambao ulijenga nyumba nafuu, lakini sikuona ule mradi kuendelea! Sijaona mkakati katika bajeti zote zilizopita ambao pia ni pamoja na huu unaoonyesha kwamba kuna dalili za kutaka ku-*address* hili suala la nyumba bora. Je, tunaridhika na hali yetu kama ilivyo? Naomba hili pia nalo lifikiriwe, kuwe na mkakati wa kuwawezesha wananchi wetu wawe na nyumba bora. Kwa mfano, *mortgage finance* ilienda wapi? Baada ya *THB* kufa, ni nini kilichokuwa badala yake?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu ndege ya Rais. Nadhani hili suala lilishazungumzwa hapa Bungeni. Mheshimiwa Rais wetu kuwa na ndege siyo anasa, Mheshimiwa Rais wetu kusafiri kwenye chombo ambacho kina uhakika wa maisha yake ni sifa kwa nchi yetu. Nchi ndogo kuliko Tanzania na labda maskini kuliko Tanzania, Rais wao ana ndege nzuri na yenye uhakika, Tanzania hatuna! Nadhani mpaka sasa hivi hatuna! Hiyo ndege mbona haijanunuliwa mpaka leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona mahali fulani kwenye vitabu vya bajeti ambapo *Government Aircraft* inaonyesha kwamba, itakuwa inaleta karibu shilingi bilioni 4. Je, hiyo ina maana kwamba iliyopo itauzwa na je, hizo fedha zitaenda wapi? Je, ndiyo moja ya mbinu za kutafuta fedha za kununua hiyo ndege ya Mheshimiwa Rais? Suala hilo lipewe kipaumbele na mwaka huu tuone ndege ya Mheshimiwa Rais inanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu kodi ya maendeleo na ni vipi tuweze kufidia Halmashauri zetu. Mapendekezo kadhaa yametolewa, binafsi naona ni mazuri, lakini pia naomba niongeze jambo moja. Mwaka 2002 tulifanya sensa ya watu, hizo *data* za sensa ziko kwenye Wizara ambazo ndizo zimetoa hizi hoja. *Data* hizo zinaonyesha kwa kila Wilaya wananchi ambao wana uwezo wa kulipa kodi. Wananchi hawa wanafahamika na hizi Wizara ndiyo ambazo zingetazamiwa kwamba, kuanzia Julai 1 mwaka huu wa 2003, wangelipa kodi za maendeleo kwenye maeneo yao na Halmashauri zao, basi *data* hizo ndizo zitumike kwa kila Halmashauri. Ifahamike kwamba, kila Halmashauri, kwa mfano, Arumeru ilikuwa wanatoza Sh. 4,000/= kwa kila mwananchi mwenye uwezo na anayestahili kulipa kodi ya maendeleo, basi watumie hizo *data* kufanya *estimate* kwamba, Halmashauri ya Arumeru wapate kiasi gani, badala ya kutumia *historical data.* Hilo ni mojawapo ya ombi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuhusu *management* ya *liquidity* katika uchumi wetu. Nadhani *issue* ya kuwa na fedha nyingi katika *Commercial Bank, Non Finance Institutions*, ninavyoona kwenye vitabu na pia makabrasha ya Benki Kuu inaonyesha kwamba limekuwa ni tatizo kwa muda na sijaona ni mkakati gani ambao umewekwa ku-*address* hii *issue*. Naomba watueleze wanatazamia kutatua tatizo hili vipi. Nadhani hii ni kazi ya *Bank of Tanzania,* lakini pia ni suala ambalo linahusu *Central Government.*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tofauti kati ya *saving deposit rates,* yaani riba tunayopata sisi tunaowekeza kwenye *savings deposit* na *landing rates* kutoka kwenye *Commercial Banks* ni kubwa mno kiasi ambacho kinatuogopesha. Inaonyesha kabisa kwamba, huu uchumi huenda unakuwa *managed,* lakini sijui unakuwa *managed* kivipi? *Deposit rate* sasa hivi *in real sense* ni *negative*, maana ukichukua *inflation rate* kwenye *four point something, savings deposit rates* nadhani iko kwenye *one point something,* ina maana kwamba *real rate* ni *negative*. Kwa kweli tunapoteza fedha zetu kwa kuwekeza katika *Banking Sector.* Kwa hiyo, jinsi tunavyo-*manage* uchumi wetu sasa hivi inatu-*discourage* tusiweze ku-*save* fedha zetu. Kwa kweli suala hili linahitaji kuwa *addressed* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Napenda kumsaidia Mheshimiwa Talala Mbise, kuhusu utaratibu ni kwamba, hiyo shilingi uliyotishia kuikamata huwezi kuikamata katika hoja hizi zilizopo mbele yetu, itabidi usubiri Wizara zinazohusika hapo ndiyo utaweza kufanya hilo unalolikusudia. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. FRANK G. MAGOBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho, ambayo binafsi naiita ni nafasi ya heshima kubwa kwangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niwapongeze Mawaziri wote wawili, wa Fedha na wa Mipango na Ubinafsishaji, Manaibu wao, Makatibu wa Wizara hizo na pia Watendaji wa Wizara hizo, kwa kufanya kazi nzuri ya kuandaa bajeti ambayo itatusaidia katika kutekeleza kuinua uchumi wa nchi yetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa katika kipindi kifupi kilichopita katika Majimbo mbalimbali. Naomba niwape pole kwa kampeni walizofanya na baada ya kuingia hapa naomba tuwe nao pamoja ili tuweze kuchangia mawazo yetu kwa ajili ya kuinua uchumi wa Taifa letu na kuwasaidia Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nijongee kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Katika hotuba hiyo Waziri amezungumzia mipango mingi ambayo inakusudiwa kutekelezwa katika kipindi cha bajeti tuliyonayo sasa hivi. Mipango hiyo ni pamoja na kutengeneza barabara, madaraja, mambo ya kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapa pongezi Mawaziri hao, kidogo nina wasiwasi hasa katika suala la utekelezaji. Katika Jimbo langu kuna suala la daraja la Kigamboni, sijasikia likizungumzwa kwenye mipango ya Waziri. Sijui kama nimepitiwa, lakini ninaamini kwamba sijasikia. Nilitegemea kabisa katika mipango yake basi hilo lingekuwa ni suala moja kubwa ambalo lingezungumzwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, ninachojiuliza ni kwamba, ni kwa nini suala hili asirudie kulizungumza kila mwaka, kuna nini? Suala la daraja la Kigamboni si kwamba linajengwa kwa faida yangu binafsi, ni kwa faida ya nchi yetu ya Tanzania na kwa Wananchi wote ambao wanaishi kule. Sasa ni kwa nini iwe ni *issue* ya kila mwaka tunazungumzia daraja la Kigamboni, kuna nini hasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kulitumia daraja la Kigamboni kama kampeni ili nipate Ubunge mwaka 2005, nisingependa kufanya hivyo. Napenda Serikali itekeleze ahadi ambayo imekuwa ikiitoa kila mwaka. Hili suala la kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki linanitia wasiwasi na kama ni tatizo la pesa basi naamini Tanzania tunazo fedha za kutosha. Nasema hivyo kwa sababu kama tunaweza kuwalipa *IPTL* shilingi bilioni 3 kwa mwezi, tutashindwa vipi kujenga daraja la Kigamboni kwa fedha hiyo ya Tanzania ambayo tunawalipa *IPTL* ambao hawafanyi kazi ya aina yoyote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linasikitisha, kwa sababu tukisema hatuna fedha wakati kuna watu ambao tunawalipa na hawakufanya kazi, tunakuwa tunasema nini? Tunataka kuwaambia nini Watanzania? Naomba Waziri wa Mipango aangalie suala hili la ujenzi wa daraja la Kigamboni bila kuchelewa kwa sababu hili ni suala la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika Jimbo langu kuna Wananchi wengi wakiwemo Wabunge wamechukua viwanja vya kujenga nyumba baada ya Serikali kutangaza kwa Wananchi kwamba wakachukue viwanja. Watu wengi wamejitokeza kununua viwanja kule kwa ajili ya ujenzi, maeneo ya Kisota, Tuangoma na Mtoni Kijichi, lakini Wananchi hawa kama hatukuwatengenezea njia nzuri ya kufika huko itakuwa ni kazi bure. Si ajabu wakanunua viwanja hivyo na pengine visijengwe, kwa sababu watakuwa wanaogopa hakuna sehemu ya kuvuka. Siyo kwamba wote wanapenda kuvuka na pantoni,wangependa kuvuka kwenye daraja au kwa kutumia barabara. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, anieleze atakapokuwa ana-*windup. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu suala la barabara. Barabara ninayoizungumzia ni ya kutoka Chuo cha Uhasibu karibu na Uwanja wa Taifa kwenda mpaka Kongowe. Hivi karibuni Wananchi wangu wa Mbagala na maeneo ya Jimbo la Temeke walitekeleza agizo la Serikali la kubomoa nyumba zao bila masharti na wamebomoa bila tatizo lolote, lakini toka Wananchi hao wamepisha ujenzi wa barabara hiyo, inasikitisha kwamba haionyeshi kama kuna mpango wa kujenga barabara hivi karibuni. Ndiyo maana ninasema, hii mipango tunayoipanga tuangalie na athari zake, maana kama Wananchi walijitolea kuvunja nyumba zao na kutafuta maeneo mengine kwa kupisha ujenzi wa barabara, ni kwa nini sasa hiyo barabara isitengenezwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wananchi wananiuliza kwamba, mlituambia tubomoe nyumba na tumefanya hivyo, ni kwa nini sasa hii barabara haijengwi? Ninashindwa kuwajibu kwa sababu sina jibu kamili katika jambo hilo. Pia, kuna mambo kadhaa nitayazungumzia kwenye Bajeti ya Waziri wa Ujenzi, ambayo Wananchi walinituma niyaulizie. Naomba kwenye suala la barabara hiyo kama kuna mipango iliyowekwa nijulishwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kilimo, Waziri amezungumzia mipango mingi ya kilimo. Kama wenzangu walivyosema, inakuwa ni mipango ambayo inazungumzwa kwa muda mrefu kwamba kilimo ni uti wa mgongo na Watanzania wakitegemea kweli itakuwa hivyo. Lakini mara nyingi tunapopitisha Bajeti ya Kilimo, yale ambayo tunayaona kwenye vitabu hayatekelezwi.

Mheshimiwa Spika, tukubaliane na ukweli kwamba, tutakapokuwa tunazungumza mipango ya baadaye ambayo haitekelezeki, Watanzania ambao wanakuwa wanatusikiliza na kupata matumaini wanasikitika sana. Mara nyingi tunazungumza vitu ambavyo wanafikiri labda vingewasaidia, lakini wanashangaa havitekelezeki! Sasa, kila mwaka tunazungumzia Bajeti ya kilimo ambayo haitekelezeki. Nasikitika kwamba mwaka huu hakuna mvua za kutosha, sasa sijui tuna mpango gani kuhusu mambo ya chakula kwa nchi yetu, kwa sababu hali si nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika mipango ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, pia sikusikia suala la vitambulisho kwa Watanzania. Jambo hili linahusu usalama wa Taifa, kwa sababu sasa hivi Watanzania wamekuwa wanaishi kwa wasiwasi kutokana na matukio ambayo yamejitokeza hivi karibuni ya majambazi kuvamia hata Vyombo vya Serikali. Nilitegemea katika mipango hii suala la vitambulisho lingepewa kipaumbele, kwa sababu suala hili lipo kwa muda mrefu. Tulitegemea kwamba vitatengenezwa vitambulisho kwa Watanzania ili kutambulisha kwamba huyu ni Mtanzania na huyu ni mgeni.

Mheshimiwa Spika, leo hii tuna matukio chungu nzima ambayo yamejitokeza. Ninasikitika kwamba wanaofanya vitendo hivi ni watu kutoka nje ya nchi yetu na si Watanzania, labda kama wanashirikiana na Watanzania wachache. Naiomba Serikali ilipe kipaumbele suala la vitambulisho ili kuondokana na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, pia, nimpongeze Mheshimiwa Makamba, kwa tamko lake la hivi karibuni kwamba, sasa turudi kwenye suala la sungusungu. Kama tulikuwa tunalidharau basi tuchukulie umuhimu kwamba suala hilo ni la lazima na lifanye kazi kama tulivyokusudia. Suala hilo linatusaidia kuendelea kulinda maeneo ambayo Wananchi wanaishi na maeneo hayo Wananchi wa Tanzania wanafahamiana kwamba pale wanaishi watu fulani na pale wanaishi watu fulani. Katika mpango huo kungekuwa na utaratibu ambao Viongozi wengine wanafuatilia nadhani tungefika mbali. Kwa hiyo, suala la vitambulisho naomba lipewe kipaumbele ili Watanzania wajulikane na wageni wajulikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile uingiaji wa wageni wengi nchini umeongezeka. Wageni wanaingia kiholela tu kwa sababu hakuna udhibiti, lakini tukiwa na vitambulisho suala hili tutalidhibiti kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Makamba ya kutangaza kwamba saa tano iwe ni mwisho wa baa kutumika. Lakini pamoja na hali hiyo, wale Watendaji ambao tumesema kwamba tutawalipa mishahara, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Viongozi wote wa Mitaa wawe na ushirikiano wa kuhakikisha kwamba ulinzi katika maeneo yao unakuwa wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, binafsi niliwahi kufanya ulinzi wa sungusungu katika maeneo ya Kwamangaya, Charambe na maeneo kadhaa kwa muda wa siku tisa na nilifanikiwa kuwakamata vijana wengi ambao walikuwa ni wasumbufu wakubwa. Nilipata ushirikiano mkubwa japo kuna baadhi walikuwa wanabeza suala la ulinzi wa sungusungu wakidhani kwamba hizo zilikuwa ni Sera za *CUF*! Niliwaambia kwamba, si kweli suala la sera hapa halipo, tunachoangalia ni usalama wa nchi yetu na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama ilikuwa ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, binafsi niliona ni nzuri, kwa sababu ilikuwa inalenga ulinzi wa Wananchi ambao tunawaongoza. Kwa hiyo, sikuona tatizo la kutekeleza hiyo sera yao. Sasa kama tunasema ni sera nzuri, basi Chama cha Mapinduzi na Serikali iliyopo madarakani tuikazanie sera hiyo ifanyike, tusiseme tu sera, sera ambayo hatuwezi kuitekeleza. Naomba suala hilo likazaniwe ili kuhakikisha kwamba, ulinzi katika maeneo yetu unaimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba, kwa sababu Wizara yangu ya Mambo ya Ndani ya Nchi, angalau sasa hivi tumepata ahueni ya fedha za kutosha. Mheshimiwa Mramba, amenifurahisha alivyotangaza kuipa Wizara ya Mambo ya Ndani kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba matumizi hayo kweli yalenge kule ambako tumekusudia, yasiende kinyume na tulivyopanga. Kama kuna magari yanatakiwa yanunuliwe, kama ni silaha zinunuliwe, kama ni *radio calls* zinunuliwe na kama ni ujenzi wa nyumba za Askari wetu ambao wanaishi kwenye nyumba za *full suit,* ambazo ni za mabati zijengwe, pasiwepo na ubabaishaji tena katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli bajeti hii imenifurahisha sana kwa sababu tulikuwa tunapiga sana kelele. Naamini Wabunge tukipiga sana kelele Serikali inasikiliza. Sasa hivi naamini kwamba, tuliyoyasema katika kipindi cha bajeti iliyopita au vikao vingine, Serikali imechukulia uzito na kuipa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi fedha za kutosha kuhakikisha inapata vifaa ambavyo vilikuwa vinakosekana. Hata kama havitatosha, lakini angalau tutakuwa tumepunguza idadi kubwa ya vitu ambavyo tulikuwa tunakosa katika ulinzi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kupoteza muda mwingi, kwa kuwa binafsi ni msemaji wa mwisho, napenda kurudia tu kuwapongeza Wabunge wote, waliotoa

michango yao katika bajeti hii, kwa kuonyesha umoja wao katika Bunge hili bila kujali mtu anatoka wapi wala ni mtu gani. Ninaamini kwamba, humu ndani wote ni familia moja, watoto wa baba mmoja, mama mmoja, japo kuna mambo kidogo tunatofautiana, lakini tunachojali hapa ni maslahi ya Taifa letu na kujenga nchi yetu ambayo ni Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa mjadala wa jumla. Napenda kuwashukuru wote kwa ushirikiano mzuri uliowezesha ratiba yetu kwenda kama ilivyopangwa na ratiba ya kesho nimeshawajulisha. Kwa hiyo, ili tujiandae vizuri kwa kesho, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 12.53 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 20 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*